

# Kukua au Kufa

**Mfululizo wa Semina  
Sehemu ya 1 – Kukua au Kufa  
Sehemu ya 2 – Damu na Moto**



Kitabu cha Mwongozo wa Uanafunzi wa Yesu

**Kozi ya mwanzo kwa ajili ya kuishi na kuzaa  
matunda katika ufalme wa Mungu  
kwa ushindi na malengo**

International School of The Bible (Shule ya Kimataifa ya Biblia)  
Na Larry Chkoreff

# Kukua au Kufa – Mfululizo wa Semina

Na Larry Chkoreff

Jina la Kitabu la asili: Grow or Die  
Kimetafsiriwa na: Christopher Frank  
Kimehaririwa na: Rev. Masalu  
Revised January 2013

Kukua au Kufa kimechapishwa na International School of the Bible –ISOB (Shule ya Kimataifa ya Biblia), Marietta, GA USA. Kitabu hiki ni mtaala wa uanafunzi wa Yesu katika shule hii.


Barua Pepe: book@isob-bible.org

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

Kitabu hiki ni mali ya International School of the Bible. **Kinaweza kuchapishwa tena, iwapo tu kitachapishwa chote, kwa ajili ya kukisambaza bure** (bila malipo). Hairuhusiwi kukibadili au kukihariri kwa njia yoyote ile. Kikichapishwa tena ni lazima kiwe na tangazo la haki miliki (“Copyright © 1999 ISOB”).

Kitabu hiki kisiuzwe (au kutumika kutangazia ubora wa bidhaa yoyote iliyokwishauzwa) bila ruhusa ya International School of the Bible (ISOB).

## Kukua au Kufa Njia ya Mwamini katika Kristo



## **Yaliyomo**

## **Ukurasa**

<b>UTANGULIZI</b>	<b>6</b>
<b>SEHEMU YA 1 – SEMINA YA 1</b>	<b>11</b>
<b>SURA YA 1 - MATUNDA</b>	<b>12</b>
<b>SURA YA 2 - MTO UTIRIRIKAO</b>	<b>22</b>
<b>Kiambatisho F</b>	<b>38</b>
<b>SURA YA 3 - WAFUNGWA KATIKA NCHI YA AHADI</b>	<b>44</b>
<b>SURA YA 4 - MUNGU NI NANI</b>	<b>52</b>
<b>SURA YA 5 - KUKETI</b>	<b>62</b>
<b>SURA YA 6 - KUENENDA</b>	<b>73</b>
<b>SURA YA 7 - KUPINGA</b>	<b>79</b>
<b>SEHEMU YA 2 – SEMINA YA 2</b>	<b>90</b>
<b>SURA YA 8 – NGUVU YA KUPIGA MBIO KATIKA MASHINDANO – UTANGULIZI</b>	<b>91</b>
<b>SURA YA 9 - NGUVU YA KUPIGA MBIO KATIKA MASHINDANO – MSALABA</b>	<b>94</b>
<b>SURA YA 10 - NGUVU YA KUPIGA MBIO KATIKA MASHINDANO - UKOMBOZI</b>	<b>117</b>
<b>SURA YA 11 - NGUVU YA KUPIGA MBIO KATIKA MASHINDANO – UBATIZO KATIKA ROHO MTAKATIFU</b>	<b>126</b>
<b>KIAMBATISHO A – ORODHA YA MASOMO YA ISOB</b>	<b>137</b>
<b>KIAMBATISHO B – JINSI YA KUENDELEA KATIKA ISOB</b>	<b>141</b>

Mpendwa msomaji:

Baada ya kumfuata Yesu kwa shauku, tangu mwaka 1979, ameniagiza kuandika mambo aliyonitendea siku hadi siku. Ingawa hakuna njia ya mkato ya kuzaa matunda, au ya kukuza uhusiano wako na Yesu, kuna kanuni ambazo nimejifunza zinazoweza kukuondolea miaka mingi ya maumivu na hali ya kukata tamaa katika maisha yako.

Kitabu hiki ni muhtasari wa yale yaliyomo katika kozi inayohusu Kukua au Kufa, ijulikanayo kama “Mfululizo wa Semina”. Kina semina mbili. Semina ya 1 (Sehemu ya 1) ina “masomo saba ya mwongozo.” Semina ya 2 (Sehemu ya 2) ina masomo manne ya ufuatiliaji. Masomo haya 11 yamechukuliwa kutoka katika kozi kamili ya Kukua au Kufa yenyе masomo zaidi ya 90.

Kozi yote ya Kukua au Kufa inapatikana kwa mtu binafsi na/au vikundi kwa ajili ya kuwafundisha watu. Baadhi ya masomo hayo yanaendelea kutafsiriwa kwa lugha ya Kifaransa na Kihispania.

Baadhi ya vikundi vimeanzisha shule zinazotoa ushauri (katika nchi kadhaa duniani). Shule hizi huitwa “International School of the Bible” (ISOB), yaani Shule ya Kimataifa ya Biblia. Baadhi ya vikundi hutumia masomo haya wakati vinapokutana ili kujifunza kwa pamoja. Na watu binafsi wamekuwa wakijifunza wenywewe.

Kozi ya Kukua au Kufa kwa sasa inatolewa kama semina kwa Wainjilisti katika nchi kadhaa. Semina hizo huchukua kati ya masaa 4 hadi masaa 14.

Tungefurahi kukusaidia na wewe uanzishe mahali pa kutolea ushauri au mafundisho. Katika hali ya kumuomba Mungu, tutatafakari pia ombi au hitaji la kufanyiwa semina katika eneo lako.

ISOB haidai matipo kwa masomo yake nje ya gharama za kuyatoa au kuyachapisha kwa mara ya pili. Masomo haya hupatikana pia katika diskii (CD ROM) kwa ajili ya kompyuta za “Windows” na “Macintosh” kwa bei nafuu.

Tunakubariki katika safari yako na Yesu.

Larry Chkoreff

Rais

International School of the Bible (Shule ya Kimataifa ya Biblia)

**Kitabu hiki ni kwa heshima ya rafiki yangu kupita wote, mke wangu  
nimpendaye sana, mcha Mungu, Carol, ambaye kwa miaka mingi  
amenitia moyo kuandika masomo haya, na hatimaye kuyaweka pamoja  
katika kitabu.**

Shukrani maalum zimwendee ndugu Jim Crawford wa “Project Light” ambaye amekuwa rafiki wa thamani sana na mfariji katika kazi hii.

**Ninaomba sala hii kwa kila mtu atakayesoma kitabu hiki.**

**Msalaba** Asante Bwana kwa ushindi wa msalaba wa Yesu Kristo.  
Asante kwa kuwa tulisulibiwa na wewe

**Kuzimu** Asante Bwana kwa kuvumilia mateso na kifo na kushuka  
hadi kuzimu kwa ajili yetu.

**Ufufuo** Asante Bwana kwamba ulifufuliwa kutoka katika wafu, na  
kwamba sisi nasi tulifufuliwa pamoja na wewe na kuketi  
pamoja na wewe katika ulimwengu wa roho, ndani yako  
Kristo.

**Ujazo** Asante Yesu kwa kutujaza Roho Mtakatifu

**Mateso** Asante Yesu kwa kuona kwamba tunastahili kushiriki mateso  
yako.

**Ushindi** Asante Bwana kwa ushindi uliotuahidia katika maisha haya  
na yale ya milele.

## Utangulizi

**Je umewahi kujisikia huna malengo au matumaini?** Umewahi kujisikia kana kwamba uko juu ya gurudumu kama fuko ndani ya kizimba lakini huendi popote? Umewahi kujiuliza ni kwa vipi Mungu anatazamia uishi maisha ya ushindi. Unawenza kujisikia kwamba Mungu atakupeleka mbinguni siku fulani, lakini unaona kana kwamba Mungu amekuacha bila msaada. Sawa, kama umekuwa katika hali hiyo, fahamu kwamba hata watu wanaomwamini Yesu Kristo hujisikia hivyo mara kwa mara.

**Wakati mwingine inaonekana kwamba lengo letu** ni kujaribu kupata ushindi au mafanikio katika maisha kwa nguvu zetu wenyewe. Kwa mama mzazi, lengo lake linakuwa ni kuwafundisha watoto wake wamche Mungu, kuwalisha na kuwatunza. Kwa mke, lengo linakuwa ni kutafuta kuwa karibu na mume wake na kuwa salama na kuwa na mawasiliano mazuri. Kwa mume, lengo lake mara nyingi ni kujaribu kuilisha familia na kujaribu kuonekana mtu wa maana, anataka wengine wamstahii. Kwa kijana, lengo lake linaweza kuwa ni kutafuta kujua nafasi aliyo nayo katika jamiii ni ipi, kutafuta kazi na mwenzii wa maisha. Na mara nyingi lengo letu ni kujaribu kutatua matatizo mbalimbali katika maisha. Hata hivyo, mambo haya yakifanikiwa mara nyingi ~~hivyo tunajisikia watupu bila kuwa na lengo jingine zaidi, au yasipofanikiwa huwa tunajisikia kukata tamaa na kukosa matumaini.~~

**Jibu ni nini?** ~~Kama Neno la Mungu linavyosema katika Wagalatia 2:20, tukisulibiwa pamoja na Kristo na Kristo akiwa hai ndani yetu, basi hatutajisikia vizuri mpaka pale tutakapolefanya lengo la Mungu kuwa lengo letu.~~

**Naamini kwamba Mungu ana malengo mengi kwa ajili yetu katika maisha. Hata hivyo, malengo yake yote yako chini ya lengo moja kubwa na la msingi: KUMLETA BIBI ARUSI KWA YESU.**

**Kitabu cha Waefeso kinatupa ufahamu.** Katika Waefeso 4:11-13 Paulo anaonyesha kwamba lengo au makusudi kamili ya huduma ni kuujenga mwili wa Kristo ili uifikie "cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." Katika Waefeso 4:12b tunajifunza kwamba tunatakiwa kuujenga Mwili wa Kristo. Na katika Waefeso 5:25-27 tunaona kwamba pamoja na kumleta bibi arusi kwa Kristo, Yesu anataka bibi arusi wake asafishwe ili atakapopelekwa kwake awe mtakatifu asiye na mawaa.

**Mwili au Kanisa ni bibi arusi wa Kristo.** Neno la Mungu katika Waefeso 5:32 linazungumzia juu ya siri ya Kristo na kanisa kwamba inafanana

na mume na mke. Mstari huo unasema hivi: "Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa."

**Arusi ya Mwanakondoo na bibi arusi inaonekana** kuwa ni mojawapo ya matukio ya mwisho karibu na mwisho wa Kitabu cha Ufunuo wa Yohana. Katika Ufunuo wa Yohana 19:7 tunasoma maneno yafuatayo: "Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari."

**Hii haimaanishi kwamba sisi sote tunahitaji kwenda nchi za nje** na kuhubiri katika mitaa kama mwijilisti. Hapana, kila mtu amepewa karama na Mungu kwa njia ya kipekee. Kazi (ya kumleta bibi arusi kwake) aliyotupatia tunaweza kuifanya. Kila mtu ana umuhimu wake. Fikiria jambo hilo. Kama kuna mtu mmoja tu anayepaswa kuwa bibi arusi mionganoni mwa Kanisa lakini bado hajafanya hivyo, basi bibi arusi hajakamilika. Kwa kuwa bibi arusi anahitaji kuendelea kukua mpaka awe mtu mzima, basi kazi yetu haijakamilika. Mungu anaweza kukuuta uombe, au umpende jirani yako, au uende nchi ya mbali. Ni Mungu tu anayejua mambo aliyo nayo kwa ajili yako.

Tunapaswa kujiona kama chembe ya mchanga ufukweni. Ni kama vile hatuonekani, hata hivyo, bila sisi, ufukwe haujakamilika. Mungu anatuhitaji tufanye sehemu yetu.

### **Agano la Kale linatupa picha ya moyo wa Mungu jinsi anavyojisikia kuhusu jambo hili.**

**Hawa alitoka katika ubavu wa Adamu.** Kanisa lilitoka katika ubavu wa Kristo pale msalabani.

**Angata Mwanzo 24.** Ibrahimu (mfano wa **Baba**) anamtuma mtumishi wake (mfano wa **Roho Mtakatifu** – aliye ndani yako na ndani yangu) kutafuta mke kwa ajili ya mtoto wake Isaka (mfano wa **Yesu**).

Maneno ya Mungu katika **Mwanzo 24:4-9** yanasema, “bali enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu, ukamtwalie mwanangu Isaka mke. Yule mtumishi akamwambia, Labda yule mwanamke hatakubali kufuatana nami mpaka nchi hii, je! Nimrudishe mwanaao mpaka nchi ulikotoka? Ibrahimu akamwambia, Ujihadhari, usimrudishe mwanangu huko. BWANA, Mungu wa mbingu, aliyenitoa katika nyumba ya babangu, na kusema nami katika nchi niliyozaliwa, aliniapia akisema, Nitawapa uzao wako nchi hii; ye ye atampeleka malaika wake mbele yako, nawe utamtwalia mwanangu mke tokea huko; na yule mwanamke asipokubali kufuatana nawe, basi, utafunguliwa kiapo changu hiki; lakini usimrudishe mwanangu huko. Yule mtumishi akaweka mkono wake chini ya paja la Ibrahimu bwana wake, akamwapia katika neno hilo.”

Soma habari yote hiyo katika Mwanzo 24. Yule mtumishi akampata Rebeka, aliye kuwa akiwanywesha maji ngamia, na kisha akampa maji ya kunywa alipofika katika eneo lile. Hii ilitokea “kabla hajamaliza kuzungumza” (sura ya 24: 15). Na kabla hajatamka yale maneno, Rebeka alijitokeza akatimiza yale maneno.

Katika **Mwanzo 24:64-67** tunasoma maneno yafuatayo: “Rebeka akainua macho, naye alipomwona Isaka, alishuka juu ya ngamia. Akamwambia mtumishi, Ni nani mtu huyu ajaye kondeni kutulaki? Mtumishi akasema, Huyu ndiye bwana wangu. Basi akatwaa shela yake akajifunika. Yule mtumishi akamwambia Isaka mambu yote aliyoyatenda. Isaka akamwingiza Rebeka katika hema ya mama yake, Sara, akamtwa Rebeka, akawa mkewe, akampenda; Isaka akafarijika kwa ajili ya kufa kwa mamake.”

**Hiyo ni njia nzuri ya kupata picha ya moyo wa Mungu!** Baba alikusudia kupata mke kwa ajili ya mtoto wake, lakini siyo mke tu bali yule aliyekuwa katika jamii ile ile ya mtoto wake.

**Huenda unajiuliza swalii hili: Ni kwa vipi Mungu anatazamia nishiriki katika huduma ya kumleta bibi arusi, wakati mimi mwenyewe siwezi hata kuyafanya maisha yangu yawe mazuri?**

**Nafurahi kwamba umeuliza. Hilo ndilo suala tutakalozungumzia katika kitabu hiki**

**Tunahitaji kujua aina ya mtumishi aliyetumwa na Ibrahimu kumtafuta mke**

“Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake, aliyetawala vitu vyake vyote, Tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu.” (Mwanzo 24:2).

Angalia, Ibrahimu hakumtuma mtumishi ye yote tu. Alimtuma yule aliyetawala vitu vyake vyote. Katika kitabu cha Mathayo 24 tunapata habari ya mtumwa aliyevekwa juu ya vitu vyote. Hebu tuone mambo tunayoweza kujifunza kwake. Habari yewewe ipo katika Mathayo 24:42-51.

**Kwanza, mtumwa yule aliweka tayari kwa ujio wa Bwana wake.** Hii inamaanisha kwamba tunapaswa kujiveka tayari kumlaki Yesu atakapokuja tena duniani, lakini pia tunapaswa kuwa tayari kumlaki Yesu sasa anapokuja kuangalia jinsi tulivyo waaminifu kuyatunza yale tuliyopewa.

**Mtumwa alikuwa mwaminifu.** Kuwa mwaminifu katika madogo ni jambo muhimu kwa Mungu. Mungu anapenda kujua jinsi tunatenda mambo yetu ya kila siku katika maisha yetu. Mungu hawezi kutupatia zaidi mpaka kwanza tuwe waaminifu kwa madogo aliyotupatia. Tunahitaji kuwa waaminifu katika mambo ya kimwili na mambo ya kiroho.

**Mtumwa alikuwa pia mtoaji.** Aliwapa watu wengine chakula. Katika Mathayo 24:46 imeandikwa hivi: “Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo.”

**Mtumwa hakuwatenda vibaya wengine.**

**Mtumwa hakuishi kama watu wasioamini.**

**Mtumwa alikuwa na hekima.** Ni wazi kwamba hekima hii siyo ya dunia, ni hekima ya Mungu.

Katika 1 Wakorintho 2:6-8 tunaambiwa hivi: “Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenyewe kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangalijua, wasingalimsilibisha Bwana wa utukufu.”

Katika 1 Wakorintho 1:23-24 tunaambiwa kwamba Kristo aliyesulibiwa, ni hekima.

**Naamini, kwamba hekima ya kweli kutoka kwa Mungu imehifadhiwa kwa ajili ya wale** waliopita katika mauti. Imehifadhiwa kwa ajili ya wale waliopoteza matumaini, maono, ndugu zao, kazi, heshima na kadhalika. Kitabu cha Ayubu sura ya 28 kinazungumzia kutafuta hekima. Kwamba hekima haionekani katika nchi ya walio hai. Hii inamaanisha kwamba mauti tu ndiyo imeiona. Yule tajiri katika Mathayo 19 alikuwa na mengi ya kutumainia katika dunia.

**Unapojuwa kwa hakika kwamba “mfumo wa dunia”** na juhudi zako mwenyewe hazitoi matumaini, basi wewe unaweza kupata hekima. Ukiangukia katika kundi hili, nyanya kichwa chako kwa matumaini, kwa kuwa Mungu atakutendea mambo ya kupita kawaida!

**Maisha yanaweza kuwa magumu, lakini tunaweza kuishi kwa ushindi tukimwangalia Yesu siku zote.**

**Watu, wahudumu, marafiki, au hata makanisa yanaweza kutukatisha tamaa,** lakini Yesu hawesi kufanya hivyo kamwe. Katika Waebrania 2:8-9 tunaambiwa kwamba hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake, ila twamwona Yesu aliyesonja mauti kwa ajili yetu. Tunapotambua yale aliyoyafanya Yesu kwa ajili yetu na kujua Yeye ni nani, tunampenda.

**Tunapompenda,** tunaridika kujua kwamba tunaishi kwa ajili ya makusudi yake na kwamba jambo hilo inampendeza.

**Jambo zuri ni** kwamba tunapopita katika satua hii, tunamwangalia Yesu wakati wote, tunatenda kazi kwa ajili yake, tunapita katika majaribu kwa ajili yake na kumtumikia. Wakati macho yetu yanapomwangalia, Yeye anakuwa thawabu yetu. Hatuhitaji kuangalia jinsi ya kubadili tabia, au jinsi ya kutimiza mahitaji yetu, au hata huduma. Tunatakiwa tu kumwangalia Yeye na kuunganishwa naye. Tunaiona “neema ya ajabu” ya Mungu ikitufunika. Napenda kukuambia kutokana na uzoefu wangu kwamba jambo hili huweza kumfanya mtu astahimili nyakati ngumu katika maisha na kuwa na furaha.

**Sasa tunahitaji kujifunza jinsi Baba alivyomtenda yule mtumishi wake, na kutazamia jinsi Mungu atakavyotutenda sisi.**

**Ninamwona Baba akimruhusu mtumishi wake azae matunda kwa njia tatu.**

1. **Tunda la Roho.** Mtumishi huyu alikuwa na tabia ya Mungu.
2. **Tunda la kutimiziwa mahitaji yake yote.** Katika Mwanzo 24:10 utaona kwamba Baba alimpa yule mtumishi yote aliyoyahitaji kwa ajili ya safari, siyo tu ngamia 10, bali mambo yote aliyoyahitaji.
3. **Tunda la huduma.** Mtumishi huyu alishiriki kumpendeza baba na Mwana kwa kumleta nyumbani bibi arusi.

**Hayo ndiyo mambo yanayohusu uanafunzi wa Yesu na ndiyo yaliyozungumzwa katika kitabu hiki.**

**Kuzaa matunda katika maisha yetu kwa ajili ya ufalme wa Mungu katika maeneo yote hayo matatu. Ubarikiwe.**

*Reproduction, local or internet posting prohibited*

## **Sehemu ya 1 – Semina ya 1**

**Sura ya 1-7 zinazungumzia:**

1. **Tunda**
2. **Mto Utirikao**
3. **Wafungwa katika Nchi ya Ahadi**
4. **Mungu ni nani**
5. **Kuketi**
6. **Kuenenda**
7. **Kupinga**

## Sura ya 1 - Matunda

Je, umewahi kujuliza maswali haya: Mungu anatarajia kwamba nitapata ushindi kwa njia gani hapa duniani? Ninapaswa kuishi namna gani? Kwa nini sipati ushindi mkubwa zaidi? Iwapo Mungu yupo kwa ajili yangu, kwa nini basi maisha yangu hayaonyeshi hivyo? Nimesikia juu ya nguvu za Mungu, lakini labda alinisahau mimi alipokuwa akiwapa wengine nguvu zake. Katika Yakobo 2:5 imeandikwa hivi: "Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Je, Mungu hakuwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao?" (maana ya neno maskini ni: mtu asiye na mali, uwezo, kazi, heshima, anayeishi bila msaada, asiye na nguvu ya kutimiza lengo lake, ombaomba, anayeomba sadaka).

Sisi sote tunayo mahitaji halisi. Makubwa kati ya hayo ni haya: upendo, usalama na umuhimu. Ndani ya mahitaji hayo, tunayo mahitaji mengine yaliyo wazi zaidi. Baadhi ya watu wanahitaji chakula na mavazi, wengine wanahitaji watoto wao wamjue Mungu, wengine wanahitaji kuponywa magonjwa, na mahitaji mengine kadha wa kadha.

### Vyakula na mahitaji yetu yapo katika uwepo wa Mungu

Biblia *Romans 8:14-17*, katika Wafilipi 4:19 kwamba, "Na Mungu wangu atawajazeni kila unachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Iwapo Mungu anakwenda kukujaza kila unachokihitaji katika "utukufu", inabidi utafute mahali utukufu wake ulipo, na kisha umngojee Mungu kwenye utukufu huo. Vingineyyo huenda unamngojea Mungu mahali pasipostahili. Nikingojea basi katika stesheni ya treni, siwezi kulipata. Inabidi nitafute mahali kituo cha basi kilipo! Sisi nasi tunatakiwa kutafuta mahali utukufu ulipo. Neno "utukufu" linapohusishwa na Mungu linamaanisha uwepo wake. Tunahitaji kwenda katika utukufu wake, kumsikiliza anaponena nasi Neno lake. Neno lake hugeuka kuwa ahadi na mbegu iliyopandwa katika mioyo yetu na hatimaye itazaa matunda **kama** tutaitunza vizuri mbegu hiyo.

**Adam aliumbwba ili azae matunda, sisi je?**

**Tunahitaji kubadili mwelekeo wa juhudini zetu katika yale ambayo tumekuwa tukifanya, na tuongeze nguvu katika kuzaa matunda**

### Kuzaa matunda ndilo jambo muhimu kwa Mungu

"Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu" (Yohana 15:8).


"Mungu akawabarikia, akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. Mungu akasema, Tazama nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mtu, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu." (Mwanzo 1:28-29).

**Yesu alikuwa akituambia tubadilike, tutubu hali ya kujitahidi sana  
kujitosheleza kimahitaji, tuwe wazaaji wa matunda.**

"Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia." (Mathayo 4:17). Huko ndiko kubadili mwelekeo. Utakapofanya hivyo, utaona ufalme wa Mungu uko karibu nawe sana kiasi kwamba unaweza kuushika.

Huenda unauliza, alikuwa anamaanisha nini? Tuache nini? Ufalme wa Mungu ni nini? Ninaamini kwamba tunapaswa kuacha njia za kidunia za kuishi maisha na badala yake tufuate njia ya ufalme wa Mungu. Naamini kwamba jambo hili linahusu maisha yetu yote. Naamini pia kwamba Yesu hakuwa akiwaambia tu watu hawa, "acheni kufanya dhambi na pia tubuni njia zenu mbaya." Hapana, Yesu alikuwa akitupatia mpango wa jinsi ya kuishi.

**Wanadamu hutumia kanuni zote za kidunia na za kujitosheleza wao wenyewe ili kutimiza mahitaji yao. Mahitaji yetu ya msingi ni upendo, usalama na umuhimu(kuwa watu wa maana).**



**Je, Petro hakuandika kwamba ahadi za Mungu zinatukirimia vitu vyote kwa ajili ya uzima na utauwa? Soma 2 Petro 1:3-4.**

**Watu wanaposhindwa kutimiza mahitaji yao** hawataki kuukubali ukweli huu kwamba dunia kamwe haitawapa mahitaji yao. Wanajaribu kuziba pengo kwa kujitahidi kujiendeleza wenyewe, wakitumaini kuwa mambo yatakuwa mazuri. Hufikiri kwamba lazima kuna kosa fulani katikati yao. Hatimaye hujiona wana hatia na kuanza kuzifikiria vibaya tabia za Mungu. Shetani naye huzidi kuwadanganya na wao hukubaliana na uongo wake. Na kisha huona mashaka juu ya ukweli wa Neno la Mungu.

**Kwa hiyo jibu ni nini?** Tunawezaje kuupata ufalme wa Mungu kwa kugeuka au kuacha njia fulani? Yesu alisema katika Marko 4:11 kwamba **siri**

ya ufalme wa Mungu imefunuliwa katika mfano wa kupanda na kuvuna. Kupanda na kuvuna nini? **Kupanda na kuvuna Neno la Mungu!**

### **Matokeo ya mwisho ya kulima ni kupata matunda**

**Yesu alisema katika Marko 4 kwamba ufalme wote wa Mungu** hufanya kazi katika kanuni hii. Alisema kwamba hii **ni** siri ya ufalme. Siri ni ipi? Kwamba maisha huendelezwa na Neno la Mungu lililopandwa katika moyo wa mtu. Halafu kinachofuata ni hatua za kukua. Pamoja na ukuaji huo kuna maumivu. Maumivu yanayotokana na Shetani anayejaribu kuliiba Neno wakati unapomongojea "Bwana arudi" na matunda.

**Anasema kwamba tunahitaji kuwa watu wanaotegemea Neno,** wasiojitegemea, wala kuutegemea ulimwengu. Njia ya kumtegemea Mungu ni kutegemea nguvu ipitayo kawaida ya Neno la Mungu!

**Hatuhitaji kuwa wajuzi sana katika kuyashughulikia maisha kama jinsi tunavyohitaji kuwa wajuzi katika kushughulika na Neno la Mungu.**

**Kwa maneno mengine tunasema:** **tubu** (yaani, acha yale unayoyaamini na kuyategemea kwa ajili ya mahitaji yako mazito, acha kujitegemea mwenyewe na kuutegemea mfumo wa dunia) kwa sababu Ufalme wa Mungu (yaani utaratibu wa Mungu ulioelezwa katika Marko 4 wa kupanda mbegeu ya Neno la Mungu katika moyo wako, na kuiacha ikue ili izae kila kitu unachohitaji kwa ajili ya maisha na utauwa, na kwa kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu) sasa uko karibu nawe.

**Iruhusu neema ya Mungu itawale maisha yako**

**Utafute kwanza Ufalme wa Mungu**, na haki yake; na yote unayoyahitaji utazidishiwa, yatakufunika kama jinsi matunda yanavyofunika tawi la mzabibu (Mathayo 6:33).

Katika Matendo 26:18 tunasoma kwamba tunapogeuka au kutubu, tunajiondoa kutoka katika nguvu za Shetani na kujiweka chini ya nguvu ya Mungu.

### **Aina tatu za matunda**

**Mojawapo ni kwa kila kila tunachohitaji na kila anachohitaji Mungu**

**1. Tunda la Roho:** Tunda la ndani. Hili ni tunda linalokufanya ufanane na Yesu. Soma Wagalatia 5:22-23. "Lakini tunda la Roho ni

upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."

**2. Tunda kwa ajili ya maisha yetu:** Hili ni pamoja na tunda la kijamii, kifamilia, kiafya na kimwili, kifedha, nk. Katika 1 Wakorintho 9:7 imeandikwa hivi: "Ni askari gani aendaye vitani wakati wowote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunyuwa katika maziwa ya kundi?"

**3. Tunda la Kimisionari:** Tunda kwa ajili ya wengine; yaani huduma. Neno la Mungu katika Yohana 4:36 linasema: "Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeze apandaye na yeze avunaye wapate kufurahi pamoja."

**Matunda yote yana mbegu ndani yake kwa ajili ya kuzaa.** Katika Mwanzo 1:11 imeandikwa: "Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo."

Mara tunda la ndani linapokuwa ndani yetu, humwaga nje mbegu zinazozaa tunda la nje, au huduma kwa wengine.

### Kanuni ya mbegu au Neno inatendaje kazi?

**Katika Marko sura ya 4:1-21** tunaelezwa juu ya mfano wa mpanzi. Ufalme wote wa Mungu hutenda kazi katika siri hii. "Akawaambia, Nin yi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano." (Marko 4:11).

Katika mfano huu Yesu alitupata uhariblu rahisi wa kufuata ili tuenende katika ufalme wake katika hali ya kuzaa na kumpendezza

Hakuna ubaguzi wa rangi, elimu, umri, jinsia, akili, hadhi ya kijamii au kifamilia. Hakuna!

**Soma Marko 4:1-21.** Katika Marko 4:11 tunapata maneno yafuatayo "Akawaambia, Nin yi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu." Katika Marko 4:14 imeandikwa pia hivi: "**Mpanzi huyo hulipanda neno.**"

### Hutenda kazi sio tu kama mbegu, bali pia kama punje ya haradali

Katika Marko 4:30-32 tunasoma pia maneno yafuatayo: "Akasema, Tuulinganishe na nini ufalme wa Mungu? au tuutie katika mfano gani? Ni kama punje ya haradali, ambayo ipandwapo katika nchi,

ingawa ni ndogo kuliko mbegu zote zilizo katika nchi, lakini ikiisha kupandwa hukua, ikawa kubwa kuliko miti yote ya mboga, ikafanya matawi makubwa; hata ndege wa angani waweza kukaa chini ya uvuli wake."

**Punje ya haradali ni punje inayojulikana kuwa ndogo sana kuliko zote.** Mbegu nyininge zote za mboga za majani huota na kuwa mimea lakini punje ya haradali huota na kuwa mti! Sio jambo la kawaida kitu kinachoonekana kidogo kuzaa kitu kikubwa! Vile vile sio kawaida mmea wa msimu kuwa mti. Ndivyo ilivyo kwa mbegu ya Neno la Mungu na Ufalme wa Mungu. Haioneekani kubwa, lakini itakupatia mahitaji yako yote, kama jinsi punje ya haradali inavyofanya kwa ndege wa angani. Soma Luka 17:5 kuhusu imani ya punje ya haradali.

### Kila mtu lazima achague mojawapo ya njia hizi za kuishi

#### Ufalme wa Dunia

Shetani ni mfalme

Tunakuwa watumwa  
wake

Tunatumia akili zetu  
kukidhi haja zetu

Tunaishi kwa kufanya  
vitu visivyo na thamani  
katika maisha ya milele

#### Ufalme wa Mungu

Yesu ni mfalme

Tunakuwa watumwa wake  
Tunatumia Neno lake  
kukidhi haja zetu -  
matunda

Tunaishi kwa kufanya vitu  
vitakavyotupatia thawabu  
katika maisha ya milele.

Lakini angalia!

Ili tunda likue, kuna kanuni au utaratibu. ~~Kanuni hii isipofuatwa,~~  
~~tunda litakufa.~~ Tunayo mambo mawili tu ya kuchagua: Kukua au  
Kufa!

**Hii ndiyo dhamira ya "Kukua au Kufa." Ni kanuni ya Mungu ya kuzaa matunda.**

- 1) Tunahitaji kuligeukia Neno kwa ajili ya matunda
- 2) Tunahitaji kujua jinsi ya kutoka njie na kukaa mbali na hali ya kuwa Wafungwa katika nchi ya Ahadi.
- 3) Tunahitaji kujua jinsi ya kumkaribia Mungu - Hali hii ni Mto Utiririkao.
- 4) Tunahitaji kujua zaidi kuhusu tabia ya Mungu - Mungu ni nani.
- 5) Tunahitaji kujua sisi ni kina nani hasa katika Yesu – KUKETI

- 6) Tunahitaji kuuchukua msalaba wetu na kutembea kwa kulitii Neno – KUENENDA
- 7) Tunahitaji kujua juu ya adui yetu Shetani na jinsi anavyokuja kuliiba Neno; na jinsi ya KUMPINGA hadi ushindi na matunda yanapopatikana.

Haya yatakuwa masomo katika mfululizo wa Kukua au Kufa. Ni masomo ya Kibiblia, yanatenda kazi, yanahu su kile ambacho Neno linafundisha, na ninaweza kushuhudia kwamba kamwe Mungu hajashindwa kutumia kanuni au hatua hizi katika maisha yangu.

**Katika Yohana 15:18-27 Yesu anatuonya kwamba sehemu ya hatua za kuzaa matunda ni kuchukiwa na kuteswa, lakini pia Roho Mtakatifu yupo kama mfariji wetu.**

“Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu.” (Yohana 15:20). Watu wengi hawapati wanayoyahitaji kwa sababu Shetani au wasaidizi wake huja na kuliiba Neno kabla halijaza matunda. Tunahitaji kujua kwamba kuchukiwa, majaribu na mateso tunayoyapitia hayamaanishi kwamba tunda halikui, kinyume chake, mambo hayo ni dalili kwamba tunda linakua. Tunahitaji kuwa wenye hekima!

**Mbegu zinahitaji chakula. Zinahitaji maji na madini. Tunahitaji kuongeza hayo kwenye mbegu iliyopandwa.**

Kuna kanuni ambayo kwayo mtu anayemwamini Yesu Kristo hukua. Kuielewa kanuni hiyo na njia na kushirikiana na Mungu katika hiyo, kutahakikisha kwamba mtu anayemwamini Yesu atakua. Tunaamini kwamba kozi hii ya Kukua au Kufa ina maji, vitamini na madini yanayohitajika kwa ukuaji.

**Kuwa mjinga, na au kukataa kushirikiana na Mungu, kutamfanya mtu anayemwamini Yesu awe “Mfungwa katika nchi ya Ahadi”.**

Wana wa Israeli walifanikiwa kuingia Nchi ya Ahadi. Katika kitabu cha Waamuzi, watu wa Mungu, ingawa walikuwa katika agano na Mungu, walikuwa wafungwa kwa maadui zao. Gideoni na watu wake ni mifano kwetu ya wafungwa walipata kuwa huru.

Kwa namna hiyo hiyo, watu wa Mungu siku hizi ni wafungwa wa hofu, hatia, ulevi, kuhukumiwa, kiburi, majivuno na maadui wengi wa kiroho.

Njia ya kuepuka kukaa kifungoni, ni **Kukua!**

Mwisho wa hatua za kukua ni **Matunda**. **Matunda** ni matokeo ya kukaa ndani ya mzabibu utakaota “**mmisionari**” ndani ya kila mtu amwaminiye Yesu Kristo. Angalia katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana, matokeo ya mwisho baada ya vita vyote ni **Matunda**.

#### **Kuna makundi 7 makubwa katika hatua za Kukua au Kufa**

Kuzaa Matunda	(Lengo la kuzaa matunda)
Wafungwa katika Nchi ya Ahadi	(Hali tunayoweza kuwa nayo)
Mto Utiririkao	(Ushirika na Mungu)
Mungu ni nani	(Tabia yake)
Kuketi	(Nafasi yetu katika Kristo)
Kuenenda	(Wajibu wetu)
Kupinga	(Ushindi wetu katika vita)

Hayo ndiyo “Masomo 7 ya Mwongozo” yanayofanya Sehemu ya 1 Semina ya 1. Sehemu ya 2 Semina ya 2 ina masomo mengine 4 yanayohusu Msalaba, Pepo na Ukombozi na Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

**Kila kundi hapo juu lina masomo kadhaa** ambayo mwanafunzi anaweza kujifunza ili akamilishe kozi ndefu. Katika kozi ndefu, utaanza kwa masomo yaliyoperidheshwa hapo juu, kisha utaendelea na masomo mengi yaliyomo ndani ya baadhi ya makundi hayo makuu. Kwa mfano, kundi la Mungu ni nani lina masomo 18. Kuketi lina masomo 13, Kuenenda lina masomo 41, na Kupinga lina masomo 11 (kuna masomo zaidi katika Kozi ya 3). Unaweza kuchagua kutoendelea na kozi baada ya kusoma na kujifunza masomo 11 katika kitabu hiki au unaweza kuendelea kukamilisha kozi yenyе masomo zaidi ya 90.

**Ni muhimu kwetu kujuia jinsi tunavyojifunza na jinsi tunavyotenda mambo ya kiroho.** Hatujifunzi mambo ya kiroho kama tunavyojifunza mambo ya kidunia, kwa njia ya habari au taarifa tulizo nazo katika akili zetu. Ni kweli kwamba akili zetu pia ni sehemu ya njia inayotumika kujifunzia mambo hayo.

**Hata hivyo huwa tunapokea ufunuo kwa Mungu**, yaani tunapokea kitu kilichofunuliwa ambacho awali kilikuwa kimefunkwa au hakikuwa kinaonekana. Shetani huweka utaji kwenye macho yetu ya kiroho ili tusiweze kuona (Wakorintho 4:4). Lakini jambo kubwa kabisa linalotupasa kujuia ni kwamba, tunapokea ufunuo huu, tunaupokea kama mbegu, na siyo kama tunda. Hivyo kwa kila sehemu ndogo ya ukweli ambao Bwana hutufunulia, tunapaswa kuuweka katika utaratibu au kanuni ya Mungu ni

nani, Kuketi, Kuenenda na Kupinga. Mungu hutufunulia jambo fulani kuhusu yeye mwenyewe, kisha huliweka jambo hilo katika maisha yetu (Kuketi), kisha tunahitaji kutii na kuenenda katika jambo hilo. Kwa uhakika Shetani huja kuiba Neno, hivyo tunapaswa Kumpinga. Tukifanikiwa kufanya hivyo tutazaa matunda. Ukitoma Marko sura ya 4 utaona maandiko yanayoelezea jambo hilo.

**Kwa hiyo utaratibu huu wa uanafunzi wa Yesu, sio tukio moja kubwa katika maisha yetu.** La hasha, ni utaratibu unaoendelea tunaoupitia siku hadi siku, kwa kila kipindi cha maisha yetu. Utaratibu huu kamwe hauna mwisho. Tunaweza kupinga suala moja lakini wakati huo huo tukawa katika kanuni au utaratibu wa kuketi katika suala jingine la maisha yetu.

### **Ufuatao ni muhtasari wa mtaala wa Kukua au Kufa**

**Tunda** (Somo hili). Kuutumainia Ufalm wa Mungu; Neno la Mungu.

**Mto Utiririkao.** Tunahitaji kufanya tawi liendelee kuungana na mzabibu kwa njia ya ushirika. Tunahitaji uwepo wa Mungu katika maisha yetu ya kila siku. Hii ni ramani rahisi ya kibiblia kwa ajili ya kufanya hivyo katika muda wako binafsi wa kumwabudu Mungu. Sura ya 47 ya kitabu cha Ezekieli inaeleza juu ya mto unaotiririka kutoka katika hekalu la Mungu na kwenda katika bahari iliyopotea ya wanadamu. Sisi ni hekalu la Mungu. Kuwa karibu na Mungu hutangulia huduma ya kweli!

**Wafungwa<sup>1</sup> katika Nchi ya Ahadi.** Tunahitaji kuwa huru ili tusiwe matawi yatakayopewa katika moto wa kutozaa matunda. Gideoni ni mfano wa Mwisraeli aliyejkuwa na agano na Mungu, akiishi katika nchi ya ahadi, aliyopewa na Mungu, lakini bado alikuwa mafungwa kwa maadui zake. Ni aina gani ya maadui wanaotuweka kifungoni? Na je, tunawezaje kuwa huru?

**Mungu ni nani.** Tunahitaji kukumbushwa kila mara Mungu ni nani, na kwamba bila yeye hatuwezi lolote. Tutapata picha ya haraka ya tabia ya Mungu. Tutagusia masuala kama vile Utatu Mtakatifu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Tutazungumzia kuhusu Neno la Mungu, na jinsi Yesu alivyozaliwa na bikira Mariamu.

**Kuketi, Kuenenda, Kupinga.** Kama mwanafunzi wa Yesu Kristo ni muhimu kujua na kufahamu unajifunza nini na kwa njia gani. Labda utaona kwamba kuna mambo mengi tofauti utakayohitaji kujifunza. Mara nydingi mafundisho na masuala ya imani huelekea kuleta mabishano au kupingana yenye kwa yenye.

Kwa mfano, tukitaka kuishi maisha matakatifu, tunahitaji kufanya bidii. Lakini kwa upande mwingine, neema ipo kila wakati tunaposhindwa. Kwa hiyo tufanye nini sasa? Tutende mema, au tuishi maisha yale ya zamani (yasiyompendeza Mungu) na kuingojea neema ya Mungu?

**Wazo la Kuketi, Kuenenda na Kupinga** litatoa ufumbuzi wa mgongano huu. Katika kitabu cha Waefeso, masuala yote hayo matatu yamezungumziwa. Tunamshukuru pia sana ndugu Watchman Nee kwa kitabu chake kiitwacho: “Sit, Walk and Stand” (Kuketi, Kuenenda na Kupinga).

**Kuketi:** Katika Waefeso 2:6 tunasoma maneno yafuatayo ”Akaturufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu.” Mungu anataka tujue kwamba Yesu alimaliza kazi yote muhimu pale msalabani kwa ajili ya wokovu wetu. Kazi iliyomalizika ya msalaba na uufuwa wa Yesu, imetufanya kuwa viumbe vipyta. Utu wa kale ulitoweka, tukazaliwa mara ya pili. Tunahitaji kujua kwamba Mungu ndiye aliyeifanya kazi hiyo, sisi hatukufanya lolote ila tu kupokea kazi aliyoimaliza. Haijalishi makosa mangapi tunayoweza kufanya, msamaha unapatikana. Hatupo tena chini ya sheria.

**Kuenenda:** Neno la Mungu katika Waefeso 4:1 linasema, ”Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa.” Kwa kuwa sasa umejua wewe ni nani katika Yesu, unatakiwa kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo. Usiwe sheria bali kiumbe hai ndani ya Roho Mtakatifu. Umeitwa kuenenda na kuishi katika utakatifu na haki. Hii sio njia ya kupata wokovu au upendeleo kwa Mungu bali kuyafanya maisha yako ya nje yalingane na maisha ya kiroho yaliyopo ndani yako. Kila wakati jambo hili liwe chaguo lako. Ndege ni lazima aishi kama ndege, hana chaguo, lakini Mkristo anaweza kuchagua kuishi kama niwerwe dhambi. Hii ni hatari, kwa sababu kama Mkristo ataishi kwa muda inayu katika dhambi bila kuungama na kutubu, ni wazi atarudi nyuma kiroho.

Katika Luka 9:23-24 tunasoma maneno yafuatayo: ”Akawambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane inwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye ~~kuiponya~~ nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakaye ~~iangamiza~~ nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha.” Tumeitwa kuyakana au kuyakataa maisha yetu ya zamani na kuukubali msalaba.

Hivi sasa, tumeingia katika agano la damu kati yetu sisi na Mungu; na agano la damu linahitaji vifo viwili. Yesu alishamaliza kazi yake, sisi nasi tumeitwa tufanye sehemu yetu.

**Kupinga:** Hii ni nia yetu dhidi ya adui. Kuna nguvu kubwa juu ya adui kwa njia ya msalaba. Katika Waefeso 6:10-13 tunaagizwa kuzipinga hila za Shetani. Kutakuwa na vita na shida, lakini Roho Mtakatifu atatupatia faraja. Katika Waefeso 6:11 tunaambiwa ”Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.” Tunahitaji kujua kwamba Shetani yupo na anatenda kazi; na kwamba matakwa yake ni kuua, kuiba na kukuharibu wewe na familia yako. N kweli yupo! Atakudanganya na

kukufanya uamini kwamba huna nafasi ya kuketi. Atakujaribu uenende katika njia za ulimwengu na katika utu wako wa kale. Yesu alimshinda Shetani, hata hivyo anaruhusiwa kutudanganya na kutujaribu. Lakini tunao uwezo wa kumshinda. Maisha haya ya Kikristo sio rahisi. Hisia zetu na mazingira hujaribu kutudanganya kuhusu kuketi, kuenenda na kupinga. Lakini kama tukimpinga Shetani, baada ya kujua sisi ni akina nani katika Kristo, na baada ya kuenenda katika Roho na katika toba, tunaweza kumpinga hadi ushindi unapopatikana.

Mpaka siku tutakapokwenda mbinguni, tutaendelea kuhusika katika vita kubwa dhidi ya ufalme wa Shetani. Ushindi utapatikana kila wakati kama tutazingatia kuketi, kuenenda na kupinga.

“Watu na wakushukuru, Ee Mungu, Watu  
wote na wakushukuru, Nchi imetoa  
mazao yake MUNGU, Mungu wetu,  
ametubariki” (Zaburi 67:5,6)

## Sura ya 2 – Mto utiririkao

Kusafisha, kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi wa Yesu, kueneza Injili, kuifikia  
“bahari ya chumvi” ya wanadamu. Ezekiel 47:1-12

### Makusudi ya Mungu ni kuwafikia wanadamu waliopotea. Kwa njia gani?


Ezekiel 47:1-12: Picha alioonyeshwa Ezekiel ni ya Hekalu la Mungu na mto unaotoka katika hekalu hilo. Mungu aliongea na Ezekiel na kumwonyesha kwamba huu ulikuwa Mto wa Uzima unaotiririka kutoka kwa Mungu hadi kwenye bahari ya chumvi na kuingia katika maji machafu yaliyooza. Mto huu utayaponya maji hayo na kuyafanya hai.

Kwa kawaida bahari katika Biblia, humaanisha bahari ya wanadamu waliopotea. Mungu alikuwa akimuonyesha Ezekiel kwamba njia pekee ya kuwafanya wanadamu waweze kuishi, ni kwa kuguswa na Mungu, kwa njia ya kitu kinachoitwa **Mto** unaotiririka kutoka katika uwepo wake mwenyewe.

Katika Yohana 7:38 imeandikwa hivi, “Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, **Mito** ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.”

Hekalu liko wapi leo? Katika 1 Wakorintho 6: 19-20 tunaambiwa hivi; “Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenywewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika mili yenu.”

### Mto unatiririkia ndani ili kurasafisha – Mto unatiririkia nje ili kuuokoa ulimwengu uliopotea



Mungu

WEWE

Ulimwengu uliopotea

Tunahitaji uwepo wa Mungu utuweke huru na kutusafisha, ili tuweze kufanya aina yoyote ya huduma na hata kuomba maombi yaletayo matokeo.

**Tunahitaji kujua kwamba kuna maadui wanaotaka kumzuia  
Mungu asionekane kwamba ni kweli yupo pamoja nasi.**



Maadui zetu huja kwetu kwa njia kuu tatu

*Utashi wetu –  
Akili zetu –  
Hisia zetu –  
Hushambuliwa na Mwili, Ulimwengu na Shetani*

Swali  
**Tunawezaje kuwashinda maadui hawa ili tuweze kuingia  
katika uwepo wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye?**

*Prayer for protection of the family*  
**Mungu ameishatupatia ushindi dhidi ya maadui wote! Njia ya  
kuingia katika uwepo wake ilipatikana pale msalabani wakati  
pazia lilipopasuka toka juu hata chini – Marko 15:38. Sasa ni  
kazi yetu kushirikiana naye. Tunapaswa kubeba msalaba  
wetu – huo utatupatia ushindi!**

Katika Luka 9:23-25 Biblia inasema, “Akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na **ajikane** mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya **nafsi** yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza **nafsi** yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha. Kwa kuwa yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza, au kujipoteza mwenyewe?

Neno hilo **nafsi** katika Luka 9 linamaanisha utashi, akili na hisia. Neno **kukana** linamaanisha kukataa kitu fulani.

**Ufunguo wa kupata uzima tele na kupokea baraka kutoka kwa Yesu, hii ikiwa ni pamoja na uwepo wake, ni kukamilisha agano la damu kwa kubeba msalaba wetu.**

Wengi wetu tunajua kazi nzuri sana, yenyе uweza mkuu, iliyohusisha kila kitu, ambayo Yesu aliifanya juu ya msalaba wa Kalivari, jinsi alivyomwaga damu yake kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka katika wafu ili kutupatia uzima. Hatuwezi kuongeza chochote juu ya hayo. Hata hivyo, ili tuweze kunufaika na kazi hiyo, hatuna budi pia kufa. Lazima tubebe msalaba wetu, tujikane wenyewe na kumfuata. Ni lazima tuiangamize nafsi yetu.

Uhusiano na USHIRIKA wetu na Mungu umejengwa juu ya msingi wa agano la damu. Kwa wengine jambo hilo linaweza kuonekana geni. Jambo hilo linaweza kulinganishwa vizuri zaidi na ndoa. Watu wengi sana wana ufahamu usio wa kibiblia kuhusu uhusiano huu wa agano la damu. Hebu jiulize swali hili: Je, ungeweza kujadiliana na mchumba wako kuhusu uhusiano mwagine wa kimwili unaoruhusiwa kuwa nao na wanawake wengine baada ya ndoa?

**Agano la ~~damu~~ huchochewa na vifo VIWILI; cha Yesu na chako!**


**Ni kitu gani muhimu sana kuhusu agano la damu?**



Katika kitabu cha 1 Petro 1:18-19 tunasoma maneno yafuatayo: "Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa **damu** ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo."

Katika Mambo ya Walawi 17:11 tunasoma pia maneno yafuatayo: "Kwa kuwa uhili wa mwili u katika hiyo damu; nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi."

**Maisha ya kiroho yanaweza kubadilishana na ile sheria ya mbadala. Agano la damu hubadilisha urithi wa familia yako.**



Kimsingi, hii ina maana kwamba watu wanaweza kuzaliwa katika familia fulani, na katika familia au ukoo wao huo, wakapokea baraka na laana kama urithi wao. Hata hivyo, baraka na laana zinaweza kubadilishwa. Makabila kadhaa katika para ya Afrika, na pia katika utamaduni wa Wahindi wekundu na katika Jamhuri nyingine za Asia, yamekuwa kila wakati yakinifuta njia za kubadilishana na watu wengine baraka na laana.

Kabla ya kuumbwa kwa dunia, Mungu alikuwa amepanga kwamba Yesu asulubiwe kulingana na Roho wa UZIMA, na hii ina maana kwamba ile kanuni ya mbadala ilikuwa ikitenda kazi hata kabla mwanadamu hajaumbwa (Ufunuo 13:8).

**Ili agano la damu liweze kweli kufanya kazi, ni lazima kila upande unaohusika umwage damu, au ni lazima viwepo vifo viwili au misalaba miwili. Lazima utu wetu wa kale ufe na kisha tujikabidhi sisi wenyeewe na vyote tulivyo navyo kwa Yesu. Jambo la kufurahisha ni kwamba hata Yesu mwenyeewe ametoa yote aliyo nayo na kujitoa mwenyeewe kwetu!**

**Tunapounganisha msalaba wa Yesu na msalaba wetu tunakuwa  
tumeunganishwa na Mungu...  
na Nguvu hutoke!**




Kila wakati kunakuwa na misalaba miwili inayopaswa kuungana ili kufanya agano la damu.

**Hema ni alama yenyeye nguvu ya misalaba miwili inayofaa kutumiwa  
kama mwongozo wa maombi. Itatusaidia kubeba msalaba wetu na  
kutuingiza katika uwepo hasa wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye!**

"Agano la Kale linatuambia jinsi wateule wa Mungu walivyoishi duniani. Kwanza, Hema lilitumika kama kituo cha makabila 12; baadaye Hekalu ndilo lililokuwa kituo chao. Kituo cha Hekalu kilikuwa Sanduku. Hema, Hekalu na Sanduku ni aina mbalimbali za Kristo. Kadri wana wa Israeli walivyokuwa na uhusiano mzuri na Hema au Hekalu walipata ushindi, na hakuna taifa lililowezwa kuwashinda. Ingawa wana wa Israeli walikuwa hawajui kupigana, waliwashinda maadui zao wote walipokuwa wamejifunza jinsi ya kupigana. Lakini wakati walipokuwa na tatizo kuhusiana na Hema au Hekalu, walichukuliwa utumwani. Haikusaidia kitu kuwa na wafalme wewe nguvu au hekima kubwa, kitu muhimu kilichoangaliwa ni iwapo wamelikosea sengokul la maskani au hekalu. Walipotoa kipaumbele kwa Mungu, ushindi ulikuwa wao. Ndiyo ilivyo hata leo. Tukiizingatia ushindi wa Kristo, sisi pia tutapata ushindi."

Dondoo kutoka katika kitabu kiitwacho "God's plan and the Overcomers" (Mpango wa Mungu na washindaji), kilichoandikwa na Watchman Nee

**Unavyoendelea kuwa na ushirika na Mungu, jaribu kujiona kana  
kwamba unatembea katika Hema kama jinsi makuhani wa Agano la  
Kale walivyofanya.**



## Kwanza: Msalaba Wake

Kwa ajili yako

Nyakati za Agano la Kale, kila mwaka Wana wa Israeli walikuwa wakiadhimisha Siku ya Upatanisho ijulikanayo kama "Yom Kippur". Dhambi za wana wa Israeli zilikuwa zikishughulikiwa katika siku hii moja tu ya mwaka, wakati kuhani mkuu alipojiandaa kuingia katika Hema kwa niaba ya wana wa Israeli kwa ajili ya dhambi zao.

Pale kwenye madhababu ya Shaba, katika ua wa nje, kulikuwa na mbuzi wawili. Mmoja alifungwa kitambaa chekundu shingoni mwake kuonyesha kwamba atachinjwa kwa ajili ya damu. Mwingine alifungwa nje ya lango kuonyesha kwamba angekuwa Azazeli. Mbuzi wa kwanza alichinjwa madhabahuni na damu yake ilipelekwa na kuhani patakatifu pa patakatifu ambapo aliitoa kwa kufukizia kando ya madhababu ya kufukizia (mahali pa sifa). Uvumba ulipokuwa ukiungua, ulisababisha moshi ujae patakatifu pa patakatifu, na hiyo iliwalilisha (na kuleta hasa) uwepo wa Mungu. Kuhani alinyunyiza damu juu ya Kiti cha rehemaa mara moja na pia alinyunyiza damu mbele ya Kiti hicho mara saba. Nje ya marago kila mtu alilala kifudifudi wakati yote hayo yalipokuwa yakiendelea. Makuna mtu aliyeona chochote kilichokuwa kikifanyika, na hiyo ilimaanisha kwamba dhambi zao zilisamehewa kwa mwaka mzima.

Pili, kuhani aliporudi na kubadili nguo zake aliweka mikono yake juu ya mbuzi mwingine, Azazeli, kuashiria kwamba dhambi zote zimehamishiwa juu ya kichwa cha mnyama huyo. Kulikuwa na mtu aliyechaguliwa kumpeleka mbuzi huyo jangwani mahali pasipokaliwa na watu na kumwacha sehemu ambayo hawesi tena kurudi au kutoroka. Mtu huyo kwa mfano, alimpeleka mbuzi yule hadi kwenye bonde lililozungukwa na miamba na majabali na kisha mbuzi yule aliteremshwa chini ili asiweze kutoroka(Mambo ya Walawi 16:21-22).

Sasa kuhani alipoweka mikono yake juu ya mbuzi aliye hai, ili kuanza sehemu ya pili ya ibada, aliungama dhambi zote za wana wa Israeli. Alisema, "Bwana, weka dhambi zangu na za wana wa Israeli juu ya kichwa cha mbuzi huyu. Haya, we mbuzi, ondoka." Mbuzi yule alipokuwa akipelekwa nje ya marago, watu wote walismama na kushangilia. Watu wote na hata watoto waliweza kuona tukio hilo na

kufahamu. Azazeli ni mfano wa Yesu aliye Azazeli wetu, aliyeshushwa chini hata kuzimu kwa ajili yetu huku dhambi zetu zikiwa juu ya kichwa chake. Alichukua dhambi zetu na kuziondoa kabisa, zisionekane tena au kurudi. Zaburi ya 103:12 inasema "Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao." Katika kitabu cha Mika 7:19 tunasoma pia maneno haya "Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari."

Katika kitabu cha Waembrania 9:12-14 tunapata pia maneno yafuatayo "wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe alilingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyoniyiziwa wenyewe uchafu hutakasa hata kutusafisha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Pili: Msalaba Wetu



### Hema


Ua wa nje

Patakatifu

Beba msalaba wako

Patakatifu pa Patakatifu

Mahali tunapokutana na Mungu  
katika uwepo wake



Yesu aliposema kwanza ni lazima tujikane, tuiangamize nafsi kwa ajili yake, nk., alikuwa na maana kwanza tunapaswa kuikana au kuiambia nafsi "hapana".

Nafsi yetu ina sehemu tatu: Utashi (Nia / Akili) na Hisia. Patakatifu panawakilisha ile sehemu ya utu wetu, yaani nafsi. Sehemu hiyo ilikuwa na na aina tatu za fanicha au samani zinazowakilisha utashi wetu, Akili na Hisia (Angalia mchoro huo hapo juu). Kwa hiyo tunapoziambia sehemu hizi "hapana" na kusema "ndiyo" kwa yale aliyo nayo Mungu, huku ndiko kuubeba msalaba wetu.

*Utashi wetu-*

*Akili zetu-*

*Hisia zetu-*

**hushambuliwa na Mwili, Ulimwengu na Shetani**

**Sasa tutasafiri hadi kwenye sehemu zote hizo tatu wakati wetu wa  
maombi na pia tutaendelea na safari na kuwapita  
maadui zetu hadi katika uwepo wa Mungu!**

**"Mto Utiririkao"  
(Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku)**

**Kusafiri hadi katika Uwepo wa Mungu**

Maelekezo:

1. Soma kwanza kurasa 7 za mwanzo, na kisha zisome tena angalau mara moja kwa mwezi. Halafu kila siku, anzia ukurasa huu, na uwe na muda wa kuwasiliana na Mungu angalau kwa dakika ishirini.

2. Utakapoanza na hema ya kukutania, mgongo wako unapaswa kuielekeea dunia huku uso wako ukimwelekea Yesu. Hii ni muhimu kwa sababu Roho Mtakatifu hawezi kukaa na wewe iwapo unaelekeea mahali pabaya. (mwelekeo wa kiroho, Matendo ya Mitume 26:18)

3. Nenda hadi kwenye kila "kituo" ushughulike na somo hilo katika hali ya maombi pamoja na Bwana. Tafuta katika Biblia baadhi ya maandiko. Uwe macho kuhusu maeneo yanayohitaji toba, kwa sababu jambo hili ni moja kati ya michango yetu mikubwa, wakati huu tunapokuwa na ushirika na Mungu.

4. Ni vema ukipitia vituo hivi vyote kwa wakati mmoja. Unaweza kufanya hivyo kwa DAKIKA ISHIRINI. Hata hivyo, kama huna muda wa kupitia utaratibu huu wote kwa mkao mmoja, usikate tamaa. Badala yake, anza utaratibu huu asubuhi, na umalize angalau hatua moja. Kisha endelea na hatua ya pili wakati wa chakula cha mchana. Kama unahitaji, endelea siku inayofuata. Hatimaye ishi maisha yanayofuata utaratibu huu na ~~itakuwa kawaida kwako~~ kawaida kwako kukaa katika uwepo wake Mungu.

**Ua wa Nje**

**Kituo cha kwanza: Madhabahu ya Shaba - Msalaba wa Yesu.**

**Msamaha**

**Madhabahu ya Shaba**

Agano la damu hubadili mabaya yote tulio nayo na kuweka mema yote aliyo nayo Mungu. Hata hivyo hatuwezi kupata msamaha wa dhambi bila kumfanya Yesu kuwa Bwana (Warumi 10:9-10).

Anza leo kuwa mkweli mbele za Yesu. Neno la Mungu katika 1 Yohana 1:9 linasema "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu

na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Sehemu kubwa ya kubeba msalaba wako ni kuwa MKWELI KABISA mbele za Mungu. Unahitaji kuwa wazi kabisa na kumwambia kila kitu. Uwe na muda wa kuumimina moyo wako kwa Mungu kama jinsi ambavyo ungefanya kwa mtu ambaye ni rafiki yako sana! Biblia inasema katika 1 Yohana 1:7 kwamba "**tukienenda nuruni**, kama yeze alivyo katika **nuru**, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote." Yesu alisema katika Yohana 3:19 kwamba dhambi haina nguvu iwapo watu watakuja kwenye nuru pamoja na kweli, bila kujaribu kujificha gizani. Yesu hakufa kwa ajili ya visingizio vyetu. Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu!

**Unahitaji kutembea katika upendo, na ikitokea kwamba umefanya dhambi, kimbilia kwa Mungu, usafishwe.**

"Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniachaka huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti"(Warumi 8:2). Tukimeukia Mungu kila wakati, na kudumu katika hali ya uaminifu mbele zake, atatushindia makosa yetu na vikwazo.

**Angalia Mto Utiririkao Kiambatisho cha F ujithathmini mwenyewe kwa uaminifu.**

Kama hakuna dhambi zinazojulikana, basi kiri kwa kinywa chako maneno yaliyogandikwa katika Wagatalia 2:20 na 2Wakorintho 5:21.

### Kituo cha Pili Birika; Neno la Mungu

Birika la Shaba

Kwa kuwa sasa fahamu zetu ziko wazi na tunaweza kuwasiliana na Mungu, hebu twende kwenye Neno. Neno linasema kwamba kuhani angekufa kama angejaribu kuingia patakatifu kabla ya kusimama kwenye birika. Hatuwezi kwenda katika uwepo wa Mungu bila kusafishwa na Neno la Mungu (Waefeso 5:26-27).

Birika litatuondolea uchafu wa dunia. Litakuwa pia kioo cha kutuhukumu, litatuletea katika akili zetu mambo tunayopaswa kurekebisha mbele za Mungu. Neno litahuisha nafsi zetu ili tuweze kufikiri kiroho na kuwa kinyume na maneno ya pepo yanayokuja katika akili au fahamu zetu.

Neno linatuambia pia kwamba Shetani amekwisha hukumiwa (Yohana 16:11). Hakikisha unasema maneno haya kwa sauti "Shetani umekwisha hukumiwa, umeshindwa!"

Tumia dakika chache katika Neno!

- a. Tumia kitabu chako cha sala
- b. Tumia kitabu chako cha "ISOB" au kitabu kingine cha kujifunzia Biblia.
- c. Soma kitabu cha Mithali
- d. Soma Zaburi sura moja au zaidi.
- e. Soma vitabu vingine vinavyohusu Biblia au soma tu Biblia na umwombe Roho Mtakatifu akutafsirie. Soma Biblia yote kwa mwaka mmoja.
- f. Sikiliza mafundisho au kanda za nyimbo zenyе Neno la Mungu.

**Kituo cha Tatu: Pazia la Kwanza: Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu.**

### **Pazia la kwanza: Kushukuru**

Kwa kuwa sasa umekaa katika Neno, unajua uko safi mbele za Mungu na kwamba Shetani amehukumiwa, basi unayo mengi ya kumshukuru Mungu! Hata kama huoni kwa haraka mambo ya kumshukuru Mungu jaribu kuyatafuta. Kama umeshindwa kuyapata, mshukuru kwa Neno lake linalosema kwamba unao ushindi ukiendelea kulishikilia Neno. Mshukuru pia Mungu kwa ahadi alizokuahidi ambazo bado hazijatimia katika maisha yako.

### **Kituo kinachofuata kipendani ya Patakatifu**

**Hapa ndipo unapompa Yesu utashi au mapenzi yako na Yeye anakuonyesha mapenzi yake, unampa ~~ufahamu~~ wako na Yeye anakupa ufahamu wake, unampa hisia zako na Yeye anakupa hisia zake. Huku ndiko kuubeba msalaba wako, kujikana mwenyewe na kumfuata Yesu (Luka 9:23)**

### **Utashi wako**

### **Meza ya Mkate wa Wonyesho**

Badilisha haja za moyo wako (hata kama ni nzuri) kwa ajili ya mpango au mapenzi ya Mungu katika maisha yako. Weka chini matakwa na mipango yako na umwombe Mungu akuonyeshe mapenzi yake na mipango yake kwako.

Kila wakati Mungu huangalia utashi au mapenzi yetu; hii ndio maana ya mkate wa wonyesho. Mkate ni unga uliosagwa, ukachanganywa na mafuta na kuokwa motoni. Matakwa yetu na hamu zetu ni lazima kila wakati zitolewe madhabahuni zisagwe na kuchomwa. Hii ni sadaka maalum kabisa kwa Mungu, kwa kuwa ni utashi *wetu*, na yeze hawezi kutulazimisha wala kutuamrisha kufanya hivyo. Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu (Warumi 12:1-2).

Amua kusamehe hata kama hujisikii kufanya hivyo. Hii ni nafasi ya kutubu na kuacha njia za kidunia na kuzifuata njia za Mungu. Tunapoacha njia mbaya, tunapata nguvu za Mungu (Mdo 26:18 na 2 Kor 3:16).

**Badilisha tamaa za mwili, uwe na tunda la Roho. Tunda la Roho ni:** upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi (Wagalatia 5:19-23).

### Nia yako

#### Kinara cha Taa cha Dhahabu

Badili nia au mawazo yako ya zamani uwe na nia ya Kristo. Katika 2 Kor 10:4-6 tunaambiwa kwamba vita viko katika mawazo na fikra zetu. Na kwamba ngome ni mawazo yetu. Mawazo haya hutufanya tuwe mbali na elimu ya Mungu. Kuna mengi ya kusema hapa kwa sababu mawazo yetu ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Tunapaswa kuyaweka huru mawazo yetu. Kwa nia gani? Tulipokuwa watumwa wa dhambi tulitumia Mti wa Ujuzi wa Mieria na Mabaya ambao ni mawazo yetu. Sasa tunapaswa kutumia Mti wa Utima ambao ni Neno la Mungu. Siwazi tena na kuamua, bali natumia akili zangu kwa sababu ni makusudi ya Mungu, na hiyo ndiyo kusikia na kuti! Hii pekee ndiyo itakayoangusha ngome katika akili zetu. Tukiuona utukufu wa Mungu kama Paulo alivyouna alipokuwa njiani kuelekea Dameski, hatuwazi tena, tunasema tu, “Bwana, unahitaji nifanye nini.”

Mara kwa mara pepo hutushitaki na kushambulia akili zetu kwa kutumia nusu ukweli. Katika Isaya sura ya 11 tunaambiwa kwamba Mungu hubadilisha maarifa yetu ya asili na kutuwekea yale ya Roho Mtakatifu, yaani Roho wa Bwana, hekima na ufahamu, shauri na uweza, maarifa na kumcha Bwana.

Tunahitaji mawazo au nia zetu zifanywe upya kwa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu (Warumi 12:2). Wakati mwingine hatujui kuomba

jinsi itupasavyo. Katika Warumi 8:26 tunaambiwa kwamba tukiomba kwa lugha, tutaomba sawa sawa na mapenzi kamili ya Mungu. Kwa hiyo kila unapoomba kwa lugha utakuwa unaomba sawa sawa na Neno la Mungu na pia sawa sawa na mapenzi ya Mungu. Ile sehemu inayohusika na usemi au kunena, hutawala akili, na hivyo nia au mawazo yako hufanywa upya na kusawazishwa ili yaweze kuuambia mwili wako utende mapenzi ya Mungu.

### Hisia zako

#### Madhabahu ya kufukizia uvumba

Badilisha hisia zako za zamani zilizosababishwa na mwili wako na ulimwengu, na nafasi yake ichukuliwe na tunda la amani, furaha, upendo, tumaini, nk. Hapa ni mahali pa dhabihu za sifa. Soma Zaburi 145-150 kwa sauti kubwa, kama hujisikii kumsifu Mungu moyoni mwako. Mungu anawatafuta watu wanaomwabudu katika Roho na kweli (Yohana 4:24). Kutoka katika mahali hapa pa sifa, Mungu atakutafuta na atahitaji kuwa pamoja nawe!

Mpatie hizo hisia ambazo umekuwa ukificha; labda ni machozi yako, labda ni kuinua kwako mikono, au labda ni kumfunulia tu hisia zako za kweli. Songa mbele, hakuna mwingine anayeangalia isipokuwa Yeye!

Mbele ya ~~madhabahu~~ hii kuna pazia linaloficha au kutenganisha patakatifu pa patakatifu na uwepo wa Mungu. Mungu anataka upite katika pazia hilo mara nyingi zaici ya vile unavyohitaji. Atakusaidia kufanya hivyo. Hakuna mwanadamu wa kawaida anayeweza kuingia hapo bila kufa.

Pazia hili lilipasuka kutoka juu hata chini wakati Yesu alipokufa msalabani, akatuwezesha kuingia katika uwepo wa Mungu kwa damu yake, na kuonyesha kwamba kifo chake kimeondoa kizuizi kilichosababishwa na dhambi. Kizuizi hicho kilikuwa kinatuzua kuingia katika uwepo wa Mungu. Msifu Mungu kwa ukweli huu.

Patakatifu pa patakatifu ni mahali aambapo hakuna mwanga au taa isipokuwa kwa ajili ya Mungu. Kuhani Mkuu aliweza tu kuingia hapa mara moja kwa mwaka, tena kwa masharti maalum. Ukweli ni kwamba madhabahu hii iliingia Patakatifu pa Patakatifu pamoja na Kuhani Mkuu mara moja kwa mwaka. Hii inaashiria kwamba kusifu kwako na kuabudu hakuishii hapa bali ni mlango wa kuingia katika uwepo wake, na mambo hayo huenda pamoja nasi.

**Sasa Mungu atakuvuta na kukupitisha katika pazia hadi  
Patakatifu pa Patakatifu - penye uwepo hasa wa Mungu**

**Sanduku la Agano**

Hili hapa Sanduku la Agano. Limefunkwa na Kiti cha rehema kilichonyunyiziwa damu. Tulihitaji rehema kwenye madhabahu ya shaba, yaani msalaba, mwanzoni kabisa. Lakini sasa katika uwepo wake kuna ufahamu mkubwa wa rehema yake na damu ya Yesu kwa namna ambayo Roho Mtakatifu pekee ndiye awezaye kukuonyesha. Rehema zake ni za milele. Ni kama haiwezekani kabisa kuandika rehema zake jinsi zilivyo, ni lazima mtu apate usoefu wa rehema hizo.

Katika kila upande kuna malaika wakubwa wanaolinda kila kitu. Hapa pia hakuna nuru kabisa au taa isipokuwa kwa ajili ya Nuru ya Mungu.

Kumbuka, sanduku la agano lipo sasa ndani ya miyo yetu! Sio tena kitu cha nje. Sisi ni hekalu la Mungu. Tafakari jambo hilo."Hamjui ya kuwa ninyi immekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaan ndani yetu?" (1 Kor 3:16).

**Yaliyomo katika Sanduku la Agano yanaashiria mambo makubwa matatu**

**Mana au Neno la Mungu:** Unapokuwa katika uwepo wa Mungu, Neno la Mungu lililofunuliwa huwa hai! Kama unao muda, hapa ni mahali pazuri sana pa kufungua Biblia yako na kumruhusu Bwana aseme nawe.

**Mbao za sheria:** Huu ni ukumbusho wa thamani kwamba sheria ya Mungu imeandikwa katika miyo yetu. Siyo tena orodha ya mambo tunayopaswa kufanya au kutofanya.

**Fimbo ya Haruni:** Hii inamaanisha huduma yetu iliyopakwa mafuta ya kuwa watendakazi na mashujaa wa maombi kwa ajili ya Mungu. Kulikuwa na fimbo 12 zilizovunjika za mti wa mlozi zilizowekwa Hekaluni kwa amri ya Mungu. Fimbo mojawapo ambayo ingechipua kimiujiza wakati wa usiku, ingekuwa ile ambayo mmiliki wake ni mhudumu aliyechaguliwa na Mungu. Ni Mungu pekee

anayetupatia huduma, na tunatambua ni huduma gani pale tu tunapokuwa katika uwepo wake (Hesabu 17:8).

Hapa ndipo tunapoweza hasa kupokea ahadi za Mungu katika Neno lake. Tunapozipokea hapa, tunajua kwamba tutakuwa nazo!

Neno la Mungu katika wafilipi 4:19 linasema "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Hapa unakuwa katika utukufu! Huu hapa utajiri wote wa mbinguni unakungojea.

Anza kumshukuru Mungu kwamba mambo haya matatu siyo tu kwamba yapo mbele zako, bali pia yako **NDANI** yako. Siyo tu kwamba yako **NDANI** yako lakini damu na kiti cha rehema na malaika wanakulinda kwa hayo. Katika Zaburi 91 tunasoma kwamba malaika zake watakulinda katika njia zako zote.

Sasa umeandaliwa kuwa mwombezi hasa. Unashiriki huduma ya Ukuhani Mkuu wa Yesu na kuwaombea wengine ipasavyo. Yesu alisema katika Yohana 15:7 "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

**Huu unapaswa kuwa muda mzuri wa kustarehe na kufurahi katika uwepo wa Mungu.** Tumia muda wa kutosha hapa katika hali ya ukimya na kufurahia kuwa pamoja naye. Hupaswi hata kuongea. Mungu anafurahia jambo hili. Wewe pia utorialifurahia. Jambo hili ndilo lililozungumzwa katika somo hili, yaani kuingia katika uwepo wa Mungu! Usisome tu jambo hili na kuendelea.

**Amua kabisa kwamba kila siku utafanya zoezi la kuingia katika uwepo wa Mungu.** Jambo hili ni muhimu sana ili kupata ushindi katika maisha haya na yale yajayo.

## Kiambatisho F

### Kujichunguza Kiroho

- **Upendo** - Je unawatendea wengine kwa upendo wa Mungu usio na masharti?
- **Ubinafsi** - Kuweka mahitaji yako mwenyewe juu ya mahitaji ya wengine. Upendo hujishughulisha na ustawi wa mtu mwengine - je wewe unajijali mwenyewe zaidi na kujali tu jinsi unavyojisikia?
- **Kuiba** - Je unaweza kukumbuka fedha ulizopokea kwa mali iliyokuwa si yako?
- **Kulaghai** - Je, ulipata kitu chochote kutoka kwa mtu fulani kwa njia isiyo ya haki?
- **Kusema uongo** - Aina yoyote ya udanganyifu wa kukusudia
- **Kashfa** - Kumsema vibaya mtu fulani. Kumkashifu mtu siyo lazima useme uongo - Je, umewahi kuwasema wengine bila upendo?
- **Ufisadi** - Je, unajisikia hatia kuamsha tamaa usizoweza kuzitimiza kwa haki? Ufasiki, uchafu wote, hata kama ni juu ya mwili wako mwenyewe.
- **Ulevi** - Utumiaji wa madawa ya kulevyo, karamu za ulevi.
- **Lugha chafu au matusi** - maneno maovu mazungumzo mabaya au yasiyo na maana, uchafu, mazungumzo machafu, ya kipumbavu, ya kipuzi, ya upotovu.
- **Wivu** - Kwa kawaida mahali penye mazungumzo yanayohusu makosa au kushindwa kwa wengine, kuna wivu uliojificha.
- **Utovu wa shukrani** - Ni mara ngapi wengine wamekufanya vitu lakini hukushukuru?
- **Hasira** - Je, umewahi kukasirika?
- **Kulaani** - Umetumia lugha ya matusi.
- **Utani** - Maneno yasiyohitajika, maongezi ya kipumbavu, kuongea na kutenda kama punguani. Masihara na mzaha na utani wa vitendo unaoelekea kudhoofisha viwango vitakatifu na vyenye thamani vya maisha. Je, umewahi kulitania kabila fulani au sehemu fulani ya

ulimwengu, taifa au mkoa katika nchi yako, au mwanasiasa fulani? Mizaha ya kikabila au kimikoa haina nafasi katika utakatifu.

- **Ukali** - Ulijibu mapigo, ulinung'unika au kurudisha mabaya kwa mabaya?
- **Tabia** - Je, kila wakati una uchu upitao kiasi? Na vipi kuhusu tabia yako ya ulaji?
- **Hali ya kuwa shingo upande** - Unaweza kukumbuka nyakati ambazo kwa makusudi kabisa ulikwepa kufanya wajibu wako kwa ukamilifu?
- **Kizuizi** - Umeharibu imani au matumaini ya wengine kwa kupoteza bure muda wao? Je, umemghilibu mtu aliyejewa na imani na wewe?
- **Unafiki** - Je, maisha uliyoishi siku za nyuma, yamewafanya baadhi ya watu waone kwamba yale uliyoyasema juu ya Kristo na Injili yake ni ya uongo?
- **Kuvunja nadhiri** - Je, kuna nadhiri yoyote uliyoweka mbele za Mungu ambayo hukuitimiza?
- **Kutokusamehe** - Je, una kinyongo au uchungu dhidi ya mtu mwininge, rafiki au adui?
- **Mafarakano** - Misuguano, roho ya kuwa na vikundi vinavyotofautiana.
- **Kutamari** kuishi kitajiri na kutapanya mali, ulafi. Kutumia pesa kupita kiasi kwa kanunu vitu madukani. Kupoteza muda bure.
- **Kutowatendea** výema au kwa upendo na heshima, wake, waume, watoto na wazazi.
- **Kutoridhika**, kuwa na wivu kwa ~~sababu~~ wengine wana vitu lakini wewe huna.
- **Kuabudu sanamu** - Shauku yoyote katika maisha yako inayozidi shauku ya kuishi na Mungu.
- **Ugomvi** - Umechochea ugomvi kwa maneno yasiyohitajika?
- **Uchawi** - Kumtawala mwininge kwa hila ili kutimiza haja zako.
- **Kuasi mamlaka** - Mkuu wako wa kazi, mwalimu, mzazi, kiongozi wa kiroho, nk.
- **Kuupenda ulimwengu** - Pamoja na: tamaa za macho - unasoma au kutazama nini? Tamaa za mwili - unatamani nini? Kiburi cha uzima - Ni jambo gani katika maisha unalofikiri kwamba unaweza kulifanya bila Mungu kuhusika? - Kujifanya kuwa mkubwa au mdogo kuliko jinsi ulivyo kwa njia ya mawazo au kwa kuishi.
- **Kiburi** - ni dhambi kubwa kuliko zote. Chunguza maeneo haya.

- Je, unaangalia tu kushindwa au makosa ya wengine au unajishughulisha tu na mahitaji yako ya kiroho?
- Unajihesabia haki na kuwakosoa wengine au una huruma na moyo wa kusamehe, ukitafuta yaliyo bora kwa wengine?
- Je, unawaangalia wengine kwa dharau au unawaheshimu wengine wote na kuwaona bora kuliko wewe?
- Je, unajitegemea na kujitosheleza mwenyewe au unawategemea wengine na kutambua kwamba unawahitaji?
- Ni lazima udumishe hali ya kuwatawala wengine au uko tayari kuacha kutawala?
- Je, ni lazima uthibitishe kwamba uko sahihi, au uko tayari kuiachia haki ya kuwa sahihi?
- Una roho ya kuhitaji tu au roho ya utoaji?
- Unatamani kutumikiwa au una hamasa ya kuwahudumia wengine?
- Unatamani kupandishwa cheo au unafurahi wengine wanapopandishwa cheo?
- Unahitaji kupewa sifa au unafurahi wakati wengine wanapotambuliwa?
- Unasikia kujiamini kwamba unajua mengi, au yale ambayo bado hujajifunza yanakufanya uwe mnyenyeketu?
- Unajifahamini jinsi ulivyo au hujishughulishi na maisha yako kabisa?
- Unawaepuka wata au unatafuta kuwa karibu na wengine? Uko tayari kuchukua jukumu la kuwapenda watu kwa moyo?
- Unafanya haraka kuwalaumu wengine au uko tayari kukubali kuwajibika?
- Wewe ni mtu usiyetaka kukaribiwa na wengine au ni mtu rahisi kuwasikia wengine wanapokusihu?
- Wewe ni mtu unayejitetea unapokosolewa au unakubali kukosolewa kwa unyenyeketu na moyo mweupe?
- Unajishughulisha kutafuta kuheshimiwa au kuwa kama ulivyo?
- Unajishughulisha na yale ambayo wengine wanafikiri au yale anayofikiri Mungu?
- Unajitahidi kudumisha hali yako au hadhi uliyo nayo?
- Je, unaona vigumu kuwashirikisha wengine mahitaji yako ya kiroho au uko tayari kuwa wazi?
- Unajaribu kuficha dhambi zako au uko tayari kuonekana wakati unapokosea?

- Unajisikia tabu kusema, “Nilikosea, tafadhali nisamehe”?
- Unapoungama dhambi, unaungama kwa ujumla, au unakiri na kuzitaja kabisa dhambi zile ulizotenda?
- Unajutia dhambi zako unapokamatwa au unasikitika kwa kuzitenda na unafanya haraka kutubu?
- Wakati hali ya kutoelewana au migongano inapotokea, unangojea wengine waje kuomba msamaha au wewe ndiye unayeanza kufanya hivyo?
- Je, unajilinganisha na wengine na kujiona kwamba unastahili heshima au je, huwa unajilinganisha na utakatifu wa Mungu na kusikia hitaji kubwa la kupewa rehema?
- Je, unafikiri una mambo machache au huna kabisa mambo ya kutubu au kila siku una moyo wa toba?
- Je, unafikiri kila mtu anahitaji uamsho au kila siku unasikia hitaji la kupata upya ujazo wa Roho Mtakatifu?
- Unajivuna unapokaa na Mkristo mpya au unafurahia ari yake? Uko tayari kujifunza kutoka kwake?
- Je, unaogopa unapokaa na Mkristo aliyekomaa zaidi yako, au una njaa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayotokana na uzoefu wake?

### **Upasuaji unahitajika?**

**Iwapo Roho Mtakatifu anatuonyesha dhambi**, tunahitaji kwenda pale ambapo Bwana alikutana nasi kwa mara ya kwanza. Ni pale msalabani. Tunamuona Yesu kwiya amesulibowi tena, kwa ajili ya dhambi hiyo, amebeba adhabu yetu.

**Damu inachuruzika chini kutoka msalabani.** Hali hiyo inapaswa kutushtusha na kutuhuzunisha kwa sababu tunaona hukumu ya Mungu ya kutisha. Tunahitaji kufahamu kwamba ghadhabu yote na hukumu ya Mungu iliwekwa juu ya Yesu msalabani.

**Yesu anatusubiri pale**, siyo kutuhukumu, bali anafurahi tukienda msalabani na kumpa dhambi zetu. Wakristo wengi wanapotambua dhambi humkimbia Mungu kwa aibu na kujisikia hatia.

**Dawa ya Mungu ya dhambi ni kwenda Msalabani**, kwenda Patakatifu pa Patakatifu katika uwepo wake na kuruhusu tabia yake itawale tabia yako. Utakatifu wake utaondoa dhambi zako. Hii pekee ndiyo dawa. Hatuwezi kufanya jambo hili sisi wenyewe. Ni kanuni ya kuondoa na kuweka. Hatuondoi dhambi zetu, Mungu ndiye anayetujaza utakatifu na upendo wake na dhambi lazima iondoke. Usikate tamaa iwapo inakubidi kufanya hivi mara kwa mara. Mungu hatuhukumu.

Anayefanya hivyo ni Shetani. Mungu atakukaribisha kila wakati utakapomwendea. Ukiacha kumwendea hapo ndipo anapohuzunishw.

**Tembea katika nuru ya kweli.** Acha kujidanganya, ikabili dhambi hii kama ilivyo. Iache kabisa kwa moyo wa dhati. Simama upande wa Mungu na kuipinga dhambi hiyo. Kusudia moyoni mwako kutoirudia KAMWE.

### **Kuungama:**

**“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu** na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”(1 Yoh 1:9).

**“BWANA amejaa huruma na neema** Haoni hasira upesi, ni mwinci wa fadhili. Yeye hatateta siku zote, wala hatashika hasira yake milele. Hakututenda sawasawa na hatia zetu, wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu; maana mbingu zilivyo inuka juu ya nchi, kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.” (Zaburi 103:8 - 12).

**Msamaha siyo tu kuondoa.** Msamaha ni neno zito linalomaanisha kukata na kuondoa kama daktari wa upasuaji anavyokata na kuondoa saratani. Msamaha wa dhambi unamaanisha kwamba dhambi imeondolwa kwako na kuwekwa kwa Yesu aliyeibeba msalabani.

**Kuungama ni kukubaliana na jinsi Mungu** anavyoliona jambo na kulitamka kwa kinywa chako. Kuungama siyo kutamka tamka tu, ni pamoa na kukubaliana na Neno. Unyenyeketu ni kukubali kwamba umekosea.

**Je, utafanya hivyo sasa?** Uko tayari kama mtoto mdogo kumwendea Baba yako mwenye neema na upendo na kungama dhambi zako na kuomba msamaha kwa unyenyeketu?

**“Ee Mungu, unajua upumbavu wangu,** wala hukufichwa dhambi yangu...kwa ajili ya jina lako, Unisamehe uovu wangu, maana ni mwinci...BWANA kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, ili Wewe uogopwe.

Ee Mungu Baba yangu, nakuja mbele zako kuungama dhambi yangu (zangu) ya (za): (Sasa zitaje na kuziungama.)

Neno lako linasema kwamba matendo haya au mwenendo huu ni dhambi nami nakubaliana na Neno lako. Sina udhuru. Sitaki tena kufanya dhambi hii ndani ya roho, nafsi na mwili wangu. Nataka kuiacha na kutupa mbali nami. Inanitenganisha mimi na wewe. Inaniharibu. Nataka kuponywa, roho, nafsi na mwili, na pia nataka

kuwa karibu na wewe. Napokea msamaha wako. Asante kwa kuweka dhambi hii juu ya Yesu, na asante kwa kuwa aliiweka juu ya Msalaba wake kwa ajili yangu. Najua sistahili msamaha lakini nashukuru kwa kuniweka huru.”

**Malipizo ni utayari** wa kulipa au kurudisha kitu fulani kila inapowezekana. Iwapo sasa umesamehewa mbele za Bwana , uko tayari kumwomba akupe ujasiri wa kuungama na kufanya malipizo kwa wengine uliowakosea? Ukitaka kuwa huru kweli kweli dhamiri yako lazima iwe safi mbele za Mungu NA wanadamu. Huwezi kumtetea Mungu huku unajiona mchafu mbele za macho ya watu wengine.

**Kumbukumbu za kushindwa kwako** mbele ya macho yao zitakuingiza ndani sana katika utumwa kila wakati unapowakumbuka. Kama hujawaomba msamaha, hali ya kujihisi una hatia itaiua imani yako na kukuibia mwelekeo na nia yako. Hata hivyo, hupaswi kuungama kila dhambi kwa kila mtu; ni dhambi zile tu ulizowatendea watu unaowajua.

**Kanuni:** Maungamo yanapaswa kufanywa kulingana na dhambi zilizotendwa. Kama ultenda dhambi mbele za Mungu peke yake, Mungu atakusamehe na kusahau uliyoyatenda (Zaburi 103:8-13; Isaya 43:25; Yeremia 31:34). Dhambi ulizotenda mbele za Mungu na wanadamu ni lazima uzitubu mbele za wote WAWILI, Mungu na mtu (watu) uliyemkosea (uliowakosea).

Baadhi ya yale yaliyoma katika Kiambatisho F yalichukuliwa kutoka katika vijitabu vya Winkie Pratney vilivyochapishwa katika mtandao wa kompyuta (www)

## Sura ya 3 – Wafungwa katika Nchi ya Ahadi

**Agano la Kale lilitolewa kwetu kama kielelezo na onyo ili tujifunze kwalo.** Tunasoma katika 1 Kor 10:11 kwamba “Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani.”

Nchi ya Ahadi katika Agano la Kale ilikuwa nchi ya Kanaani. Nchi hiyo haikuwa kamili; maadui wa wana wa Israeli walikaa katika nchi hiyo, yenye vita na mapambano. Nchi yetu ya Ahadi siyo mbinguni, ni hapa hapa na tena wakati huu huu tunarithi ahadi za Mungu katika maisha yetu kama wakristo. Maadui zetu bado wapo hapa na wanaweza kutufanya wafungwa, hata katika nchi yetu ya ahadi! Usifikiri kwamba eti kwa sababu sisi ni wakristo hatuwezi kudhurika na vifungo nya Shetani.

**Katika Agano la Kale Wana wa Israeli walikuwa wafungwa katika Nchi yao ya Ahadi. Wakristo wanaweza pia kuwa wafungwa, na wengine tayari wamefungwa na Shetani lakini hawajui jambo hilo.**

**Onyo! Jambo hili ni la kisirisiri. Linaweza kuwa hatari kwa afya yako!** Kwa kuwa Shetani hakuweza tena kuwafanya watu wa Mungu wakae katika njaa, alijaribu kuwafanya watumwa katika nchi ya Misri. Alijaribu tena kuwaangamiza jangwani walipokuwa safarini kuelekea Nchi ya Ahadi lakini hakuweza kuwazuia katika mto Jordani wala Yeriko. Lakini waipofika katika Nchi ya Ahadi, aliwapata katika mji mdogo uitwao Ai. Kwa nini? Kwa sababu ya dhambi zao wenyewe. Dhambi zikawa **adui wa ndani**, sio nguvu za kijeshi zinazoonekana (Yoshua 7).

Kwa mamia ya miaka, wana wa Israeli walimlilia Mungu na akawaokoa kutoka katika mateso yao. Baadaye wakaanza tena kuabudu sanamu na kuwa wafungwa katika jambo jingine. Kwa nini?

“Kisha niliwaambia, Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu; msiiiche miungu ya Waamori, ambayo mwaketi katika nchi yao; **lakini hamkuitii sauti yangu(Neno)**” (Waamuzi 6:10).

Katika Waamuzi sura ya 6 Mungu alimwenda Gideoni katika hali aliyokuwa nayo. Waebrania walikuwa katika Nchi yao ya Ahadi, lakini kila walipopanda mbegu, Wamidiani na Waamaleki waliyavamia mashamba yao na kuyaharibu mazao. Wakaiba mbegu kama jinsi Shetani anavyoiba mbegu ya Neno la Mungu. Kwa hiyo hawa watoto wa Mungu walikuwa kwa hakika wamefungwa na adui yao, ingawa walikuwa katika Nchi ya Ahadi.

## Agano la Kale linaonyesha jinsi watu wa Mungu walivyoishi kama wafungwa katika nchi ya ahadi.

Ha! Ingawa ni Wakristo,  
ninaweza kuwafanya  
wafungwa



**Hivi ndivyo adui anavyofanya ili kukunasa.** Hutafuta yale matendo ya mwili wako (utu wako wa kale) ambayo hutayaacha.

**Atakushawishi kwamba huna haja ya kuishi kwa kulifuata Neno la Mungu, eti unaweza kuishi unavyotaka mwenyewe. Atakushawishi kwamba huna haja ya kuufuata ufalme wa Mungu na utaratibu wake wa kuzaa matunda.**

Baada ya muda huyang'ang'ania yale matendo ya mwili na hatimaye unajikuta umedanganywa na pepo hili. Haina maana kwamba utakuwa umepagawa na pepo, la hasha, bali utakuwa umearthiriwa na pepo. Mambo haya huwa ngome na kukufanya ujisikie huna matumaini. Wewe ni Mkristo katika nchi ya Mungu ya ahadi, hata hivyo umefungwa kama wale watu wa Agano la Kale. Wewe si mteule tena unayetoa maji yatiririkayo ili kuwasaidia wengine. Shetani ameusimamisha mto kwa kuwa umempa nafasi.

**Shetani anaweza kutuweka katika vifungo gani?**

**“Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaameta, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi” (Yohana 8:34).**

**Magonjwa, maradhi**

**Ukosefu wa fedha**

**Kutokupendwa.** Kama hatupati upendo usio na masharti kutoka kwa wazazi wetu, tuko kifungoni.

**Ubinafsi,** au kujipenda mwenyewe ni kinyume cha upendo wa kweli. Huku ni kufikiria kwamba wewe ni kitovu cha dunia na kwamba vitu vyote vinakuzunguka.

**Kujidharau** – hali ya kujiona hufai, umeshindwa. Hatupaswi kusikia jinsi tulivyo kutoka mahali pengine au kwa mtu ye yeyote isipokuwa Mungu na Neno lake. Mwili na Ulimwengu vinajaribu kutuwekea hali isiyo ya kweli kuhusu jinsi tulivyo. Ama tunajiona wakubwa sana na kujivuna, au tunajiona hatufai, tumejaa aibu na unyonge. Njia nzuri ya

kushinda jambo hili ni kujua kwamba Mungu anaishi ndani yako, na kwamba kila uendako umebarikiwa kwa sababu unatembea pamoja na Mungu. Kila unayekutana naye amebarikiwa na wewe kwa sababu wewe ni chombo cha udongo kilichojazwa utukufu wa Mungu. Hata kama wengine wanakuona tofauti, wewe endelea tu kujiona umebarikiwa. Kazi yako au biashara yako haikutambulishi jinsi ulivyo. Unapokwenda kazini kwako, unaipa heshima kazi hiyo. Yesu alipowatawadha miguu wanafunzi wake, ilikuwa kama kusafisha choo, lakini kwa kuwa Mungu ndiye aliyefanya hivyo, kutawadha miguu limekuwa jambo la heshima.

**Wajane na Yatima.** Yakobo 1:27. Mungu ameweka mkazo maalum kuhusu hali ya wajane (neno hili linajumuisha pia watu waliopewa talaka) na yatima (neno hili linajumuisha pia watoto wa mtu aliyepewa talaka. Hali hii inahusu kukosa kuwa na mamlaka, mtu wa kukufunika na kumkosa baba. Linahusu pia hali ya kuachwa bila ulinzi au mtu wa kukutetea. Agano la kale limejaa maonyo kwa Wana wa Israeli wawatunze wasio na baba na kuwajali wajane. Kanisa la leo linapaswa kufanya vivyo hivyo.

Wote tunahitaji usalama, hivyo mtu anapokuwa mjane au yatima anakuwa amekosa sana usalama. Nawafahamu watu waliopata shida sana baada ya kuwa wajane au yatima. Iliwachukua muda mrefu kuweza kuikabili hali hiyo. Sisi kama waamini, tunapaswa kuuwakilisha moyo wa Mungu kwa wajane na yatima. Moyo wake unawatafuta ili kuwapa faraja maalum na kuwapa mahitaji yao. Yeye ndiye anayewafunika, yeye ndiye usalama wao. Kama umewahi kuwa "mfungwa" wa aina hii, unahitaji kujua kwamba Mungu anasema katika Yakobo 1:27 kwamba ibada ya kweli "dimi" ya kweli na kumcha Mungu ni lazima viambatane na kuonyesha moyo wake wa upendo unaojali wajane na yatima. Hii ni kauli muhimu sana ya Mungu, hivyo unahitaji kujua jinsi anavyopendezwa na wewe na jinsi anavyokujali! "Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane, Mungu katika kao lake takatifu." (Zaburi 68:5).

**Ukwasi** – Kuutumainia ulimwengu ukupatie vitu unavyovihitaji katika maisha, badala ya kumtumaini Mungu.

**Kudhalilishwa** – Watu wengi sana wamedhalilishwa kijinsia na kwa namna nytingine.

**Kujihesabia haki** ni kifungo kikubwa sana. Hii ni hali ya kujiona bora kuliko watu wengine kutockana na jinsi unavyofanya mambo kwa nguvu zako mwenyewe.

**Maadui wengine** ni kutokusamehe, hatia, kwenda kinyume na maadili, zinaa, uchungu, umbeya, hasira, kukosa kuwa mwaminifu na mkweli.

**Ulevi** – kuna ulevi wa aina nyingi, lakini kwa ujumla ni kutawaliwa na tabia au mambo mabaya badala ya upendo wa Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**Wengi wamenaswa** katika laana za vizazi kama vile kushindwa kuonyesha upendo na huruma, kukaa katika hali ya utumwa, kuwa mtu anayetafuta tu kuwapendeza watu, kuwa mtu asiyeridhika na chochote au anayetaka kufanya onyesho kwa lengo la kujitokuza. Maeneo mengi katika hayo hujidhihirisha katika mahusiano yaliyoharibika, kutoweza kuishi kwa amani, kutoweza kuridhika.

**Uchawi** au kuwatawala wengine. Unaweza kuwa mwathiriwa au mkosaji.

### **Hata hivyo ninaamini kwamba mojawapo ya masuala yaliyoenea sana ni KUKATALIWA**

**Ninaamini kwamba kukataliwa** ni mzizi wa mamia ya matatizo mengine. Tunahitaji kukubaliwa na wazazi wetu bila masharti yoyote tunapokuwa wadogo. Tunahitaji kukubaliwa na wenzetu, wenzi wa ndoa nk. Katika jamii ya leo, watu walioharibika husababisha pia uharibifu kwa wengine kwa njia ya kuwakataa na hii huenea kutoka kizazi hadi kizazi. Hatiwezi kuonyesha upendo kwa wengine bila kuupokea kwanza upendo huu. Neno la Mungu katika 1 Yoh 4:19 linasema hivi: “Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.” Dawa ya Mungu ya kutibu hali ya kukataliwa na sehemu mbili

1) Alichukua kukataliwa kwetu na kuitiba hali hiyo kwa ajili yetu. Biblia inasema katika Isaya 53:3 kwamba, “Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.”

2) Anatukubali bila masharti kwa upendo wake mkuu! Katika Waefeso 1:6 tunasoma maneno yafuatayo, “Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha(ametukubali) katika huyo Mpendwa.”

**Yesu hatuhukumu katika maeneo haya.** Yesu anataka kutuweka huru. Hii ndio misheni yake. Lakini sisi wenyewe tunahitaji kuwa waaminifu, tutupe mbali kiburi chetu na kuwa tayari kushiriki hatua za uponyaji utakaotuweka huru.

**Gideoni ni mfano wetu wa mfungwa aliyewekwa huru**, na yeye akawaweka huru watu wake! Gideoni alizaa matunda kwa ajili Mungu.

### Fuata njia ya Gideoni – Waamuzi sura ya 6

• - 6:1 **Aliathiriwa na tabia ya baba zake ya kuabudu sanamu.** Watu wake walikuwa katika kifungo cha umaskini kwa muda wa miaka 200 ya kuabudu sanamu. Kitu cha kwanza tunachohitaji kufanya ni kuwasamehe wale waliotuweka katika vifungo hivi. Tusipotoa msamaha huu, kwa moyo wa dhati, hatua zinazofuata za kutuweka huru hazitatimilika. Kama tumeshindwa kusamehe ni lazima tuungame dhambi hiyo kwa Bwana na hapo ndipo tutakapopata msamaha wake.

• - 6:1-11 **Alikuwa akijitahidi** sana kwa nguvu zake kuyafanya maisha yawe mazuri, lakini alishia kushindwa tu, kujiona hafai na kukosa matumaini. Alikuwa akijificha chini ya ardhi katika pipa lake kubwa la divai ili kuwaepuka Wamidiani waliokuwa wakija kwa wingi kuiba mazao na mifugo. Yeye na watu wake walijitahidi sana lakini hawakuweza kuwashinda maadui. Midiani walikuwa maadui walioyapiga malisho ya Bwana na kuiba mbegu. **Kwa njia hiyo hiyo, wamidiani wa leo, mapepo, huliiba Neno la Mungu ili kutuzuia tusizae matunda.** Hebu angalia, walingojea mpaka pale Wana wa Israeli walipopanda mbegu, ndipo walipokuja kuyavamia mazao na kuyaharibu. Walikuja kama nzige, na Wana wa Israeli wakawa maskini sana.

• - 6:8 **Mungu akasema na wana wa Israeli.** Kwa rehema yake, Mungu alisikia kilio cha wana wa Israeli, akamtuma nabii. Rehema zake ni za milele. Nabii akawaambia wana wa Israeli kwamba Mungu ndiye Mungu wao, alikuwa amekwishawatoa katika vifungo au utumwa lakini sababu iliyowafanya wawe katika utumwa tena (safari hii katika Nchi yao ya Ahadi) **ni kwamba hawakuitii sauti ya Mungu (Neno la Mungu).** TUSIPOISHI kwa kulifuata Neno la Mungu kila siku, ni hakika tutakuwa watumwa na wafungwa wa maadui zetu. Hakuna njia nyininge.

• - 6:12 **Mungu akasema na Gideoni.** Malaika wa Bwana, mwakilishi binafsi wa Mungu, akaja kwa Gideoni. Inawezekana Yesu alijitokeza kwa njia hii wakati wa Agano la Kale. Alimwita Gideoni “Shujaa”. Kwa nini alimwita shujaa mtu aliyekuwa akiishi kama mwoga, mtu ambaye hakujistahi, aliyekuwa akipura ngano kwa

kujificha ili kwamba maadui zake wasimuone? Siku zote Mungu hushughulika na sisi kwa njia hii; huona jinsi tutakavyokuwa. Huyataja yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako (Rum 4:17). Haangalii jinsi tulivyo, bali jinsi tunavyoweza kuwa katika yeye. Haya ni maneno ya imani yanayoongea.

• - 6:13 **Gideoni alikuwa mwaminifu mbele za Mungu.**

Alimwambia jinsi alivyojisikia; “ikiwa Bwana yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Watu wengi huuliza maswali haya. Kama Mungu ni upendo, kwa nini watu wema wanateseka? Kama nimekuwa nikintumikia Mungu, kwa nini basi ninapita katika wakati huu mgumu sasa?” Alimuuliza Mungu “yako wapi matendo yake ya ajabu, waliyotuhadithia baba zetu, wakisema, Je, siye Bwana, aliyetuleta huku kutoka Misri? Ila sasa ametutupa, naye ametutua katika mikono ya Midiani.” Alijisikia kana kwamba Mungu amemwacha.

• - 6:18-21 **Mungu alijifunua mwenyewe kwa Gideoni kama Mungu afanyaye agano.**

Alimuonyesha Gideoni jinsi yeye Mungu alivyo; alimuonyesha pia Gideoni nafasi yake halisi kama mshiriki wa agano pamoja na Mungu. Mara nyangi sana Mungu hujibu maswali yetu kwa ufunuo wa jinsi Yeye alivyo!

• **Gideoni alimletaea Mungu vitu vivilvyo bora. Gideoni aliubeba msalaba wake mwenyewe.** Gharama ya mbuzi na mkate uliookwa nyumbani ambao Gideoni alileta ilikuwa kubwa kupita kiasi kwa mtu aliyejewa katika mazingira ya kimaskini. Sio hilo tu, Gideoni alipika supu!

• **Gideoni aliona msalaba wa Yesu.** Ingeweza tu kuwa unga wenye gharama, lakini Mungu aliugeuze ukawa unga wa agano. Katika kitabu cha Mambo ya Walawi 2:1 sadaka ya minyama au unga ilipaswa kuteketezwa madhabahuni na kuhani. Kitendo cha Malaika wa Bwana kuiteketeza sadaka ya Gideoni kwa ncha ya fimbo yake kilikuwa ishara ya agano. Ninaamini kwamba katika fikra za Kiebrania za Gideoni, siku hiyo aliona agano la damu kati yake na Mungu. Alimuona Mungu akibadilishana naye uwezo, jina na mazingira.

• **Agano la Damu hubadilisha familia yako, jina lako, na urithi wako.** Gideoni alipata jina la Mungu, na Mungu alipata jina la Gideoni. Shujaa: lilikuwa jina la Bwana, mtu dhaifu aliyeshindwa: lilikuwa jina la Gideoni. Walibadilishana.

• - 6:22 **Katika hali bora zaidi Gideoni aliweza kumsikia Mungu akinena.** Hii ilikuwa tabia kuu ya Gideoni. Alitumia muda mwingu kujenga uhusiano na Mungu na akaendelea kumsikia Mungu akinena.

• - 6:23-24 **Alikuwa na amani ya Mungu kwa sababu ya Msalaba. (Yehova-Shalomu).**

• - 6:25-32 **Ilimbidi Gideoni abomoe sanamu za kifamilia.** Baada ya kupata uzoefu wa msalaba wa Yesu tunahitaji kuziangusha madhabahu. Hali ya kuabudu sanamu imejengwa juu ya kitu kimoja tu: KUJIPENDA. Hii hufanyika mara nyingi zaidi ya kuchukua msalaba wetu. Sanamu haziko wazi sana siku hizi kama ilivyokuwa nyakati za Agano la Kale. Sanamu ni kitu chochote kinachokufanya uenende kimwili badala ya kiroho. Kipimo sahihi zaidi ni nini au ni nani unayemwabudu? Kipimo sahihi zaidi kwa ibada ni nani unayemtii: Fikira zako, mwili wako, mtu mwagine au Roho wa Mungu na Neno la Mungu? Kuenenda katika mwili ni kutii mwili wako (tamaa za asili) na kuenenda kwa Roho ni kumtii Roho Mtakatifu na Neno la Mungu. Ili mtu aweze kubomoa sanamu inabidi alishike Neno la Mungu na kuwa na ushirika na Roho Mtakatifu; kwa njia hiyo ataweza kuacha kutii tamaa zake za asili.

• **Kwa mfano katika Warumi 12:1** baada ya Mungu katuonyesha rehemta tulipokuwa tumepotea, na tena baada ya kuutoa msalaba na neema yote katika Warumi sura ya 1 hadi ya 11, alisema "...nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu ilioy hai..." Kwa maneno mengine, bomoa miungu yako kama Gideoni alivyofanya. Vitoe viungo ~~hukumtu~~ vyako vyote kwa Mungu, mpe mwili wako uwe chombo cha udongo kilichoazwa na Mungu kama Adamu alivyopaswa kuwa. Uwe tayari kuwa "totau" kwa ajili ya Mungu, usiifuatise namna ya dunia hii.

• - 6:34 **Baada ya kubomoa sanamu, Gideoni alijaa Roho wa Mungu.** Akawa na nguvu ya Mungu. Gideoni alikuwa na nguvu ya kumtii Mungu na kuacha kutii fikra zake na mazingira ya asili katika maisha yake. Kitu cha kwanza kilichotokea ni kwamba adui alishambulia. Kwa kawaida, tunapobomoa sanamu za kiroho, tunaweza kutazamia kuona vita.

• - 6:36-40 **Alijifunza kuwa na ushirika na Mungu kwa kiwango imara** cha imani bila kujali hali ya mazingira (labda pia kwa sababu ya mazingira).

• **Gideoni alizaa matunda kwa ajili ya ufalme wa Mungu.** Akawa mmojawapo wa wakombozi wakubwa wa watu wa Mungu katika historia. Soma Waamuzi 7 hadi 8:21 utapata habari za vita. Mungu akamgeuza mtu aliyeshindwa, aliyeishi katika mazingira yasiyo na matumaini kuwa mshindi mkubwa katika historia kwa sababu ya mambo mawili: 1) Msalaba, na 2) Hali ya Gideoni ya kuuthamini

msalaba kiasi cha kuwa tayari kwenda vitani kwa ajili ya Mungu na kumfanya Mungu kuwa kiini cha maisha yake yote, sio tu kumpa nafasi ya kwanza au ya pili; na ushirikiano wa Gideoni katika kubomoa au kuangusha sanamu na ngome.

**Ingawa Gideoni alikuwa akitawaliwa na dhambi za ukoo, laana** na hali ya kuabudu sanamu, Malaika wa Bwana alileta Msalaba katika eneo lile pamoja na dhabihu, akasema, "Kijana mwanamume, hakuna njia nyingine, isipokuwa kukuondolea laana na dhambi zako. Kwa sababu ya agano hili, ninakuondolea dhambi zako, laana za ukoo wako, dhambi za vizazi vyako ulizorithi na matokeo ya kuabudu sanamu, yaliyosababishwa na wewe na mababu zako. Nitalifuta jina lako 'lililolaaniwa na Mungu' na utaitwa kwa Jina langu, Shujaa."

Gideoni akakutana na Mungu pale pale alipokuwa. Mungu hakutaka Gideoni ajifanye kuwa mtu wa aina fulani wakati hayuko hivyo. Lakini Mungu alikuwa na imani naye. Gideoni alijifunza kwamba huwezi kupata ushindi kwa nguvu zako mwenyewe bali kwa kuzaa **MATUNDA**. Alijifunza kwamba alikuwa **MFUNGWA KATIKA NCHI YA AHADI**. Alijifunza jinsi ya kuwa rafiki wa Mungu (**MTO UTIRIRIKAO**), alijifunza **MUNGU NI NANI**. Alijifunza pia **KUKETI, KUENENDA na KUPINGA**. Na matokeo ya mwisho ni matunda kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Sura ya 4 - Mungu ni nani

**Unaweza kumjua Mungu. Anataka ushirika na wewe. Mungu anataka utegemee kuwa na mawasiliano na Yeye pasipo kutegemea matendo na desturi za kidini.  
Ili kumjua mtu fulani tunahitaji kujua tabia yake ikoje.**

**Jambo la kwanza tunalohitaji kujua kuhusu Mungu ni kwamba Yeye ni Muumbaji!** Licha ya kuwa Muumbaji, kwa njia yake, vitu vyote viro na hushikana pamoja.

Katika Wakolosai 1:16-17 tunasoma kwamba: “Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vivilyo mbinguni na vivilyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.”

Tunasoma pia katika Waembrania 11:3 kwamba “Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanya kwa vitu vivilyo dhahiri.”

Katika Waembrania 1:2 tunapata pia maneno yafuatayo: “mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Mstari wa 3b ...akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake.”

### **Hapa kuna kweli nydingine kuhusu Mungu**

1. Hakuumbwa na pia ni wa inele (Yohana 1:1-3 na Mwanzo 21:33)
2. Anaweza yote. (Luka 1:37)
3. Anajua yote. (Zaburi 147:5)
4. Yupo kila mahali. (Yeremia 23:23-24)
5. Mungu ni Roho. (Yohana 4:24)
6. Mungu ana nafsi tatu. Mungu Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. (Mathayo 3:16-17, Yohana 1:1-14, 14:9-20)
7. Hana mwisho. (Isaya 40:12-13)
8. Ni mwenye upendo. (Waefeso 2:1-7, 1Yohana 3:1, 1Yohana 4:9-10). Mungu HANA upendo, Mungu NI upendo. Mungu anatupenda kwa upendo usio na masharti. Upendo wake hautegemei jinsi tulivyo wema au wabaya. Tulipokuwa tumekufa katika dhambi, alitupenda. Mtu aliyekufa hawezি kufanya chochote isipokuwa kupokea uzima! Wanadamu hupenda kwa masharti.

- “Kama wewe ni mwema, au kama utafanya ninayokuambia, nitakupenda.” Mungu hayuko hivi! Anatupenda kwa sababu ye ye NI upendo. Upendo wa aina hii huitwa AGAPE, upendo usio na masharti.
9. Tabia yake ni tunda la Roho lililoelezewa katika Wagalatia 5:22-23.
  10. Habadiliki. Hisia zake haziwi moto na baridi kama wanadamu. (Waebrania 13:8). Katika Yakobo 1:17 tunaelezwa juu ya kivuli cha jua kinachobadilika badilika kadiri jua linavyosogea wakati wa mchana. Lakini Yakobo anasema kwa Yesu, HAKUNA kivuli cha kugeuka-geuka. Kwa maneno mengine, anang’aa siku zote kama mwezi mpevu! Unaweza kumtegemea.
  11. **Yesu ni Neno. Yesu ni Mungu.** (Yohana 1:1-2&14)
  12. Yesu alizaliwa na bikira. (Luka 1:26-38). Neno la Mungu katika Warumi 1:3-4 linasema hivi: “habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya Roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.” Hebu jaribu kuwaza kwamba uko mbele ya kijana Yesu unamuuliza swali hili: wazazi wako ni akina nani? Halafu Yesu anakujibu: “Unajua, kwa upande wa mama yangu, natoka katika ukoo wa Daudi, lakini kwa upande wa Baba yangu, mimi NDIYE.”
  13. Roho Mtakatifu ni Mungu. (Yohana 14:16-23)
  14. Zaidi ya yote, Mungu ni upendo! Anakujali zaidi ya jinsi unavyojiali wewe, na pia kuliko jinsi wazazi wako na ukoo wako wanavyokujali.

***Neno la Mungu katika ile mifano ya Yesu  
Luka sura ya 13, linalezeza upendo wa Mungu na jinsi  
anavyokujali wewe na mimi.***

Hakuna mchungaji mwenye akiili imani anayeweza kuwaacha kondoo 99 na kumwendea kondoo mmoja aliyejepotea, lakini Mungu hutufuata kule tulikopotelea.

Katika mfano mwingine wa pili, mwanamke alikuwa amepoteza matumaini yake. Mahari aliyohitaji ili aweze kuolewa ilikuwa shilingi 10, akapoteza shilingi moja. Kama asingeitafuta, angekaa katika umaskini au ingebidi auze mwili wake. Mungu hutufuata ili atufanye wazima na kutimiza matumaini na ndoto zetu.

Yule baba katika mfano unaofuata alikaa barazani akimngoea mtoto wake aliyejepotea arudi. Alipomuona kwa mbali, alifanya kitu kisichokuwa na heshima, alikimbia kwa haraka kadiri alivyoweza, akafunika uchafu wake ili wale watumishi wengine wasimuone, hakupenda mwana wake atahavarike.

## Baadhi ya maswali ya kawaida kuhusu Mungu

### Inabidi usimamishe saa ili uyaelewe

Je, Mungu anatupangia maisha yetu yawe namna gani? Ni nani mwenye amri juu ya maisha, Mungu au mimi au ulimwengu unaonizunguka? Je Mungu ana watu fulani tu watakaokolewa, na kwenda mbinguni, na wengine hawana nafasi? **Mambo mawili ya kukumbuka:**

1. **Mungu alimuumba mwanadamu na kumpa hiari ya moyo na kamwe hawezi kупингана na jambo hilo.**
2. **Mungu haishi kwa muda**, anaishi milele, sio muda mrefu bali muda usio na mwisho. Inabidi usimamishe saa. Mungu anajua yote kutoka mwanzo hadi mwisho.

Biblia inasema katika kitabu cha Kutoka na Warumi sura ya 9 kwamba Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu. Je, jambo hilo lilikuwa zuri kwa Farao? Mungu alijua kabla kwamba Farao asingekuja kwake, kwahiylo Mungu angeweza tu kumfanya mkaidi. Ukweli ni kwamba, Mungu HAAMUI kumfanya mtu awe mkaidi, lakini kuna kitu ndani ya mwanadamu kinachomfanya awe mkaidi mbele za Mungu, anapomkataa Mungu. Tunapomwambia Mungu hapana, kitu fulani ndani yetu huanza kuwa kigumu kidogo kidogo. Hatimaye hatuwezi tena kuchagua.

Mungu alijua jambo hili kabla. Lakini je, Mungu alilisababisha? **HAPANA!** Hiari ya Farao ndiyotyolilisababisha.

Mungu anasema katika Waefeso 2:10 kwamba Mungu alituumba tutende matendo mema. Ndiyo, kuna mpango kwa kila mmoja wetu, lakini ni juu yetu kuuchagua mpango huo.

Mungu ni mkuu, anatawala, lakini hufanya hivyo bila kuondoa hiari ya mtu, au hata hiari ya watu waovu wanaokula njama dhidi ya watu wa Mungu na makusudi yake.

**Hata watu na pepo ambaao ni maadui wa Mungu wanautekeleza  
mpango wake kwa ajili yake.**

Katika Zaburi 33:10-11 imeandikwa hivi, “BWANA huyabatilisha mashauri ya mataifa, huyatangua makusudi ya watu. Shauri la BWANA lasimama milele, makusudi ya moyo wake vizazi na vizazi.”

Tunasoma pia katika Zaburi 2:1-4 kwamba “Mbona mataifa wanafanya ghasia, na makabila wanatafakari ubatili? Wafalme wa dunia

wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja, juu ya BWANA, na juu ya masihi wake, na tuvipasue vifungo vyao, na kuzitupia mbali nasi kamba zao. Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka.”

Kama bado unashindwa kulielewa jambo hili, kumbuka tu kwamba, Mungu huishi milele, haishi kwa muda. Anayaona maisha yetu yajayo, maisha yetu yaliyopita na maisha tunayoishi sasa. Mungu huona yote hayo kwa wakati mmoja na kwa ufahamu huo, anatubariki. Lakini hawezi KAMWE kuingilia hiari yetu.

**Mungu ni Neno, na tunaweza kuliamini (kumwamini)**

Neno la Mungu linaweza kutabiri kwa uhakika mambo yajayo. Jambo hili halizezi kufanywa na yitabu yingine vya kidunia.

**Hii inathibitisha wazi kwamba Mungu pekee ndiye chanzo cha Biblia.**

Kuna aya au mistari 8,352 inayohusiana wazi wazi (au bila kuwa wazi sana) na unabii katika Maandiko matakatifu. Mstari kama mmoja hivi kati ya sita unazungumzia matukio yajayo. Changamoto kubwa ya Mungu kwa ulimwengu ni kwamba tumthibitishe. “Maana mimi ni BWANA; mimi nitanena, na neno lile nitakalolinena litatimizwa;...” (Ezekieli 12:25).

Wafuasi wa Budha, Konfyushasi, Muhammad wana maandiko yao matakatifu, lakini katika maandiko hayo suala la unabii halionekani wazi wazi. Kuharibiwakwa Tiro, kuvamiwa kwa Yerusalem, kuanguka kwa Babeli na Rumi matukio yote hayo yalitabiriwa na kutimizwa lakini maelezo yaliyotolewa ni kidogo sana. Kuingia kwa Yesu Yerusalem kulitabiriwa na nabii Daniel miaka zaidi ya mia moja kabla HADI SIKU YENYEWE! Siku na mwazi wa kuundwa kwa Israeli kama taifa jipya mwaka 1948 kulitabiriwa katika Agano la Kale.

Kuna unabii zaidi ya 300 ambao Yesu aliutimiza katika kuzaliwa kwake, maisha yake, kifo chake na kufufuka kwake. Hebu jaribu kuwaza juu ya matukio 17 tu ya unabii kati ya yale yanayojulikana sana.

Welekeo mchangamano unaoweza kutokea dhidi ya mambo hayo  
17 yaliyotabiriwa ni sawa sawa na:

Kwa hiyo kuhusiana na matukio 300 ya unabii uliotimia kuhusu Yesu, ni mzaha kufikiri kwamba unabii wote huo ultimia juu ya mtu

mmoja kwa bahati. Nafasi moja tu katika namba inayofuatiwa na sifuri 181! Ili uelewe vizuri jinsi namba au hesabu hii ilivyo kubwa, jaribu kuwaza juu ya mpira uliojaa elektroni (milioni bilioni mbili na nusu hufanya mstari wenyewe urefu upatao inchi moja). Sasa katika akili yako, hebu fikiria kwamba mpira huo umepanuka na kufikia ukubwa wa dunia, wenyewe kipenyo cha miaka ya mwanga bilioni nne (mwaka mmoja wa mwanga ni sawa na urefu ambao mwanga husafiri kwa mwaka mmoja kwa kasi ya zaidi ya maili 186,000 kwa sekunde. Sasa zidisha namba hiyo mara milioni 500 kwa kipawa cha nne. Halafu katika kontena hili kubwa lenye elektroni, ondoa elektroni **moja** tu uipake rangi nyekundu na kisha uirudishe kwenye kontena. Ichanganye na zile elektroni nyingine kwa miaka mia moja. Mfunge kidoto mtu mmoja (macho yake yasione kabisa), halafu mwambie aingie katika kontena hilo na mara moja tu bila kutafuta tafuta aichukue ile elektroni nyekundu. Je, si jambo lisilowezekana? Sasa kwa nafasi hiyo hiyo, Yesu Kristo aliishi, akafa na kufufuka na sasa yu hai kama maandiko yanenavyo eti kwa “bahati”!

Unabii mwininge wa Agano la Kale (nafasi haitoshi kuorodhesha kila unabii) ni pamoja na kuharibiwa kwa miji kama vile Tiro na mingine, na yote yalitimia kama ilivyotabiriwa kabla katika Biblia. Kuna nabii 1817 zizhusozo mada mbalimbali 737. Nabii hizo zinaonekana katika mistari au aya 8,352. Idadi hii ni asilimia 27 ya Maandiko Maajikitifu yote.

Neno la Mungu katika Isaya 42:9 linasema “Tazama, mambo ya kwanza yamekuwa, nami hayahibiri mambo mapya; kabla hayajatokea nawapasheni habari zake.”

### Yesu ni nani sasa?

Katika vitabu vya Injili tunaona Yesu alikuwa nani alipotembea duniani. Alituonyesha nafsi ya Mungu Baba yake. Yesu alituonyesha kwamba yecheza ni Mwanakondoo wa Mungu aliyechukua dhambi zako na zangu, na kujinyenyikeza hadi kupata kifo cha mhalifu msalabani, kifo ambacho mimi na wewe tungestahili.

Mtume Paulo alikuwa na ufunuo kuhusu mambo ambayo Yesu alitufanyia, ingawa Paulo hakukutana na Yesu katika mwili. Tunaona ufunuo huo katika nyaraka za Paulo.

**Hata hivyo Yesu alichagua kujifunua mwenyewe kwa Yohana kwa njia ya kipekee sana.**

**Angalia katika Ufunuo wa Yohana** sura ya 1 mstari wa 1. Mstari huo unasema: “Ufunuo wa Yesu Kristo.” Ninaamini kwamba Mungu alitupa sura hii ya Yesu kwa sababu hatuwezi kumuona kama alivyo kwa njia nyingine. Wengi walitembea pamoja naye, wengi walimuona akifa, na baadhi walimuona alipofufuka, lakini hakuna mtu aliyemuona kama alivyo sasa. Ni shujaa, hakimu, Mwanakondoo, Mungu mwenye nguvu, yuko kwenye kiti cha enzi, hakuna kiumbe kinachoweza kushindana naye, Yeye ni mshindi, “sura ya kuogofya” kwa maadui zake, anatenda kazi kwa niaba yako. Yohana alihitaji kujua yote haya.

**Ninaamini Yesu alimuonyesha Yohana ufunuo huu ili kumfariji** kwa kumletea imani na tumaini, na kuyafanya yale mazingira yasiyofaa yawe na maana, na kufanya vivyo hivyo kwa ajili ya yale makanisa aliyoayaandikia waraka huu miaka zaidi ya 2000 iliyopita na pia kufanya vivyo hivyo kwa kwa ajili yako na mimi katika maisha yetu nyakati hizi tunapoona mambo yasiyofaa yakifanyika katikati yetu. Ni kitabu kinachotupatia ushindi katika maisha yetu.

**Hali ya Yohana:** Kwa Yohana, ulimwengu ulikuwa umeharibika. Hebu jaribu kuwaza, Yohana alikuwa akiishi na Yesu kwa miaka ipatayo mitatu, alimuona akitenda miujiza mikubwa, alimuona alipokuwa akisulibiwa, alimuona alipofufuka. Kwa hakika baada ya ufufuo alifikiri sasa kwamba kulikuwa na ushindi. Alimuona Roho Mtakatifu akishuka juu ya wanadamu na kanisa likaanza. Alianzisha makanisa, aliona watu wakiokoka. Ghafla, wale mitume wote wa kwanza wakatoweka na baadhi walisulibiwa, Petro alisulibiwa kichwa chini miguu juu, baadhi waikatwa vichwa, wengine wakauawa kwa njia nyingine. Aliuona ulimwengu ukienda kombo.

**Yohana mwenyewe ilikuwa nusura auwe kwa kuchemshwa** katika mafuta, lakini hawakuweza kumuua. Sasa kwa wakati huu alichukuliwa kama mfungwa na kutupwa katika kisiwa cha Patmo (maana yake = kuuawa kwangu – kisiwa chenyе mawemawe kisichokuwa na watu katika bahari ya Aegea). Kazi yake ya kila siku ilikuwa kuvunja miamba na kukokota mawe makubwa huku na huko katika vilima. Lazima alifikiri na kujiliza, “Je, ulimwengu umekwenda kombo? Ni kweli kwamba nilimjua Yesu? Ni kweli Yesu alikuwa Mungu katika mwili kama nilivyoandika katika kitabu changu cha Injili? Je, kanisa ni kitu kilichoangamia? Maisha yangu yamepotea bure?” Kisha kwa ghafla, kitu fulani kikatokea kwake ambacho hajawahi kukiona kabla.

**“Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana;** nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu, ikitisema, Haya uyaonayo

uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia. Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu; na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini. Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto; na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi. Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenyewe makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama juu liking'aa kwa nguvu zake. Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akasema, usiogope mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.” (Ufunuo wa Yohana 1:10-18).

### Yesu amefunuliwa

**Katika Ufunuo wa Yohana sura ya 1** Yohana sasa anatambua Yesu ni nani! Ni tofauti na yule aliyemuona mara ile ya mwisho. Ni Kristo aliyepaa amefunuliwa! Amefunuliwa kama Mwaminifu, Shahidi wa kuaminika. Mzaliwa wa kwanza katika wafu, Mfalme wa wafalme wa dunia hii, Yeye ajaye upesi, wa Kwanza na wa Mwisho, Mwenye nguvu na uwezo wote!

Amefunuliwa kama yeye ajaye kumelikumu kanisa lake huku akiwa na mwali wa moto katika macho yake, upanga mkali ukitoka kinywani mwake na miguu kama shaba iliyosuguliwa sana. Hukumu hii siyo ya kulilaani kanisa, bali kuliepusha na ghadhabu ijayo. Utakatifu ndio utakaoliepusha kanisa na ghadhabu hiyo!

**Katika Ufunuo wa Yohana sura ya 2-3** Yesu anasema na Kanisa, wakati ule na sasa kana kwamba ni Jenerali aliyekuwa akisema na majeshi yake na kuyaweka tayari kwa vita. Kwa kuwa mapambano makubwa yalikuwa karibu kutokea na makanisa saba kuharibiwa kama hayakuandaliwa, Yesu alilihubiri kila kanisa kulingana na upungufu wake. Aliyahimiza kuwa safi mbele za Mungu. Utakatifu ndio utakaoliepusha kanisa!

**Katika Ufunuo wa Yohana sura ya 4,** Yesu anamualika Yohana, na wewe na mimi tuyaoone mambo yatakayotukia. Tunahitaji kuyaona mambo katika maisha kama jinsi Mungu mwenyewe anavyoyaona.

Tunaweza kuchukuliwa na mambo ya dunia na macho yetu yakapofushwa kiasi cha kushindwa kuona kama Mungu anavyoona. Tumeketishwa pamoja na Kristo, kwahiyio Roho Mtakatifu anaweza kutupatia macho hayo. Tukiyaangalia yale yanayotuzunguka kama jinsi Mungu anavyoyaona hayawezhi kuonekana mabaya.

**Katika Ufunuo wa Yohana sura ya 5**, Mungu ndiye anayeanzisha vita. Shetani haanzishi vita katika maisha yetu. Angalia, hakuna mtu aliystahili kukitwaa kile kitabu na kuzifungua muhuri zake isipokuwa Yesu, kama Simba wa kabile la Yuda na Mwana Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi zetu. Tusingeweza kustahimili kusimama katika shida na mambo magumu ya maisha haya kama Yesu asingezichukua dhambi zetu!

Yesu ndiye anayeanzisha vita. Tunahitaji kukumbuka jambo hili matatizo yanapotupata. Linaweza kuwa shambulio baya, lakini ni Yesu anayekuwa ameweka ndoana katika pua za maadui zetu ili waje tupate kuwaharibu katika Jina lake. Libarikiwe Jina la Bwana milele!!! Haleluya!

**Katika Ufunuo wa Yohana sura ya 5-16**, kuna vita kuu, mapambano, hukumu na mateso wakati kitabu kilipofunguliwa. Mambo yanayotokea ni ya kutisha, yanazidi kuwa mabaya, hayavumiliki. Hata hivyo katika yote hayo Mungu anatafuta watu watakaoshinda na kusimama imara.

**Ufunuo wa Yohana 7:3** inaonyesha kwamba wanale waaminio walio waaminifu ~~kalika~~ hatua hizi za kushinda watapigwa muhuri na Mungu na kutunzwa salama. Mambo yatazidi kuwa mabaya.

**Kauli iliyoko kwenye mabano tmetolewa katika Ufunuo wa Yohana 11** ikionyesha ushindi wa Msalaba na kuonyesha pia kwamba ulimwengu utatawaliwa na ufalme wa Mungu na Bwana Yesu Kristo.

**Ufunuo wa Yohana 12:11** inatuonyesha kwamba kama tukisimama imara wkatii huu wa matatizo makubwa tutamshinda adui kwa damu ya Mwana Kondoo na kwa Neno la Mungu linaloshuhudiwa kwa vinywa vyetu. Lakini hii itawezekana iwapo tutampenda Mungu na makusudi yake kuliko jinsi tunavyoyapenda maisha yetu.

**Ufunuo wa Yohana 17** ni ufunuo wa mfumo wa “ulimwengu” na uhariibifu wake. Inaonyesha ushirikiano uliopo baina ya mambo ya kiroho na yale ya kisiaa.

**Ufunuo wa Yohana 18** ni onyo jingine kwa watu wa Mungu kutoka katika mfumo wa “ulimwengu” kwa sababu karibu utaharibiwa na kwamba mfumo hauaminiki. Imeelezwa jinsi mfumo huo utakavyoharibiwa.

**Katika Ufunuo wa Yohana 19** kuna ushindi, na Bwana anarudi akiwa amepanda Farasi mweupe kutimiza ahadi yake na kuleta thawabu yake. "Kisha nikaziona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda, aitwaye Mwaminifu na Wa-kweli, naye kwa haki ahukumu na kufanya vita. Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolija mtu ila yeye mwenyewe. Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa, Neno la Mungu. Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi. Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, **MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA.** (Ufunuo wa Yohana 19:11-16).

**Katika Ufunuo wa Yohana 20** Shetani anafungwa; na hukumu inafanyika.

**Ufunuo wa Yohana 21** inaonyesha jinsi ufalme wa Mungu unavyoonekana wazi, na Yerusalemu Mpya. Inaonyesha ushirika wa karibu kabisa na Yesu kutokana na yote tuliyoyapitia.

**Ufunuo 22** inaonyesha huduma kwa wale wliosimama na kushinda hadi mwisho. Hapa kuna picha ya mto utiririkao, unaotajwa katika Ezekiel 47, ~~hukiuwa na matunda pande zote kwa ajili ya kuwaponya mataifa au watu wasiongwa~~ Mungu. Katika usoefu wangu, huduma ya kweli huja baada ya mateso mengi na kushinda. Tunayo mamlaka juu ya pepo katika vita.

**Ufunuo 22 ina yo pia maneno ya kutia moyo.** "Tazama naja upesi, shika sana utabarikiwa. Shika sana ~~utayageuza~~ mateso na matatizo yote haya katika maisha yako kuwa baraka."

**Ufunuo huu au kutukuzwa kwa Yesu Kristo** kunafanana sana na yale aliyosema Yesu kwa wale watu wawili waliokuwa njiani kwenda Emau, na baadaye kwa wanafunzi 11, kutoka Musa, Zaburi na Manabii katika Luka 24. Hata hivyo, huu ulikuwa ufunuo kamili. Tunapoona Yesu akitukuzwa kwa jinsi hii tunakuwa mionganoni mwa wale wanaostahili kujazwa Roho Mtakatifu (Yohana 7:39).

**Siwezi kudai kwamba ninajua kitabu chote cha Ufunuo wa Yohana,** wala siwezi kudai kwamba nimefundisha kwa ukamilifu kitabu hicho hapa. Na wala sisemi kwamba hakibusiani na unabii wa mambo au matukio yatakayoupata ulimwengu. Ninachosema ni kwamba ni ZAIDI ya hayo. Ni kitabu kinachotufaa sana katika maisha

yetu leo. Tunahitaji kujua Yesu ni nani SASA! Pia ninajua kwamba tarehe 26 Agosti 1979, nilipokuwa nikisoma kitabu cha Ufunuo wa Yohana, kwa njia ya muujiza, Yesu aliniokoa na kunijaza Roho Mtakatifu. Alijidhihirisha mwenyewe kwangu na tokea wakati ule nimebadilika!

**Baadaye Yohana alifahamu** kwamba kuna kitu cha ziada katika maisha, kuliko kufikiria tu kwenda mbinguni na kuishi maisha mazuri hapa duniani. Tumeitwa kuingia katika vita, na Yesu yu hai amejaa nguvu, kuhakikisha tunapata ushindi! Hii ni picha tunayopaswa kuionna wakati mambo yanapokuwa hayaendi vizuri. Tunahitaji kujiweka mahali fulani katika hatua hizi na kujua kwamba hili limeagizwa na Mungu. Hatimaye tutashinda!

**Mpaka hapa umepata picha ya kwanza ya Mungu.** Hakuumbwa. Amekuwepo siku zote. Kamwe hajawahi kutokuwepo. Na wala hatakoma kuwepo. Ana uwezo wote, anajua yote kwa sababu anaishi milele nje ya mipaka ya muda. Anajua mambo yajayo kwa sababu kwake yanakuwa tayari yametokea. Anajua yote. Anaweza kujua unawaza nini. Anajua utawaza nini hata kabla hujaanza kuwaza. Yupo kila mahali kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**Ni Mungu Baba, Yesu Mwana wa Mungu** anayeitwa pia Neno la Mungu, na Mungu Roho Mtakatifu.

**Ni mtawala juu ya yote.** Ni mshindi juu ya maadui wote. Mambo yote yako mikononi mwake!

**Unaweza kurawamini na kuliamini Neno lake bila kujali chochole!** Mungu ni wa kushangaza! Hatuwezi kuanza kuelewa jinsi alivyo mkuu sana! Anatupenda kuliko jinsi tunavyofikiri!

## Sura ya 5 – Kuketi

Kuketi kunahusiana na sura yetu na jinsi tulivyo katika Kristo. Ibilisi anaweza kutuua, kutuiba na kutuharibu kama mwenendo na maisha yetu hayampendezi Bwana. Hata hivyo mwenendo wetu husababishwa na jinsi tunavyojiona wenyewe, au sura yetu wenyewe. Tunaweza kujaribu sana kubadilisha mwenendo wetu, lakini ukweli ni kwamba mwenendo husababishwa na sura yetu. Kitu pekee tunachoweza kubadilisha ni jinsi tunavyoionna sura yetu. Ili tuwe na sura au picha iliyo sahihi (sahihi mbele za macho ya Bwana) ni lazima tufanywe upya nia zetu kwa Neno la Mungu. “Wala msiiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” (Warumi 12:2).

1. Tunahitaji **KUMPINGA** Ibilisi – (vita) – (Yohana 10:10).
2. Lakini hatuwezi **KUMPINGA** mpaka tujifunze kwanza jinsi ya **KUENENDA** – (mwenendo wetu au jinsi tunavyoishi) – (Waefeso 4:27).
3. Hata hivyo, hatuwezi **KUENENDA** mpaka tujifunze kwanza **KUKETI** – (sura yetu wenyewe) – (Luka 6:45).

**Tunaishi katika vita vya kiroho** na kwa sababu hiyo tunahitaji **KUMPINGA**, lakini hatuwezi kumpinga kama hatuishi maisha safi, na hatuwezi kuishi maisha safi iwapo tuna sura isiyo sahihi.

**Tunahitaji kujúa jinsi tulivyo (KUKETI) kabla ya kuishi itupasavyo (KUENENDA)**, na kabla ya (KUMPINGA) Ibilisi katika maisha yetu. Mambo hayo yanatokana na mistari mitatu katika Waefeso:

**KUKETI – Katika Waefeso 2:5-6** tunasoma kwamba “hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhiisha pamoja na Kristo; yaani, mmeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, **akatuketisha** pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu.”

Je, kulingana na mstari huo, TUMEKETI pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho, au tutaketi pamoja naye baada ya kufa na kwenda mbinguni?

**KUENENDA – Katika Waefeso 4:1** tunasoma maneno yafuatayo “Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, **mwenende** kama invyoustahili wito wenu mlioitiwa.”

**KUPINGA – Katika Waefeso 6:11** tunaambiwa hivi: “Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.”

### **Kwa hiyo hebu tujifunze kwanza kuketi**

Tunaenenda sawasawa na jinsi mioyo yetu inavyotuambia. “Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake.” (Luka 6:45).



Kuketi pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho hutegemea msalaba wake. Angalia tena Waefeso 2:5: Mstari huo unasema kwamba tulikuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu. Je, mfu anaweza kufanya jambo lolote? Hapana. Mfu hana haja ya kujifunza kuenenda au kupinga, au kuziacha tabia mbaya, mfu anahitaji UZIMA! Mfu hawezi kujipa uzima, wala hawezi kujaribu. Mungu kwa njia ya Kristo ndiye aliyetupa uzima.

### **Hebu kwanza tufafanue neno hili kuketi kwa kulihusisha na ulimwengu wa kiroho**

Miguu yetu inauhikilia tunaposimama, lakini tunapoketi tunapumzisha uzito wetu yetu ya kiti. Ni suala la kutumia nguvu au kupumzika. Ama tunachoka au tunapumzika. Tunapumzisha uzito wetu wote kwa Yesu, nafsi zetu wenyewe na maisha yetu vajayo.

Katika uumbaji, Mungu alifanya kila kitu kila hajatuumba. Adamu alianza maisha yake na Sabato. Mwanadamu alipaswa kufanya nini katika uumbaji katika siku 6 za kwanza? Mungu alipata msaada gani kutoka kwa Adamu katika kuumba mbingu na nchi? Siku ya kwanza ya Adamu ilikuwaje? Ilikuwa siku ya kupumzika. Soma Mwanzo sura ya 1. Mungu aliumba kila kitu kwa siku 5, kisha akamuumba mwanadamu siku ya 6. Mwanadamu hakumsaidia Mungu. Siku ya kwanza ambayo mwanadamu aliamka au kutoka usingizini ilikuwa siku ya 7, na siku hiyo ilikuwa siku ya mapumziko. Ni pale tu Adamu alipopewa kila kitu ndipo alipokwenda kufanya kazi.

### **Mungu alifanya kazi, kisha akapumzika Mwanadamu hupumzika, kisha hufanya kazi**

**Hii ni Injili! Mungu alimaliza kazi ya ukombozi.** Alitununua kutoka katika utumwa wa dhambi na Shetani, akatupa utu mpya, uzazi mpya uliopandikiza maisha na tabia ya Mungu ndani yetu. Tusingeweza kufanya lolote ili kuyapata hayo. Tunachoweza tu kufanya ni kuingia kwa imani tunaposikia juu ya sadaka au kitu kitolewacho.

**Unaweza kujisikia tofauti au la**, lakini hisia zako siyo za kuaminika. Unahitaji kujizoeza kuliamini Neno la Mungu na kuweka pembeni hisia zako. Baadhi ya matukio mazuri na ya ajabu yametokea katika maisha ya Mkristo. Adui, Shetani atatumia moyo wako uliokuwa ukitawaliwa na ufahamu wa kale kuficha kweli hizo mbali na wewe. Ni mambo ya kweli, yanayoweza kuaminika. Tutakapoanza kuona Neno la Mungu lina mamlaka ya mwisho, tutaanza kuona ukweli. Mamlaka ya mwisho siyo mazingira, siyo hisia zako, ni Neno la Mungu. Soma Neno la Mungu uone wewe ni nani!

**Suala la wewe ni nani lina upande mmoja wa kisheria na mwingine wa kiuzoefu.** Wakati ulipompokea Yesu kuwa Bwana, na pia wakati Neno la Mungu lilipopandwa na Mungu katika moyo wako, ulikuwa na kufufuka pamoja na Yesu. Ulizaliwa upya. Biblia inasema katika 1 Petro 1:23 kwamba “Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa mbegu ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.”

**Kisheria, tumesulibiwa pamoja na Kristo kama maandiko yanenavyo** katika Wagalatia 2:20 na Warumi 6:6. Katika Wagalatia 2:20 tunasoma maneno yaafuatayo: “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimifena bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.”

**Hata hivyo huenda bado hatujapata uzefu wa ukweli huo.** Hapa ndipo Wakristo wengi wapya au watu waliookoka hivi karibuni wanapokosea njia. Eti kwa kuwa hawaoni ukweli wa Neno, au jambo baya zaidi, kile wanachokiona ni kinyume cha yale yanayolezwa na Neno, basi wanakata tamaa na kuiacha imani. Katika dunia, kuona ni kuamini, lakini kwa Mungu, ni lazima kwanza uamini kabla ya kuona.

**Tunahitaji kujuu kwamba sisi siyo watu wawili.** Hatuna nafsi mbili! Baadhi ya Wakristo wanakiri hivyo kwa sababu ya kukosa kuona ushindi juu ya dhambi. Baadhi hudai kwamba maneno ya Paulo katika Warumi 7 yanaonyesha kuwa tuna asili mbili ndani yetu. Warumi 7 haisemi hivyo. Inachosema ni kwamba “kanuni ya dhambi” inatenda kazi ndani yetu. Kama tumesulibishwa na Kristo na kuzaliwa mara ya

pili, basi utu wetu wa kale umekufa, na mtu mpya amezaliwa ndani yetu.

Tunahitaji kugeuzwa nia zetu. Tunapozaliwa mara ya pili, roho zetu hufanywa upya. Tutakapokwenda mbinguni miili yetu itageuzwa (itabadiishwa), lakini nia zetu hugeuzwa kila siku tunapoishi kwa kufuata Neno la Mungu. Nia zetu zina “kanda” za zamani zinazosababisha tuenende katika utu wa kale. Ni kama mti ambao umekatwa lakini majani yake bado hayajanyauka. Andiko linalokubaliana na kauli hii ni Warumi 12:1-2. Mistari hiyo inasema hivi, “Basi , ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenze maana. Wala msifiuatishenamna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpare kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.”

### Hii ilitokeaje?

#### **Yesu alifanyika dhambi zako na wewe ukawa haki yake**

Katika 2 Wakorintho 5:21 imeandikwa hivi: “Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeze.”

**Agano la damu limetumika katika maisha yako.** Badiliko kubwa limefanyika kati yako na Yesu Kristo. Pale msalabani, Yesu alichukua kila kitu kibaya katika maisha yako. Na wakati alipofufuka alikupa kila kitu kizuri kwa nguvu za Mwenyezi Mungu! Alikuzaa kama mtoto wa kiume au wa kike na kukuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho JUU kabisa ya maadui zako wote. Shetani, adui yako, kwa nguvu zake, atatumia kila njia kukuibilia jambo hili kwa udanganyifu. Hata hivyo, ukiijua kweli, na kusimama katika kweli, utakuwa mshindi. Ulipitia mateso na kifo cha Yesu, na sasa tayari umekwishafufuka pamoja naye.

**Ni lazima tuangalie jinsi Yesu alivyokuja katika sehemu hii ya kuketi.** Alisulibishwa, akafa, akazikwa na kufufuka. Siku ya kufufuka kwake alikuwa mzaliwa wa kwanza wa viumbe vipyta. Baada ya kuonekana kwa muda mrefu na wanafunzi wake na watu wengine wapatao 500, alirudi kwenye mkono wa kuume wa Baba, na kuketishwa kama Mfalme na mtawala wa dunia.

**Sasa kama tumeketi pamoja naye katika ulimwengu wa roho,** ni wazi kwamba tulipitia hatua zote pamoja naye, yaani kifo, kuzikwa, kufufuka na kuwa viumbe vipyta, na kupaa. Ni kama kuweka alama katika kitabu na kukihamisha kitabu hicho huku na kule. Alama hiyo

huenda pamoja na kitabu. Huenda unajiuliza, “inawezekanaje kwamba nilipata uzoefu wa hatua hizi pamoja na Kristo, wakati ambapo hata kuzaliwa nilikuwa bado?”

**Jibu la swali hilo limo katika ukweli huu kwamba Mungu huishi milele**, yaani bila muda. Kwa hiyo tunapopata uzoefu wa kuzaliwa mara ya pili, tunachukua historia nzima ya Yesu, bila kujali

tofauti ya muda. Baadhi ya maandiko yanayolezea jambo hili ni haya yafuatayo:

“basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?” (Waebrania 9:14).

“neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele.” (2 Timotheo 1:9b).

**Baadhi ya mambo ambayo Mungu anataka uyajue.**  
**Roho Mtakatifu kwa njia ya Neno anaweza kufanya jinsi ulivyo**  
**katika Kristo kuwa kitu halisi. Unahitaji kulichukua Neno kama**  
**jinsi lilivyo na kuliamini kama waraka halali.**

**Tulikuwa tumeopotea pasipo tumaini:** Katika Waefeso 2:12 imeandikwa hivi: “kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmeferakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani.”

**Tulikuwa tumeokuwa kwa sababu ya makosa yetu. Akatuhuisha pamoja na Kristo.** Katika Waefeso 2:5 imeandikwa, “hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo...” Huo ndio msimamo wetu halali tulio nao pamoja na Mungu leo, na pia ndio msingi wa haki zetu.

**Neno la Mungu katika Waefeso 2:6 linanena kwamba tunaketi kihalali pamoja naye katika ulimwengu wa roho.** “Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu”

**Katika 2 Petro 1:4 tunaambiwa kwamba tunakuwa washirika wa tabia ya Uungu** na pia tumeokolewa na uharibifu ulioingia duniani kwa sababu ya kosa la Adamu. Uharibifu huo ni kifo cha kiroho. Na kuokolewa ni Uzima wa Milele.

**Uhalisi wa kuwa Kiumbe Kipyä.** Tumekuwa jamii mpya ya watu. Biblia inasema katika 2 Wakorintho 5:17 "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyä; ya kale yamepita; tazama, yamekuwa mapya." Katika tafsiri nyingine, mstari huo unasema

kwamba tumekuwa spishi mpya. Huu ni ukweli sio dini! Kama mtu angeweza kuchukua Eksirei ya kiroho na kuangalia ndani ya moyo, angeona tofauti kati ya mtu aliyeokoka na mtu ambaye hajaokoka.

**Katika Yohana 10:10b** imeandikwa hivi: "mimi nalikuja ili wawe na **uzima**, kisha wawe nao tele."

**Neno hili "uzima" linatokana na neno la Kiyunani "Zoe".** Zoe linamaanisha tabia ya Uungu ya Mungu. Mungu aliweka tabia yake ndani yetu. Sisi si wenye dhambi tena, tumefanywa upya kabisa. Wakati fulani tunaweza kujikuta tumetenda dhambi. Hata hivyo tunabaki tu kuwa watoto wa Mungu waliotenda vibaya, sio wenyе dhambi. Shetani anajua hilo, ndio sababu anajaribu kuuficha ukweli huo usiuje.

**Tuna msamaha wa dhambi zetu.** Neno la Mungu katika Wakolosai 1:14 linasema: "ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, **msamaha** wa dhambi" Vile vile katika Waefeso 1:7 tunasoma maneno yafuatayo: "Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, **masamaha** ya dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake." Neno, "msamaha", lina maana hasa ya kutenganisha au kuondoa. Dhambi zetu zimechukuliwa na kuwekwa mbali nasi.

**Msamaha maana yake kufuta kila kitu** ambacho tumewahi kufanya hadi siku ile tulipokwenda kwa Kristo. Haijalishi ni kwa kiasi gani Shetani alitufunga katika mitego yake. Dakika ile ile tunayokuwa tumezaliwa mara ya pili tunasimama mbele za Mungu kama viumbe vipya bila hanifu ya maisha yetu ya zamani katika roho zetu. Mara tu tunapozaliwa mara ya pili tunafanyika Haki ya Mungu katika Kristo (2 Wakorintho 5:21).

**Muda ule tulipozaliwa mara ya pili tulifanyika Haki ya Mungu - si kwa matendo yetu bali kwa kile alichopanda Mungu ndani yetu.** Biblia inasema katika Warumi 3:21 kwamba<sup>10</sup> Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii." Na pia katika Warumi 4:3-9 tunapata maneno yafuatayo: "Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki. Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni. Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki. Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo, heri waliosamehewa makosa yao, na waliositiriwa dhambi zao. Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi. Basi je! uheri huo ni kwa hao waliotahiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa? Kwa

kuwa twanena ya kwamba kwake Ibrahimu imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki.”

**Yesu alimshinda Shetani.** Tunasoma hivyo katika Waebrania 2:14 “Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, **Ibilisi**.”

**Tunayo njia ya kumfikia Mungu wakati wowote tunapohitaji kufanya hivyo kwa damu ya Yesu.** Neno la Mungu katika Waebrania 10:19-20 linasema: “Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia ilio mpya, ilio hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake.” Imeandikwa pia katika Waebrania 9:12 kwamba “wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe alingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.”

**Yale aliyoyasema Mungu kuhusu ukombozi wetu** hayamaanishi kitu kwa watu wengi katika kanisa. Na kwa waalimu yanaonekana tu kuwa ni ukweli wa kiteolojia lakini hauna umuhimu. Biblia inasema katika Waefeso 1:7 kwamba “Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.”

**Utawala wa Shetani juu yetu umeunjwa.** Shetani alikuwa na mamlaka juu ya utu wetu wa kale, lakini sasa utu wetu mpesa ni Roho ya Kristo mwenyewe ambayo tayari imemshinda Shetani. Katika Warumi 6:8-10 tunasoma ~~hivyo~~: “Lakini ikiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. Maana kwa kule kufa kwake, alifia dhambi mara moja tu, lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu.”

**Kama hii ni kweli, kwa nini maisha bado yanashindha? Kwa nini sijisikii kama vile Maandiko haya yanavyonena?**

**Nafurahi sana kwamba umeuliza.** Hayo ni maswali muhimu. Rafiki yangu ilikuchukua miaka kupata ufahamu wa dhambi na laana, vivyo hivyo itachukua muda fulani mpaka moyo au nia yako ifanywe upya kwa Neno la Mungu. Kwa mtazamo wa Shetani anajaribu kuiba mbegu ya Neno katika moyo wako. Akikuwekea shinikizo kubwa kwa kutumia mazingira na hatia, utaacha kuamini. Kwa mtazamo wa Mungu, anakujaribu (anakupima). Anataka kukuza tabia ndani yako. Sio aina ile ya majaribio yanayotolewa na walimu na kwa majaribio hayo kuna kufaulu au kufeli. Kujaribu kunakozungumzwa hapa ni kama

kile kitendo kinachofanyika wakati wa kusafisha dhahabu. Neno kujaribu linamaanisha kuweka motoni na kuunguza uchafu wote. Mungu anafurahia kuona uaminifu wako katika shida au dhiki. Anataka kujua kama utaliyamini Neno lake hata kama mambo yanaonekana kinyume.

**Tunahitaji kugeuzwa nia zetu.** “Basi , ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali **mgeuzwe kwa kufanya upya nia zenu**, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” (Warumi 12:1-2).

**Hii hapa ni ahadi ya Mungu kwako.** Neno la Mungu katika Waembrania 8:10 linasema, “Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli. Baada ya siku zile, asema Bwana; nitawapa sheria zangu katika nia zao, katika mioyo yao nitaziandika; nami nitakuwa Mungu kwao, nao watakuwa watu wangu.

**Soma 1 Petro 1:6-7. Mistari hiyo inasema nini kuhusu kujaribiwa?**

**Uthibitisho unaoonyesha kwamba unaamini au la SIYO jinsi unavyojisikia.** Uthibitisho ni yale yatakayotoka kinywani mwako kutoka katika hazina ya moyo wako. Katika Luka 6:45 Neno la Mungu linasema: “Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema ~~na mtu mwovu~~ katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, **kinywa chake hunena** yale yaujazayo moyo wake.”

**Njia pekee ya kushinda na kuponywa** kutoka katika vitu kama dhambi, hofu, hatia, ulevi, kujisikia hufu; kujisikia kushindwa nk, ni kukubali ukweli huu. Tunapojuwa kwa hakika, kwamba Mungu anatupenda, kwamba sisi ni mali yake, kwamba ametufanya viumbe vipya na ya kale yamepita, na tukijua kwamba tunafanana na Kristo, kwamba tumenunuliwa kutoka utumwani na kupewa uwezo wa kuchagua kukubali utawala kamili, mamlaka na uangalizi wa Mungu, hapo ndipo tunapoanza hatua za kushinda mabaya yote katika maisha yetu.



**Kitu rahisi kabisa kukumbuka ni msalaba.** Msalaba wa Yesu ulichukua kila kitu kibaya katika maisha yetu, na yale yanayokuja katika maisha yetu huyabadilisha kuwa baraka.

**Habari zote hizi njema na za ajabu kuhusu jinsi tulivyo hazipaswi kutupa kiburi.** "Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi" (Yohana 15:5) Tusipotegemea kwa ukamilifu maisha ya Mungu yaliyomo ndani yetu hatuwezi kitu. Hatukuitwa kuwa watu wanaotegemea nguvu zao. Tumeitwa kuwa watu wanaotegemea mia kwa mia maisha yaliyoingizwa ndani yetu. Tawi haliwezi kufanya lolote, litakufa, lisipoungana na mzabibu. Tunahitaji kuvaajohoh la unyenyekevu na kujua kwamba bila yeze sisi si kitu! Ukichunguza Neno la Mungu katika Yohana sura ya 15, utaona kwamba kutegemea ni jambo linalohusiana siku zote na Neno la Mungu.

### **Usiwe kifaranga wewe ni tai!**

**Siku moja yai la tai lilitoka kwenye kiota chake** likaangukia kwenye kizimba cha vifaranga. Tai akatotolewa pamoja na vifaranga na kuishi kama kifaranga, lakini akaanza kujiona tofauti kadiri alivyoendelea kukua. Hakuna aliyejukwepo pale wa kumwambia kwamba hakuwa kifaranga bali tai.

Dhoruba ilipokuja, tai alikimbilia haraka ndani ya kibanda cha kuku pamoja na vifaranga wengine, ili kujificha. Lakini tai kila wakati alikuwa akiangalia juu na kuwaona ndege wengine juu ya majabali. Hawakuwa na hofu, tena walikuwa hawakimbii. Walikuwa wamesimama huku mabawa yao yamechomekwa kwenye soketi maalum (zinazowafanya wawe kama bawa lililouniganishwa kwenye kiunzi cha eropleni). Waliikazia macho dhoruba hata ilipokuwa bado mbali inakuja. Waliingojea na kuingojea na kisha iliwigongwa! Dhoruba iliwapiga lakini badala ya kuwaumiza iliwfanya waruke. Walipaa angani kiasi cha futi 30,000 juu kabisa ya dhoruba kwenye hewa tulivu. Yule tai alijisemea moyoni, "jamani, ona ndege wale, natamani ningekuwa kama wao."

Siku moja alitazama JUU, akamuona tai anaruka na kupaa juu pamoja na dhoruba. Ghafla akatambua, "Mimi siyo kuku, mimi ni tai. Kwa nini nikimbie?" Akapanda mlima, akakunjua mabawa yake, kisha akaruka na kupaa!

**Rafiki yangu, wewe siyo mwanadamu tu,** wewe siyo kifaranga. Umeumbwa kupaa katika ulmwengu wa roho pamoja na Kristo. Tazama juu!

Sasa kumbuka mfano wa mpanzi katika Marko sura ya 4 (soma mfano huo). Shetani huja kuiba mbegu ya Neno la Mungu iliyopandwa ndani ya moyo wako. Leo mbegu ya wewe ni nani katika Kristo imepandwa ndani yako. Kesho, mambo ya kuvunja moyo yakija kwa njia yoyote ile, simama imara. Neno ni la kweli! Mambo huja na kutoweka.

Dondoo kutoka katika kitabu cha maombi cha ndugu Richard Wurmbrand kii twacho, "Reaching Towards the Heights" - Mei 15

"**Katika jaribio tulamini gunduwa kwamba wadudu ambao** kwa kawaida huishi gizani huweza kushurutishwa kuyaacha makazi hayo na kupendelea nuru. Kila wanapokimbilia gizani, hushtuliwa kwa umeme, na wakija kwenye nuru upata chakula kingi. Baada ya muda, viumbe hawa, kwa maneno ya kibiblia, "huva mdudu mpya." Kinyume na tabia ya wadudu wenzao, tokea wakati huo na kuendelea, walipendelea nuru kuliko giza. Kisha wadudu hawa walikatwa vipande vidogo vidogo na kuongezwa kwenye chakula walichopewa wadudu wenzao. Ajabu ilioje, wadudu hao nao walibadili tabia zao. Wadudu wale (baada ya kupewa nyongeza ile ya nyama ya aina mpya ya wadudu) walipata ongezeko la aina fulani ya asidi katika miili yao na hivyo kuongeza uwezo wa kukumbuka. Waliweza kuepuka giza na kupendelea mwanga kama wale viumbe waliowala walivyokuwa wakifanya. Majaribio kama hayo yamefanywa pia kwa wanyama wengine.

Ukitaka kuwa mtu mpya, mtu wa haki, mtakatifu, mle Yesu. Alifanyika mwili ili kwamba aweze kuwa chakula chako cha kila siku."

**Katika Zaburi ya 22:6 imeandikwa "Mimi ni mdudu" (Yesu alisema msalabani).**

Neno hilo mdudu katika Kamusi ya "Strong", limefafanuliwa kuwa ni rangi nyekundu iliyotengenezwa kuto kana na mwili uliokauka wa mdudu wa kike aitwaye "coccus ilicis".

Wakati mdudu huyo wa kike mwenye rangi nyekundu alipokuwa tayari kuzaa, aliuambatisha mwili wake kwenye shina la mti na kujikongomea kwa uthabiti kabisa, katika hali ya kudumu bila kuondoka. Mayai yaliyopo chini ya mwili wake yalilindwa hadi lava walipoanguliwa na kuweza kuingia katika hatua zao anuwai za maisha kamili ya kiumbe. Mdudu huyo mama alipokufa, mwili wake pamoja na eneo alilokuwepo mdudu yule, lilitiwa rangi na aina fulani ya uevu mwekundu. Rangi nyekundu zilizokuwa zikitumika zamani kibashara zilitokana na miili iliyokufa ya wadudu hao wa kike wekundu.

Ufafanuzi huo unatupa picha ya ajabu ya Kristo, aliyekufa mtini, akamwaga damu yake ya thamani ili "alete wana wengi waufikilie utukufu" (Waebrania 2:10)! Alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi katika yeche!

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Sura ya 6 – Kuenenda

**Hatuwezi kusimama bila kwenda. Adui yetu  
"atakula chakula chetu".**

"**Shetani** asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake." (2 Wakorintho 2:11).

"Wala msimpe **Ibilisi** nafasi" (Waefeso 4:27).

"Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa **Ibilisi**" (1 Timotheo 3:7).

"wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa **Ibilisi**, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake" (2 Timotheo 2:26).

"Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu **Ibilisi**, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze" (1 Petro 5:8).

**Maandiko hayo na mengi mengine yanaonyesha wazi** kwamba ingawa tumeokoka, kuna uwezekano wa kutegwa na Ibilisi na wasaidizi wake, kwa njia nyingi mbalimbali. Maandiko hayo yanaonyesha pia kwamba tabia na kuenenda kwetu vinaweza kumfanya Ibilisi apate nafasi ya kutudhuru.

**Ushindi wetu dhidi ya Shetani na mambo mengine** unaweza tu kupatikana kutohaka na "kuenenda" kwetu. Ili kuwa salama, tunahitaji kuwa na tabia ya Yesu katika maisha yetu. Tukijaribu kuishi kwa kufuata mwenendo wetu wa zamani tutashindwa vita. Lakini kama tunaenenda katika tabia ya Mungu, adui atakuwa anamuona Yesu tu na siyo sisi. Kumbuka, adui hana nafasi katika Yesu. Yesu alimshinda Shetani.

Neno la Mungu katika Waefeso 4:1 linasema "Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, **mwenende** kama inavyoustahili wito wenu mlolioitiwa."

**Katika somo la "Kuketi"** (somo kuhusu "kula mdudu") **tulijitahidi kusema wazi** kwamba sura yetu ndiyo inayobainisha tabia yetu, na kwamba maisha ya Kikristo hayaanzi na "kuenenda". Au kwa maneno mengine utendaji wetu, au kitu chochote tunachoweza kufanya au kukamilisha.

**Kila kitu msingi wake ni kazi ya Yesu iliyomalizika msalabani** Golgotha na yale aliyoyakamilisha pale na jinsi tulivyopata kuwa kutohaka na msalaba wake. Bwana amefanya kila kitu kwa ajili yetu. Amekaa kwenye kiti cha enzi, na sisi tumeketishwa pamoja naye.

Tulisulibishwa, tukafa, tukazikwa,tukafufuliwa pamoja naye na kisha tukaketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho. Tunasoma katika Waefeso 2:6 kwamba "Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu."

**Hata hivyo maisha ya Kikristo hayaishii pale.** Mwenendo wetu wa Kikristo ni uhusiano baina yetu na Mungu. Uhusiano huu hauji ghafla, unahitaji muda mwangi. Wakristo wengi wanapata shida katika jambo hilo. Hawahitaji kuwa na muda wa kutosha, au kutoa kipaumbele katika kuufanya hai uhusiano wao na Mungu. Neno la Mungu katika Warumi 12:2 linasema wazi kwamba kwa huruma zake Mungu, tunahitaji kuitoa miili yetu iwe dhabihu ilioyai, ndiyo ibada yetu yenye maana. Kwa kufanya hivyo, kila siku tutakuwa tunaifanya upya mioyo yetu iondokane na maisha ya kale. Matokeo na ahadi iliyopo baada ya kufanya hivyo ni kwamba tutaweza kufanya mapenzi ya Mungu katika maisha yetu.



**Kuenenda** kama inavyostahili kunategemea msalaba wetu. Katika Luka 9:23 imeandikwa hivi "Akawaambia wote, mtu ye yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, **ajitwike msalaba** wake kila siku, anifuatu."



**Kumbuka, uhusiano wetu na Mungu ni agano la damu.  
Ili kuufanya halali uhusiano huu, wanahitajika watu wawili  
na vifo viwili.**

**Kila siku tunafanya chaguzi kadhaa.** Uchaguzi tunaoufanya unaweza kutupeleka karibu au mbali na Mungu.

a. **Uchaguzi wa mema au mabaya.** Kukubali au kukataa kuiba, kusema uongo, kudanganya, uzinzi na uasherati, umbeya na kadhalika. Je, tunalitii Neno, au miili yetu?

b. **Majaribu na mateso.** Kukubali au kukataa kulitumaini Neno la Mungu kuliko mazingira yetu. Je, tunalitumaini Neno au miili yetu?

c. **Mamlaka.** Kukubali au kukataa kutawaliwa na Yesu na Roho Mtakatifu. Kukubali au kukataa mamlaka ambayo Mungu anaweka juu

yetu, kama vile walimu, wachungaji, polisi, wazazi, na kadhalika. Kama huwezi kumtii aliye juu yako, ondoka. Kama wanakuambia utende dhambi, usiwatii. Mungu atakulinda na mamlaka au utawala mbaya.

**d. Dunia.** "Dunia" ni ufalme wa kiroho kama vile Ufalme wa Mungu. Katika 1 Yohana 2:15-16 Neno la Mungu linasema tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima hutokana na "dunia". Kila wakati tunapochagua mojawapo ya hayo, tunakwenda mbali na Mungu.

**Sisi siyo wakamilifu, lakini tunaweza kuenenda na kuishi katika toba.** Tunaweza kukosea hapa na pale, lakini Mungu hutupatia msamaha kamili, kana kwamba hatujawahi kutenda dhambi kamwe. Tunasoma 1 Yohana 1:9 kwamba "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Mungu anajua kwamba wengi wetu tunakosea si kwa sababu tunataka kufanya hivyo bali kwa sababu tunakuwa tumeathiriwa na kitu fulani. Dawa yake siyo kutupiga makofi, bali huja na kutufahamisha sisi ni akina nani katika Yeye, na kutupa tumaini litakalotufanya kumkaribia Yeye zaidi.

**Usiwe kama Esau.** Esau alikuwa ndugu pacha wa Yakobo. Esau, kwa nje, hakuonekana mbaya kuliko ndugu yake pacha Yakobo. Yakobo, alikuwa mwongo, lakini Mungu alilingilia kati na kwa muujiza alimpa Yakobo haki ya mzaliwa wa kwanza, ingawa Yakobo alikuwa wa mwisho kutoka tumboni mwa mamaye. Esau aliidharau haki yake, kwa kufikiria kwamba hakiuwa kubwa sana, akaiuza kwa Yakobo kwa bakuli la mchuzi. Baadaye alipojaribu kutubu hakuweza kurudishiwa haki yake. Tuna haki ya kuzaliwa ya kiroho, tunapozaliwa na Mungu, na hilo ni onyo kwetu tusiidharau haki hihi. Tunaweza kuwa kama Esau (Waembrania 12:16).

### Kuenenda kwa Roho

Katika Wagalatia 5:16 tunasoma maneno yafuatayo "Basi nasena, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili."

Vile vile katika Warumi 8:1 tunasoma maneno haya "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo." (wasioenenda kwa mwili bali kwa Roho).

**Kuenenda kwa Roho ni njia rahisi ya kuishi lakini iliyo tofauti. Ni njia rahisi kabisa ninayoifahamu ya kuenenda kwa unyofu mbele za Mungu kila siku. Ili kuishi katika njia hiyo inabidi kufuata hatua kama hizi zifuatazo:**

- Endelea kuliangalia Neno la Mungu** (kioo) na umwombe Mungu akuonyeshe jinsi ya kuishi. Mwombe Mungu na utafute kujua viwango anavyotaka uishi ni vipi. Kwa mfano, Neno la Mungu linasema usiseme uongo, watendee marafiki zako kwa upendo, watii wazazi na walimu wako, watendee ndugu zako vyema, usilewe, usiwe mchoyo, usikasirike, kila wakati samehe, na kadhalika.
- Amua kuishi katika njia ambayo Mungu anataka uishi**, ukijua kwamba ni Mungu pekee ndani yako auezaye kukusaidia kuishi maisha yampendezayo.
- Ukishindwa, (unawenza kushindwa)**, uwe mkweli kabisa, mbele za Mungu na wengine wanaokuzunguka. Tubu (geuka) haraka. Ahadi ni kwamba tunapotubu (tunapogeuka) ufalme wa Mungu unakuwa karibu yetu.
- Kiri dhambi zako kwa Mungu.** Biblia inasema katika 1 Yohana 1:9 kwamba “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”
- Kiri yale ambayo Neno la Mungu linasema** kuhusu hali yako. Kwa maneno mengine, kiri maandiko yafuatayo katika Wagatalia 2:20 “Nimesulibowi pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, minao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitaa ~~hafsi~~ yake kwa ajili yangu.”
- Utakavyokuwa unaendelea kuishi namna hii** tabia zile za zamani na njia za dhambi ulizokirwa ukifanya zamani zitaanza kutoweka. Neema ya Mungu itakuwa pamoja nawe na kukupa tabia ya Mungu badala ya tabia yako ya zamani.
- Neema itakaa ndani yako badala ya dhambi zako.** Hukuhesabiwa haki kwa matendo uliyofanya, kwa hiyo haki yako bado ipo pale pale, ila tu ina vumbi. Wakati unapoendena kwa Roho, Mungu anakupa neema kwa ajili ya makosa yako, anachukua adhabu ya dhambi ambayo ungestahili kupata, anakupa baraka usizostahili.
- Siyo tu kwamba neema inakuondolea dhambi**, na pia siyo tu kwamba Mungu anakupa baraka usizostahili, bali neema unayopokea ni nguvu inayokuondolea dhambi (au tatizo) unalohangaika nalo.

**Ulimwengu unatuhukumu  
Kwa sababu hiyo inabidi ujitzame kwenye kioo**

Biblia inasema katika Yakobo 1:23-25 kwamba “Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.”

Neno la Mungu ni hakimu wetu kama jinsi kioo kilivyo hakimu wetu. Hutuangalia na kisha hutuambia ukweli wa yale yaliyo mema na yale yaliyo mabaya. Lakini tunaweza kuona uchafu usoni, tukaenda zetu na kusahau kuuondoa uchafu ule. Yakobo anasema tunaweza kufanya vivyo hivyo tunapoliangalia Neno la Mungu. Tunaweza kuona yale tunayopaswa kufanya lakini tukaenda zetu kana kwamba hatujayaona kamwe. Iwapo mtu anayetii amebarikiwa, basi mtu asiyetii amelaaniwa!

### **Kutii Neno ni jambo lenye nguvu!**

1. Lina “**beba msalaba wako**” linakamilisha agano la damu na kukuweka chini ya ulinzi wa Mungu.
2. **Linamfanya Shetani aondoke katikati yako.** Bado atajaribu kukudhuru, mambo mabaya yanaweza kuonekana, lakini hayawesi kukudhuru. Katika Mathayo 7:24-27 tunasoma maneno yafuatayo “Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya menanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.”
3. **Linakuandaa kwa uzima wa milele.** Jinsi unavyozidi kutii, ndivyo Yesu anavyozidi kukupa Roho wake na kuydhiiirisha kwako. Pia, kuna kitu kinachotokea ndani kwa muda fulani, kinachokutenganisha wewe na ulimwengu na kukufanya uwe karibu na Yesu. Utakapofika mbinguni, utapata nafasi ya kuwa karibu na Yeye milele!
4. **Siku zote kuna thawabu ya kutii Neno lake.** Katika Yohana 14:23 tunaona kuwa thawabu yetu ni kwamba Mungu atatupenda, atakuja kwetu na kukufanya makao kwetu. Na hapo tunapata uzoefu wa uzima wa milele, tunakuwa washiriki wa tabia ya Uungu!
5. **Unakuwa mtumwa wa yule unayemtii.** Je, utamtii Yesu au mtu mwengine? Neno la Mungu katika Warumi 6:16 linasema “Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.”

**Utii kwa Mungu haujengwi juu ya hofu** kwamba usipomtii atakuadhibu, bali umejengwa juu ya ukweli kwamba unampenda na unataka kumpendeza. Katika Yohana 14:21 tunaambiwa kwamba “Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.”

**Ukitaka kumuona mtu anayempenda Mungu, angalia huku na kule uone ni nani anayetoka kwake ili kwenda kumtii Mungu!**

Sasa hebu tuangalie kioo.  
Tafadhali rejea kile kiambatisho cha  
**Kujichunguza Kiroho katika**  
**Sura ya Mto Utiririkao**

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Sura ya 7 – Kupinga

Umewahi kununua kitu fulani kisichofanya kazi kisha ukaamua kukirudisha kwa mwenye duka? Hivyo ndivyo Wakristo wengi wanavyofanya. Wanaskia Habari Njema, lakini hawangojei muda wa kutosha ili kuona zikidhihirika katika maisha yao, badala yake huzirudisha kama kitu kisichofanya kazi!

### Wakati mwagine ni vigumu kuamini kuamini ukweli tusiuonona

**Hakuna Ushindi bila Mapambano** – Ni lazima tutambue kwamba tunaishi katika eneo la adui. Lengo la adui ni kuwafanya waliopotea waendelee kupotea na kwenda jehanum. Lengo lake kwa Wakristo ni kuwafanya wavutwe sana na ufalme wa dunia hii na mifumo yake ya fedha, burudani, mamlaka, kupendwa na watu, na kadhalika, ili wasijue kwamba wanaweza kuishi katika ufalme ulio juu zaidi, Ufalme wa Mungu. Shetani hatumii kila wakati mambo “mabaya” kutujaribu, wakati mwagine hutumia mambo “mazuri” ya ulimwengu kutuvuta mbali na Ufalme wa Mungu. Shetani hutumia mazingira na mawazo kutudanganya kwamba HATUJAKETI pamoja na Kristo, na kwamba hatupaswi KUENENDA kama anavyoenenda na kwamba tunapaswa kukata tamaa badala ya KUSIMAMA katika ahadi za Mungu. Sisi ni warithi wa Ufalme wa Mungu, sasa kwa nini tuishi kama watu wasio warithi?

#### *Kuzipingo hila za mwovu*

Katika Waefeso 6:11 tunaambiwa “Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.”

**Sasa kwa kuwa tunafahamu Kuketi (sisi ni nani katika Kristo),  
na Kuenenda (kuishi maisha yanayompendeza Bwana),  
tumejiandaa kwa vita vya kiroho, Kuzipingo hila za Shetani**



+



=



Msalaba wake +  
Kuketi

Msalaba wako  
Kuenenda na Kupinga

= Ushindi

**Mpango wa Mungu wa kushughulika na mahitaji yako yote**  
ni kukupa tunda kutoka katika mbegu ya Neno. Mpango wa Shetani ni

kuzuia tunda hilo kwa kuiba mbegu na/au kukufanya usizae. Kupinga ni hatua ya mwisho katika kuzaa matunda kwa ajili ya maisha yako. Kupinga ni kwa ajili ya wale tu waliopokea KUKETI na KUENENDA. Kupinga ni kushikilia kwa subira, uaminifu, uvumilivu na kuongea maneno ya imani hata kama mazingira yanaonekana kuwa mabaya, au hata kama unajisikia vibaya. Ni kuyatendea kazi yale ulioyifunza katika Kuketi na Kuenenda kila siku.

### **Hivi ndivy o inavyofanyika**

Yesu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake katika Marko sura ya 4. Aliwaambia kwamba siri ya Ufalme wa Mungu imo ndani ya mfano huu. Akawauliza katika mstari wa 13, “Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?” Yesu alitumia mfano huu unaohusiana na kilimo, unaoonekana kwa wazi, wa mbegu inayopandwa, ili kuelezea na kufunua siri ya ulimwengu usioonekana. Katika Marko 4:9-11 imeandikwa hivi: “Akasema, Aliye na masikio ya kusikilia, na asikie. Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano. Akawaambia, Nin yi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje *yote hufanywa* kwa mifano.”

**Ufalme wote wa Mungu unafanana na mfano huu.** Mungu hupanda mbegu za maneno yake ndani ya miyo yetu (bila kujali hali ya miyo yetu). Mbegu hizi zinawakilisha makusudi yote ya Mungu katika maisha yetu, kuanzia siku tunapozaliwa mara ya pili hadi tunapoja zwa Roho Mtakatifu, kuponywa kimwili na kiakili, kupewa mahitaji yetu, kuwa na mahusiano mazuri kimaisha na kila kitu kingine ambacho Mungu anatukusudia. Yote hayo hufanyika kwa mbegu ya Neno inayokuwa imepandwa.

Neno la Mungu katika **Marko 4:14-20** linasema hivi “Mpanzi huyo hulipanda neno. Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa miyoni mwao. Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kw furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa. Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, likawa halizai. Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu

walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia.

**Umeona sasa kwamba Shetani huja kuliiba Neno.** Hii hasa ndio silaha pekee aliyo nayo Shetani dhidi ya wanadamu; kuliiba Neno au kutupofusha tusilione Neno (2 Wakorintho 4:4). Mtu yejote akilipokea Neno la Mungu, ataatokolewa na kwenda mbinguni. Mtu yejote akilipokea na kuliadini Neno la Mungu, ataponywa roho, nafsi na mwili, atapata mahitaji yake, maisha yake yatakuwa mazuri. Shetani hawesi kumdhuru mtu yejote anayeliamini Neno la Mungu. Anaweza (na ndivyo anavyofanya) kumjaribu, anaweza kumuwekeea ishara zitakazolifanya Neno lione kane kana kwamba siyo la kweli, lakini hawesi kukudhuru kama umejitoa kabisa kuongozwa na Neno, na Neno ni Yesu mwenyewe!

Kila wakati tutahitaji kupambana na mambo magumu, hata hivyo tunaweza kushinda. Mungu mwenyewe ndiye anayetupatia ushindi. Mara nydingi mambo hayaendi kama tulivyopanga. Hata hivyo tunapaswa kumtumaini katika mambo yote!

**Shetani akiweza kukufanya uishi katika utu wa kale (kimwili) na kwa kuzifuata njia za ulimwengu,** anaweza kukuibia ahadi za Mungu. Katika Wagalatia 5:19-21 tunasoma maneno yafuatayo “Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria. Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ujisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uacuri, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyoziwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.” (Mbegu ya Neno ikizaa matunda katika maisha yako.)

**Kwa hiyo, kwa kutumia njia rahisi sana, ya kitoto, ya kuangalia vita vya kiroho,** hebu tulenge macho yetu kwenye silaha pekee ya Shetani na juu ya itikio letu kwa vitendo vyake. Vita vya kiroho, havijawekwa kwa ajili ya mtakatifu wa Mungu ambaye amekuwa akiendelea na Mungu kwa miaka 20. Hapana, vita hivyo viro kwa kila mtoto wa Mungu; na Mungu anatuwezesha sisi sote kupigana vita kwa nguvu na uweza wake. Hatuhitaji kuwa mabingwa. Kumbuka, Mungu humpa neema mnyenyekemu. Tunasoma hivyo katika Yakobo 4:6 “Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema **wanyenyekemu.**”

**Kuna hatua ambazo Mungu anafuata katika kuleta  
mapenzi yake duniani**

**Inachukua muda kubadili matatizo yetu kuwa baraka, na pia  
inahitaji subira kuendelea kung'ang'ania hata baada ya  
matumaini yote kuonekana yametoweke**

Katika Luka 19:11-13 wanafunzi wa Yesu walifikiri kwamba ufalme wa Mungu ungekuja duniani saa ile ile na kwamba matatizo yao yangetatuliwa siku inayofuata. Akawafundisha wanafunzi wake somo linalokuhusu pia wewe na mimi.

“Waliposikia hayo, aliongeza kusema mfano, kwa sababu alikuwa karibu na Yerusalem, na wao walidhani ya kuwa ufalme wa Mungu utaonekana mara. Basi akasema, mtu mmoja kabaila, alisafiri kwenda nchi ya mbali, ili ajipatie ufalme na kurudi. Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, **fanyeni biashara** hata nitakapokuja.” (Luka 19:11-13).

Akawasimulia mfano kuhusu mtu mmoja aliyesafiri kwenda nchi ya mbali ili ajipatie ufalme na kurudi. Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, **WAFANYE BIASHARA** hadi atakapokuja. Lakini wengi wao walichukia sana mamlaka yake

**Kulikuwa na makundi manne va watu waliokuwepo siku aliporudi**

1. **Kundi lililochukia mamlaka yake** na ambalo halikutaka mtu ye yote awatawale lilifukuzwa mbali naye na kuuawa.

2-3. **Wengine WALIZIFANYA BIASHARA** zile fedha. Kulingana na mafanikio yao walipewa fedha zaidi na kuzawadiwa mamlaka juu ya miji mingi.

4. **Wengine HAWAKUFANYA BIASHARA** kwa sababu walifikiri mtu yule ni mgumu na kwamba angewaadhibu kwa **KUFANYA BIASHARA**. Licha ya kutopata thawabu yoyote, fedha zao zilichukuliwa. Zitumie au zipoteze!

Nini maana ya maneno haya **KUFANYA BIASHARA**?

**KUFANYA BIASHARA ni kutafuta faida.** Kwa ufanuzi zaidi, biashara ni kuchukua mali ghafi au huduma, kuongeza thamani juu yake na kuifanya iwe na faida zaidi ili iwe na manufaa au iuzwe. Ni

kubadilishana au kubadilisha kabisa kitu na kukifanya kuwa chenye manufaa. Maneno hayo yametumika katika Biblia kuelezea watu waliokuwa na biashara, mashamba yenyne ng'ombe na biashara nyingine nzuri na mbaya.

Tunasoma katika **Mithali 3:13-15** kwamba “**Heri mtu yule aonaye hekima**, Na mtu yule apataye ufahamu. Maana biashara yake ni bora kuliko biashara ya fedha, Na faida yake ni nyingi kuliko dhahabu safi. Yeye ana thamani kuliko marijani, Wala vyote uvitamanivyo havilingani naye.”

**Tunapaswa kubadili matatizo yetu kuwa faida.** Tunapaswa kuchukua mali ghafi za matatizo na kuzifanya biashara kwa kuzalisha baraka. Neno jingine ni kupatanisha, ambalo linamaanisha kumbadilisha adui kuwa rafiki.

### **Mathayo sura ya 25 inafunua siri hii**

**Mfano wa Talanta; Mathayo 25:14** ni mfano unaofanana sana na ule wa Luka 19. Mtu alisafiri akawapa watumwa wake talanta wazifanyie biashara hadi atakaporudi.

**Wanawali wenyе Busara na wanawali Wapumbavu:** Katika Mathayo 25:1 tunaambiwa juu ya wanawali 5 wenyе busara na wanawali 5 wapumbavu. Tofauti pekee waliyokuwa nayo ni kwamba wanawali wapumbavu walishindwa kuendelea kungojea muda mrefu wakati bwana aristi alipochelewa kutimiza ahadi yake. Wanawali wapumbavu hawakuwa na mafuta ya kutosha kuendelea kungojea muda mrefu.

Wanawali maana yake ni kwamba dhambi zao zilikuwa zimesafishwa mbele za Bwana. Kwa hiyo wote walikuwa wameokoka. Tofauti ni katika kuwa wenyе busara au wapumbavu. Busara ni kumsikia Mungu akisema. Taa ni Neno la Mungu (Zaburi 119 na Mithali 6:23) na mafuta ni Roho Mtakatifu. Yote hayo yakijumlishwa pamoja yanaleta uvumilivu, subira, uweza wa kudumu na tunda la Roho. Wanajua kwamba Bwana wao atakuja kuwaokoa hata kama matumaini yote ya **KIBINADAMU** yametoweka. Wanaendelea kuyangojea yale ambayo Yesu aliwaambia bila kujali lolote. Bwana atarudi sasa katika hali uliyo nayo kubadili matatizo yako kuwa baraka. Wanawali wenyе busara au hekima walimfahamu bwana wao jinsi alivyo. Nawasikia wakisema, “Sisi hatujali akichelewa, yeye ni mtu wa heshima na uaminifu, atalitimiza neon lake. Hawezi kutuacha wala kutusahau.” Kila wakati wanawali wenyе busara walikuwa pamoja na

Mungu na Neno lake na Roho wake Mtakatifu kwa namna ambayo hakuna kitu cha kuwaondoa.

Sasa HEKIMA hii ni nini?

**Hekima ni kujua na kuutumaini ukweli kwamba msalaba wa Yesu ulifyonza uovu wote na kila kitu lazima kigeuke kuwa baraka.** Sheria ya uvutano inasema kwamba chochote kinachokwenda juu LAZIMA kirudi chini. Sheria ya Roho wa Uzima katika Kristo Yesu (Warumi 8:1-2) inasema kwamba umeachwa huru mbali na maovu yote, na sasa ni lazima upate baraka, KAMA unaamini.

Hekima ni kujua kwamba watu wote wamepatanishwa kwa njia ya Msalaba. Siyo tu watu bali pia mambo yote. “Na kwa yeze kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeze, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi au vilivyo mbinguni.” (Wakolosai 1:20)

**Kupatanisha ni neno lenye nguvu. Itifaki ya Strong** inalielezea neno hilo kuwa ni “kurejesha hali ya zamani ya mapatano.” Maana nyininge ya neno hilo ni, “kutengeneza, kurejesha katika hali nzuri ya mwanzo, kufanya amani kati ya pande mbili au makundi mawili yanayopingana.” **Kamus ya Biblia ya Vines** inalielezea neno hilo kuwa ni, “kubadili hali ya uadui kuwa ya urafiki.” Msalaba wa Yesu Kristo unachukua “maadui” wetu wote, kwamba ni watu, pepo, mazingira, magonjwa, umaskini, kila kitu, na kuvibadilisha kuwa marafiki. Hii ni Hekima ya Kristo aliyesulibiwa!

2 Wakorintho 5:18 inasema, “lakini vyote pia, vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi wake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho;” Kwahiyo hii ndiyo huduma yetu hapa duniani, kuwchukua maadui wetu wote, kuwachovya katika damu na Msalaba wa Yesu Kristo, na kuwageuza kuwa marafiki. Nakwambia, kwa Neno la Mungu na kwa uzoefu wangu mwenyewe, kwamba jambo hili ni kweli, linafanya kazi, ukisimama imara.

**Hekima ni kufahamu kwamba Shetani ameshindwa kwa damu ya Yesu.** Ina maana gain kuwa na ushindi juu ya Shetani? Damu ya Yesu inatupaje sisi nguvu? “Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeze naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeze aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.”(Waebrania 2:14,15)

“Lakini tukiwa tumekufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena.” (Warumi 6:8,9)

Mistari hii inasema kwamba Shetani “aliharibiwa”. Hiyo inamaanisha nini hasa? Anaonekana akikimbia huko na huko akifanya kazi ya kuwaharibu wengine.

**Neno kuharibu katika Itifaki ya Strong's limeelezwa kuwa ni:**

- 1) kusababisha kitu kisifanye kazi, kutokuwa na kazi, kutotenda chochote, kutofanya lolote.
- 1a) Kumfanya mtu au kitu kisiwe na manufaa tena
- 1b) Kumuondolea mtu nguvu, uwezo wake wa kuathiri na silaha zake.

**Wakati Yesu na wewe na mimi tulipofufuliwa kutoka katika wafu,** tulizaliwa tena kama uzao mpya usiotawaliwa tena na Shetani. Hana tena mamlaka juu yetu. Badala yake sisi ndio wenye mamlaka juu yake. Shetani alitumia nguvu zake zote juu ya Yesu pale Msalabani, lakini Yesu alifufuka baada ya pale. Shetani hana tena zana wala silaha.

Anaweza kumharibu mtu asiyemwamini Yesu, na anaweza pia kumdanganya mwamini, lakini tukiija kweli, hawezi kamwe kutudhuru. Ukweli ni kwamba, ameharibiwa. Tukisimama katika kweli, anachowenza tu kufanya Shetani ni kutudanganya. Shetani hana nguvu juu ya kiumbe kipyaa. Kiumbe kipyaa ni wewe na mimi!

“Naye ndiye kihya cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.” (Wakolosai 1:18)

**Ayubu sura ya 28 inaonyesha kwamba hekima ya kweli inapatikana hasa katika mateso.** Tunasoma hayo katika Ayubu 28:12 “Bali hekima itapatikana wapi? Na mahali pa ufahamu ni wapi?” Ninaamini kwamba jibu la swali hilo linaonyesha kuwa, miili yeu inapokufa, tunapopita katika bonde la uvuli wa “mauti” tunaweza kusikia hekima ya kweli. Tunasoma katika Ayubu 28:22 kwamba “Uharibifu na Mauti husema, Tumesikia habari zake kwa masikio yetu.” Mithali 11:2 pia inaunga mkono maneno hayo ikitsemwa, “kijapo kiburi ndipo ijapo aibu; bali hekima hukaa na wanyenyekemu.”

**Haya ni maneno yenyeye uzima.** Tunahitaji kuyafahamu. Yatatufanya tuweze kustahimili mateso. Ndiyo, Yesu atarudi tena duniani, lakini pia atarudi kwa ajili yako sasa, kubadili tatizo lako kuwa baraka.

Mfano mzuri wa mtu aliyepata ushindi huu ni Danieli katika tundu la simba katika Danieli sura ya 6. Danieli alikuwa akimfuata Mungu kikamilifu na kwa sababu hiyo akateswa na maadui zake na maadui wa Mungu. Badala ya kutolewa katika tundu la simba, aliwashinda simba ndani ya tundu hilo. Matokeo yake ni kwamba maadui zake walishindwa kabisa.

“Mfalme akaamuru, nao wakawaleta wale watu waliomshitaki Danieli, wakawatupa katika tundu la simba, wao, na watoto wao, na wake zao, na wale simba wakawashinda wakaivunja mifupa yao vipande vipande, kabla hawajafika chini ya tundu. Ndipo mfalme Dario akawaandikia watu wa kabilia zote, na taifa zote, na lugha zote, waliokaa juu ya uso wa dunia; amani na iongezeke kwenu. Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli; maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho. Yeye huponya na kuokoa, hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, ndiye aliyemponya Danieli na nguvu za simba. Basi Danieli huyo akafanikiwa katika enzi ya Dario, na katika enzi ya Koreshi, Mwajemi.” (Danieli 6:24-28).

Siamini kama Danieli angefanikiwa na maadui zake kushindwa kama asingeingia katika tundu la simba.

### **Wajibu wetu ni kini tunapokuwa katika kipindi cha kungoja?**

Kusimama kunahitaji tuianye kitu fulani, hatupaswi tu kukaa na kungojea. Waebrania 6:12 inasema, “Hii msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na ujumilivu.”

Ni lazima tuutunze “ubikira” wetu. Hii ina maana kwamba ni lazima tukae safi mbele za Bwana. Hatuhitaji kukaa na dhambi, badala yake tuziungame na kuwa safi mbele za Mungu na wanadamu.

### **Naamini pia kwamba Biblia inatufundisha kwamba wakati wa kipindi hiki cha kungojea, tunahitaji kulitumia Neno la Mungu kama upanga.**

Waefeso 6:17b inasema, “Na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu.”

Tunaambiwa katika Waebrania 3:1 “Kwahiyo, ndugu watakatifu, wenyewe kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu, Yesu,” Yesu huchukua maungamo yetu kwa Baba kama Kuhani wetu Mkuu, na Baba

huhakikisha kwamba hilo linafanyika, maadam ni Neno la Mungu. Adui naye huchukua maungamo yetu yaliyo kinyume na kufanya yale tunayosema.

**Tunapolikiri Neno la Mungu na kuomba** kwa kutumia Neno juu ya mtu au hali fulani, lina nguvu sana! Yesu aliumba kila kitu kwa Neno lake. Yesu NI Neno. Yesu alitupa mamlaka ya kutumia Neno kana kwamba ni Yeye anayelitamka!

**Yohana 1:1-3, inasema “Hapo mwanzo kulikuwako Neno,** naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeche hakikufanyika chochote kilichofanyika.”

Pasaka ilipoadhishwa na Wana wa Israeli katika Kutoka 12 , Wana wa Israeli waliambiwa kuweka damu ya mwana-kondoo asiye na ila juu ya milango yao na malaika wa mauti (pepo) “atapita juu” yao bila kuwadheru. Yesu ni Mwana-Kondoo wa Mungu, tunaweza kuweka damu yake juu ya milango yetu na milango ya wapendwa wetu na juu ya wale tunaowaombea. Kwa njia gani?

Ufunuo wa Yohana 12:11 inasema, “nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.”

**Maneno ya vinywa vyetu yataiweka damu.** Ukiangalia katika Kutoka 12 unaona kwamba ile damu iliyokaa tu ndani ya bakuli haikufanya lojote jema. Lakini walipochukua hisopo na kuichovya ndani ya damu na kisha kuipaka juu ya milango yao, hapo Shetani na Mungu walianza kuionga damu. Hisopo ulikuwa mmea wa kawaida tu ulioonekana hauna thamni. Maneno ya vinywa vyetu hayaonekani kuwa na thamani lakini tukiyachovya katika Neno la Mungu (ambalo ni Yesu mwenyewe) na kuyatumia kama damu, Mungu huyaona na pia Shetani huyaona!

**Yesu huchukua maungamo yetu na kuyafanya kuwa na nguvu sana.** Waebrania 3:1 “Kwahiy, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu, Yesu.”

**Tunapolitamka Neno la Mungu, Yesu hulipeleka kwa Baba na kumuomba alitende.**

Yohana 16:23 inasema, “Tena siku ile hamtauliza neno lolote. Amini, amini, nawaambia, mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa jina langu.”

**Hatimaye tunaweza kuingia katika raha na kuliacha Neno lifanye kazi.**

Waebrania 4:1 inasema, “Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wetu asije akaonekana ameikosa.”

Waebrania 4:12 inasema, “Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake.”

### **Malaika huenda kufanya kazi wanapolisikia Neno la Mungu.**

Zaburi 103:20 inasema, “Mhimidini Bwana, enyi malaika zake, ninyi mlion hodari, mtendao neno lake, mkiisikiliza sauti ya neno lake.”

### **Pepo hutoka!**

Zaburi 149:5-9 inasema, “Watauwa na waushangilie utukufu, waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao. Sifa kuu za Mungu na ziwe kinywani mwao, na upanga mkali kuwili mikononi mwao. Ili kufanya kisasi juu ya mataifa, na adhabu juu ya kabilia za watu. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo, na wakuu wao kwa pingu za chuma. Kuwafanya hukumu ilioandikwa; hiyo ndiyo heshima ya watauwa wake wote. Haleluya!”

**Kwa kweli, hii siyo nzuri hata kwa Shetani. Angalia jinsi Mungu  
anavyomtendea.  
Mtakanyaga nyoka!**

Neno la Mungu katika **Luka 10:19** linasema “Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga **nyoka** na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowachuru.

Adui alishindwa hata kabla vita hajiaanza. Biblia inasema katika Yoshua 11:18-20 kwamba “Yoshua ekapiga vita siku nyingi na wafalme hao wote . Haukuwapo mji hata mmoja uliofanya amani na wana wa Israeli, isipokuwa ni wale Wahivi wenye kukaa Gibeoni; wakaitwaa yote vitani. Kwa kuwa lilikuwa ni la BWANA kuifanya mioyo yao kuwa migumu, hata wakatoka kupigana na Israeli, **ili apate kuwaangamiza kabisa, wasihurumiwe** lakini apate kuwaangamiza (maadui), kama vile BWANA alivyomwamuru Musa.”

**Endelea kutafakari juu ya tatizo lako baya kuliko yote. Sasa  
tafakari au angalia ahadi katika Neno la Mungu.**

**Sasa amua mwenyewe. Ni jambo gani linaloweza kubadilishwa,  
na lipi haliwezi kubadilishwa?**

**“Watu na wakushukuru, Ee Mungu, Watu wote na wakushukuru. Nchi imetoa mazao yake MUNGU, Mungu wetu, ametubariki.” (Zaburi 67:5,6).**

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

**Sehemu ya 2 – Semina ya 2  
Damu na Moto!**

**Kwa kuwa sasa umeanza vizuri, unahitaji nguvu ya kumaliza mashindano.**

**Sura ya 8-11 zinazungumzia:**

8.     **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Utangulizi**
9.     **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Msalaba**
10.    **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ukombozi**
11.    **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ubatizo katika Roho Mtakatifu**

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Sura ya 8 - Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano – Utangulizi

Katika Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, sura 7 za kwanza, tulijifunza kwamba lipo tumaini kwetu sisi tusioweza kupata tumaini katika “mfumo wa dunia”. Tuliona kwamba tukiacha kuutegemea ulimwengu, ufalme wa Mungu utakaribia (utakuwa karibu nasi).

Tulijifunza kwamba Yesu alifundisha katika Marko 4:11 kwamba siri ya ufalme wa Mungu imo ndani ya mfano wa mpanzi. Alifundisha kwamba Neno la Mungu ni mbegu, mioyo yetu ni udongo na matokeo yake ni matunda.

Matunda yatabadilisha tabia zetu zifanane na tabia ya Yesu, yatatupa mahitaji yetu binafsi na pia yatusukuma kwenda katika ulimwengu unaoangamia kuzaa matunda ya uzima wa milele kwa ajili ya wengine.

**Tulijifunza kwamba mbegu hupitia hatua nyingi ili kuwa tunda halisi  
Hii hapa ndiyo dhamira ya kitabu cha “Kukua au Kufa.”**

- 1) Tunahitaji kuugeukia ufalme wa Mungu na Neno ili tuzae matunda.
- 2) Tunahitaji kujuja jinsi ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu - yaani Mto Utiririkao.
- 3) Tunahitaji kujuja jinsi ya kutoka na kukaa mbali na hali ya kuwa Wafungwa katika nchi ya Ahadi.
- 4) Tunahitaji kujuja zaidi tabia ya Mungu - Mungu ni Nani
- 5) Tunahitaji kujuja sisi ni akina nani katika Kristo - KUKAA.
- 6) Tunahitaji kuubeba msalaba wetu na kuenenda katika hali ya kultini Neno - KUENENDA.
- 7) *Tulijifunza katika somo la KUPINGA kwamba kuna adui wa kiroho anayepinga mambo yote hayo. Huyu ni Shetani na pepo wake. Tulijifunza kwamba tunahitaji uvumilivu na nguvu ya kumpinga adui huyu hadi matunda yanapopatikana. Kwa maneno mengine, tunahitaji kumngoea Bwana aje aitimize ahadi. “Ili msiwe wavivu, bali mkawe wafiasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu” (Waebrania 6:12).*

Namshukuru Mungu iwapo umeyashika mambo hayo yaliyoletwa kwetu kwa njia ya Neno la Mungu. Kama umefanya hivyo, unahitaji nguvu katika maisha yako ili kukamilisha hatua na kuona udhihirisho wa matunda katika maisha yako.

Kama jinsi mimea inavyohitaji maji na mbolea ili ipate nguvu hadi inapozaa matunda, sisi pia tunahitaji nguvu. Sehemu ya 2 imelenga kukusadia kufahamu jinsi ya kujitwalia nguvu hii.

## Maisha yetu katika Kristo sio uzoefu, bali ni mashindano.



**Ni jambo zuri kuanza mashindano**, hata hivyo tunahitaji kujua jinsi ya kumaliza. Watu wengi huanza lakini hawamalizi. Tunahitaji **nguvu** ya kumaliza mashindano vinginevyo tutashindwa. Katika Waebrania 12:1 tunaambiwa hivi: “Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila **mzigo** mzito, na **dhambi** ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale **mashindano** yaliyowekwa mbele yetu.”

### **Maandiko yanatuambia kuwa nguvu tunayohitaji inapatikana katika:**

**1. Msalaba au damu ya Yesu.** “Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu” (1 Wakorintho 1:18).

**2. Nguvu ya Mungu ya kukomboa.** “Alipokuwa katika kumwendea, pepo akambwaga chini, akamtia kifafa. Yesu akamkemea pepo mchafu, akamponya mtoto, akamrudishia babaye. Wote wakashangaa, wakuiona ukuu wa Mungu” (Luka 9:42,43a).

**3. Ujazo wa Roho Mtakatifu.** “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

**Mungu hakutuacha yatima hapa duniani** tuihudumie wenyewe hadi tutakapokufa na kwenda mbinguni. Mungu ni mwewye busara. Ana njia ya kututunza, lakini wengi hawaijui njia hiyo. “Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu” (Yohana 14:18). Yesu alikuwa akizungumzia kuja kwa Roho Mtakatifu. Katika sura zifuatazo tutaangalia jinsi Roho Mtakatifu alivyo muhimu katika kutufanya tusiwe yatima au watu wasio na msaada katika dunia hii.

**Msalaba wa Yesu ndio uliomshinda Shetani** na kutupatia ushindi. Hiyo ni nguvu. Tukiutendea kazi ukweli wa Msalaba tunapata nguvu. Hata hivyo, nakubali kwamba ukweli wa msalaba hauwezi kuonekana kikamilifu katika maisha yetu pasipo nguvu inayozungumzwa katika Mdo 1:8, yaani ujazo wa Roho Mtakatifu.

**Kwa mfano**, nguvu ya kuwashaa taa katika jengo hutokana na jenereta inayotengeneza umeme. Unaweza kusimama kando ya soketi ukutani na kuifurahia soketi hiyo huku ukijua kwamba ina nguvu ndani yake. Hata hivyo usipochomeka kifaa cha umeme kwenye soketi hiyo, utakuwa bado hujafaidika

na nguvu ya umeme. **Tutachunguza kuhusu ukweli** wa nguvu ya msalaba, na pia tutachunguza jinsi ya kuufanya ukweli huo uwe wako binafsi katika maisha yako.

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

## Sura ya 9 – Nguvu ya kupiga mbio katika mashindano – Msalaba

### Hebu kwanza tuangalie Msalaba na damu ya Yesu

**Msalaba wa Yesu Kristo** umekuwa ukizungumzwa na Wakristo kwa maelfu ya miaka, hata hivyo ni watu wachache sana wanaoelewa maana kamili ya msalaba na jinsi unavyohusika na maisha yao. Watu wengi wamesikia juu ya damu ya Yesu, lakini hawajaelewa kikamilifu thamani yake na maana yake ya kweli.

**Katika Yohana sura ya 6**, Yesu aliwaona watu wengi maskini, na kwa huruma akawalisha kwa muujiza wa mikate na samaki. Jambo hili lilikuwa kubwa sana kwa watu wale kiasi kwamba waliamua kumfuata Yesu hadi ng'ambo ya pili ya ziwa ili waweze kula tena kwa muujiza mwgingine.

**Yesu alikataa kufanya muujiza ule ule siku iliyofuata.** Akawaambia watu wale kwamba ana dawa ya kuuondoa kabisa umaskini wao. Akaonyesha kwamba watu wale walikuwa wanahitaji kuondokana na umaskini wao kwa njia ya agano la damu. Walihitaji kula mwili wake na kunywa damu yake. Wengi wao walikwazika, wakifikiri kwamba alikuwa akiwaambia wawe wala watu na kuula hasa mwili wake wa nyama. Hatimaye akawaambia kwamba ikiwa neno lile linawakwaza itakuwaje basi wamwonapo akipaa huko alikokuwako kwanza?

**Kisha Yesu alianza kuzungumzia mambo ya kiroho**, Akasema, “Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima” (Yohana 6:63). Alikuwa akimaanisha kwamba kama unataka kunywa damu na uzima wa Mungu, unapaswa kufanya hivyo kwa njia ya Neno lake. Soma habari niya! Katika Yohana sura ya 6.

**Ukombozi wetu kutoka katika kila aina ya “umaskini”** katika maisha unapatikana katika agano la damu inalefanywa kati ya mwanadamu na Mungu. Msalaba na damu ya Yesu vinawakutisha agano la damu.

#### Shetani anatudanganya na kutupofusha tusione nguvu halisi ya Msalaba

Ha! Ninachopaswa tu kufanya ni kuwadanganya hawa Wakristo kwamba wanaweza kushika sheria nyingi ili kumpendenza Mungu na kwamba wanaweza kuishi maisha ya ushindi kwa nguvu zao wenye. Kwa njia hiyo, hawataweza kamwe kiuona ikweli wa Msalaba



**Shetani anajaribu sana kuficha ujumbe wa kweli wa Msalaba.** Katika Wagalatia 3:1 tunasoma maneno yafuatayo: “Enyi Wagalatia msio na akili, ni nani aliyewaloga, ninyi ambaño Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulibiwa?”

Tunasoma pia katika Wagalatia 3:10 kwamba “Wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye.”

Paulo alikuwa akiwaambia hawa Wagalatia waliomwamini Yesu kwamba wameelogwa na Shetani waudharau Msalaba na kuzingatia mambo mawili:

1. **Kushika sheria.** Kuishi kwa sheria badala ya kuwa na uhusiano na Yesu.
2. **Nguvu ya mwili au utu wao wa kale.** Kujaribu kuishi kwa nguvu zaowenye.

Uchawi ni nguvu inayojaribu kukutawala na kukudhibiti na kukuweka chini ya mamlaka potofu. Kila wakati nguvu hii hudhibiti na kutawala. Kwa njia hii, Wagalatia waliwekwa chini ya mamlaka ya pepo aliyewadanganya kwamba wangeweza kumpendeza Mungu kwa miili yao na kwa kushika sheria. Hilo lilificha Injili halisi na nguvu ya Msalaba.

**Kama ungekuwa Shetani**, na Yesu amekushinda kabisa Msalabani, na ukajua kwamba watu wa Mungu wanaweza kudanganywa wasijue kuhusu kushindwa kwako na ushindi wao, ungefanya nini?

**Ungeeneza uongo unaosema**, “mnahitaji kushika sheria zote hizi ili muwe safi mbele za Mungu, na kwamba mnawenza kwa nguvu zenu wenyewe kutenda kila jambo analotaka Mungu. Hamhitaji kujua nguvu ya Msalaba na Damu ya Yesu. Hayo ni mapokeo tu ya kidini?” Uongo huu ndio ule ule ambao yule Kijana Tajiri katika Mathayo 19 alilogwa nao. Soma sura hiyo.

**Paulo alifadhaishwa na mafundisho haya** ndio maana alisema kwa ukali maneno yafuatayo katika Wagalatia 1:8, “Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.”

**Mtume Paulo alihubiri Msalaba tu.** Kulingana na Wagalatia 6:14-15, Paulo alioneshwa kwamba kushika sheria sio jambo linalopaswa kuhubiriwa. Badala yake, ~~Paulo alihubiri Msalaba, na hilo lilisababisha kuzaliwa mara ya pili.~~

**Shetani hutumia nguvu zake kuitatao katika ukweli wa Msalaba kwa sababu unawakilisha agano la damu kati ya Mungu na wanadamu.**

**Msalaba ndio uliomshinda Shetani.**

**Tutaangalia vipengele viwili vya agano la damu:**

1. **Sheria ya kubadilishana**
2. **Urafiki wa karibu sana**

## **Agano la Damu**

### **Kubadilishana**

a. Sheria ya urithi

b. Sheria ya kubadilishana

### **Urafiki wa karibu sana**

Maneno husababisha urafiki wa karibu na kisha huleta kubadilishana

### **1. Kwanza, tutazungumzia kuhusu sheria ya kubadilishana**

**Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Mungu aliweka sheria ambazo ni msingi wa sheria ya kubadilishana.**

**Zote zinafanya kazi kwa damu**



**Zote zinafanya sheria ya kubadilishana**

- 1. Sheria ya Kubadilishana katika agano la damu  
(sehemu 2)  
Sehemu ya 1-A ni sheria ya urithi**

**Sehemu ya 1-B ni sheria ya kubadilishana**

**1-A Sheria ya Urithi**

**Tunarithi baraka na laana kutoka kwa mababu zetu walioishi vizazi vingi vilivyopita**



### **Mungu alipanga kwamba uhai wa mwanadamu uwe katika damu.**

Tunasoma hivyo katika Mambo ya Walawi 17:11, "Kwa kuwa **uhai** wa mwili u katika hiyo damu; nami nimewapa ninyi hiyo **damu** juu ya madhababu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo **damu** ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi." Biblia inasema pia katika Yohana 6:56 kwamba, "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake."

**Tunarithi baraka na laana kutoka kwa mababu zetu.** Katika kitabu cha Kutoka 34:6-8 imeandikwa hivi, "BWANA akapita mbele yake (Musa), akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwelesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Musa akafanya haraka, akainamisha kichwa chake hata nchi, akasujudu." **Mstarini huo unaonekana kama fumbo la maneno.** Inakuwaje Mungu awe mwenye kusamehe na wakati huo huo si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia?

**Tunajisababishia baraka na laana kwa dhambi zetu wenye.** Katika Warumi 6:23 tunasoma maneno yafuatayo, "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Vile vile katika Wagalatia 6:7 tunaambiwa hivi, "Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna."

**Je, sheria ya urithi inakaa wapi? Inakaa katika mwili au katika roho?**

Inakaa katika mwili na roho. Ndiyo sababu watu hufanana na wazazi wao. Sehemu isiyoonekana ya kile kilichorithiwa katika roho huwapumbaza watu wengi. Kuna sehemu mbili za jitu zinazoweza kuwa na uhai au urithi wa kifamilia.

Katika Yohana 3:5-6 tunasoma maneno yafuatayo, "Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mta asifozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho."

**Maisha ya kimwili.** Maisha ya kimwili hubeba sura na umbo la mwili.

**Maisha ya kiroho.** Maisha ya kiroho ni maisha yanayobeba urithi wa baraka na laana.

**Hiyo haionekani kuwa sawa, lakini kuna ufumbuzi**



**Hii ni Habari Njema!**

**Mfano.** Sheria ya mvutano huifanya ndege ikae juu ya ardhi. Lakini ndege inapoambaa kwa haraka kwenye barabara ya ndege, sheria ya kuinua huchukua nafasi na kuibatilisha sheria ya mvutano. Vivyo hivyo, sheria ya kubadilishana huibatilisha sheria ya urithi.

**Sheria hii inamaanisha kwamba watu wanaweza kuzaliwa** katika ukoo fulani na kutoka katika ukoo ule watapokea baraka na laana kama urithi wao, lakini laana zinaweza kubadilishwa. Baadhi ya watu katika makabila ya Afrika, katika utamaduni wa Wahindi wekundu na katika jamii za Kiasia wamekuwa wakitafuta njia ya kubadilishana baraka na laana. Huweza kubadilishana silaha, makoti, na vitu vingine vya thamani kama ishara kwamba kila mmoja amejitoa kwa mwингine na kwamba wako tayari kulindana hadi kifo. Katika baadhi ya tamaduni za Kiafrika, kama familia imepanga mtoto, baba humwaga damu na kuiweka katika mikono ya mtoto huyo ili kumfanya wa kwake.

**Tangu zamani, watu wamekuwa wakinywa damu** inayotolewa kwa miungu yao, ili waweze kuwa kama Mungu.

**Kabla ya kuwekwa misingi ya Dunia**, Mungu alikuwa amepanga kwamba Yesu asulibiwe kulingana na Roho wa MILELE. Hii ina maana kwamba kanuni ya kubadilishana ilikuwa ikifanya kazi hata kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu.

Biblia ~~inasema~~ katika Ufunuo 13:8b kwamba, "...katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia."

**Mfano mzuri wa sheria ya kubadilishana ni Pasaka.** Katika kitabu cha Kutoka 12:13-14 imeandikwa juu: "Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nani nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakaperipiga nchi ya Misri. Na siku hii itakuwa ukumbusho kwenu, nanyi mtaifanya iwe sikuu kwa BWANA; mtaifanya iwe sikuu katika vizazi vyenu vyote, kwa amri ya milele." Maisha ya mwanakondoo, yanayowakilishwa na damu yake, yalichukua nafasi ya mzaliwa wa kwanza katika familia. Mwanakondoo aliuawa badala ya mtoto wa kwanza kuzaliwa. Mwanakondoo wa Pasaka hakutakiwa kuwa na dosari, alipaswa kuwa mkamilifu.

**Hii ndio sababu Yesu alizaliwa na bikira**, asiyechafuliwa na dhambi ya uzao wa Adamu. Ukamilifu na hali ya kutokuwa na mawaa ndiyo njia pekee iliyomuwezesha kuwa Mwanakondoo wetu wa Pasaka. Baba yake alikuwa Mungu, na mama yake alikuwa Mariamu. Ni Mungu kamili na pia mwadamu kamili. Ni Adamu wa pili, asiyeha na dhambi, mwenye uwezo wa kuchukua dhambi zetu.

**Hii inaelezea lile fumbo** katika Kutoka 34:6-8. Njia pekee aliyokuwa nayo Mungu ya kuwapatia wanadamu rehema bila kuacha kuwaadhibu

watenda dhambi, ni kumwadhibu Yesu, Mwanakondoo mkamilifu wa Mungu, badala yao.

**Mungu alikuwa ametabiri kwamba sheria ya kubadilishana itakuwepo katika agano jipya.** Neno la Mungu katika Yeremia 31:29-34 linasema hivi: "Siku zile, hawatasema tena, Baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi. Bali kila mtu atakufa kwa sababu ya uovu wake mwenyewe; kila mtu alaye zabibu kali, meno yake yatatiwa ganzi. Angalia, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano lile nililofanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema BWANA. Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema BWANA; nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue BWANA; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo mionganoni mwao hata aliye mkubwa mionganoni mwao, asema BWANA; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena."

**Maisha ya kiroho yanaweza kubadilishana na sheria ya kibadala.**

**Agano la damu hubadilisha urithi wa familia yako.**




Maisia yangu  
ya kale yalijaa  
laana na  
dhambi.  
Na kutengwa na  
Mungu



Utu wako wa  
kale unaweza  
kubadilishwa na  
agano la daramu.

Asili ya  
Mungu ni  
baraka tu



Mtume Paulo katika Wagalatia 2:20 anasema: "Nimesulibwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

Katika Isaya 53:4-6 tunasoma pia maneno yafuatayo: "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhwiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."

**Kwa miaka mingi, watu wamejitatidi kubadilisha maisha yao ya  
kiroho kwa kubadili damu**

**Tamaduni nyingi bado zinafanya agano la damu.** Hata hivyo, agano hili halitendi kazi inayokusudiwa kwa sababu linakuwa limefanywa kimwili tu. Wahusika katika agano hilo wanaweza kujitoa kila mmoja kwa mwenzake, lakini ndani ya mioyo yao hakuna kitu kinachokuwa kimebadilika; roho zao zinakuwa bado zile zile. Maneno ya Mungu katika Waebrania 9:13-14 yanasema, "Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyoniyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kusafisha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na mafendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?" **Kuna mambo mengi bandia yanayotumiwa na tamaduni za kale na washirikina.**

**Msalaba au agano la damu linatubadilishia nini? Msalaba ulitupatia  
nini, na kumpa Yesu nini?**

**Mimi mhalifu?**




**KWA AJILI YAKO**

**Kwanza, msalaba ulimpa Yesu hali yetu yote. Alikufa kifo cha mhalifu kwa sababu tulikuwa waasi.**

**Sisi sote tulikuwa waasi na wahalifu kabla Mungu hajatukomboa.** Dhambi ya Adamu na Hawa ilikuwa uasi. (Uasi ni kutokutii sauti ya Mungu na Neno lake). Kwa sababu hiyo, sisi nasi tulizaliwa katika uasi au dhambi

Katika Waefeso 2:1-6 Biblia inasema, “Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwinci wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu.”

**Habari za Baraba.** Katika Mathayo 27:16 tunaambiwa kwamba Baraba alikuwa mfungwa mashuhuri. Kulikuwa na misalaba mitatu Golgotha. Ile misalaba miwili, kila upande, ilitengenezwa kwa ajili ya wahalifu. Na je, msalaba wa katikati ultengenezwa kwa ajili ya nani? Kwa ajili ya Yesu? Hapana. Kwa ajili ya **Baraba**. Yesu alichukua nafasi ya Baraba.



Katika Isaya 53:4-6 tunaona kwamba Yesu alichukua yale tuliyopaswa kuyapata. Imeandikwa hivi: “Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.

**Pili, msalaba ultupatia hali aliyo nayo Mungu na yote aliyo nayo.**

**Mambo yaliyoorodheshwa ukurasa unaofuata ni baadhi ya mabadilisho makubwa ambayo Yesu aliyafanya kwa ajili yetu ili tuwe na furaha timilifu. (Angalia maneno yaliyo kinyume!). Baadhi ya hayo ni mizigo, na baadhi ni dhambi. Mzigo ni kitu kizito kinachokulemea au kukukandamiza, hasa hasa kile kilichowekwa kwako na mtu mwengine. (Waebrania 12:1).**

**Kukubali nguvu ya msalaba itakukomboa kutokana na haya laana na zinginezo kuu. Kuwa tayari!**

**Msamaha: Alichukua hatia yetu ili tuweze kusamehewa.**

**Wakolosai 2:13 inasema,**

**13 Mlipokuwa wafu katika dhambi zenu na kutokutahiriwa katika asili yenu ya dhambi, Mungu aliwafanya mwe hai pamoja na Kristo. Alitusamehe dhambi zetu zote,**

**Uponyaji: Alichukua mapigo kumaanisha vidonda vya damu, ili tupate kupona. 1 Petero 2:24 inasema**

**24 Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponya.**

**Haki: . Msalabani Yesu alichukua dhambi zetu juu yake ili tufanyike wenye haki.**

Hii ni mojawapo ya mabadiliko makubwa ambayo ni ya milele. Tumekuwa wenya haki na kuhesabiwa haki kwa imani, kwa vile tu msalaba ilitengeneza njia kwa ajili ya roho mtakatifu ili aishi ndani yetu

**2Wakorintho 5:21 inasema**

**21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuishi haki ya Mungu katika Yeye.**

**Kifo ya milele , Jehanamu. Yesu aliteseka kwa ajili yetu jehanamu ili tuweze kuishi mbinguni milele.**

Yesu aliondolewa kwa baba kupitia kifo ili tuweze kufarahia uwepo wake Mungu milele

**Wahibrania 2:9 inasema**

**9 Lakini twamwona Yesu, aliyefanywa chini kidogo kuliko malaika, sasa akiwa amevikwa taji ya utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu.**

**Matendo ya Mitume 2:24**

**24 Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeche kushikiliwa na nguvu za mauti.**

### ***Haya ni maelezo zaidi kuhusu neno kifo***

Kifo cha mwili yaani kutenganishwa kwa nafsi kutoka kwa mwili ambayo kwa njia hiyo maisha hufika kikomo duniani; kwa dhana kuwa baadaye huwa na dhiki jehanamu.

### ***Ukombozi kutokana na laana za kuridhi pamoja na zile za kujiletea***

#### ***Wagalatia 3:13,14 inasema***

*13Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikwa, “Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti.”*

*14Alitukomboa ili kwamba baraka aliyopewa Abrahamu ipate kuwafikia watu Mataifa kwa njia ya Kristo Yesu, ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Raho.*

### ***Ukombozi kutokana na umaskini***

#### ***2Korintho 8:9 inasema***

*9Kwa maana mnajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba ingawa alikuwa tajiri, kwa ajili yenu alikubali kuwa maskini, ili kwa umaskini Wake ninyi mpate kuwa matajiri.*

#### ***2 Korintho 9:8 inasema:***

*Na Mungu aweza kuajaza kila neema kwa wingi; ili ninyi, mkiwa na riziki wa kila namna ziku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema*

Utoshelevu ni ya kutosha tu, bali utele ni zaidi ya kutosha ili tuweze kuwa Baraka kwa wengi.

### ***Kukombolewa kutokana na hatia na aibu***

Tunaweza kuhisi upendo wa Mungu ambayo itachukua nafasi ya hatia na aibu.

-Dhuluma ya kimapenzi husababisha aibu

-Tunapata fikira ya utumwa kutokana na aibu

-Tunapata shida na adhi kutokana na aibu

Msalabani na kupitia maisha ya Yesu duniani, alichukua aibu yetu.

Alitambuliwa na wengi kuwa motto ambaye mimba yake ilipatikana nje ya ndoa. Aibu na hatia huzuua uhusiano yetu na mungu, huwa kama kizuizi vya kiroho ambayo hufanyika kuonekana kana kwamba mtu hawezi kuwa na uhusiano , mazungumzo ya kindani pamoja na Mungu.

### ***Wahibrania 10:21-22 inasema,***

*21basi kwa kuwa tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu, 22 sisi na tumkaribie Mungu kwa moyo mnyofu kwa imani timilifu, miyo yetu ikiwa imenyunyizwa damu ya Kisto na kuwa safi kutokana na dhamiri mbaya nayo miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji safi.*

**Isaya 53:2-9 inasema,**

2Alikua mbele yake kama mche mwororo na kama mzizi katika nchi kavu. Hakuwa na uzuri wala utukufu wa kutuvuta kwake, hakuwa na cho chote katika kuonekana kwake cha kutufanya tumtamani.

3Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nydingi, ajuaye mteso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu.

4Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa.

5Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.

6Sisi sote, kama kondoo, tumepeotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, naye BWANA aliweka juu yake maovu yetu sisi sote.

7Alionewa na kuteswa, hata hivyo hakufungua kinywa chake, aliongozwa kama mwana kondoo apelekwaye machinjoni, kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya amkataye manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake.

8Kwa kukamatwa na hukumu aliondolewa. Ni nani atakayeweza kueleza kuhusu kizazi chake? Kwa maana alikatiliwa mbali na nchi yawalio hai, alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu.

9Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu, pamoja na matajiri katika kifo chake, ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

**Kukbolewa kutokana na kukataliwa na kutopendwa**

Vidonda nya nafasi na roho za wengi mara nydingi husababishwa na kukataliwa. Hii kutokana na wazazi kutowapenda watoto wao bila masharti. Wazazi hao huwakataa watoto wao waziwazi. Talaka husababisha kukataliwa sio tu kwa watu wazima, bali pia na watoto. Nimewaona watu wengi ambaao wametiwa vidonda kwa sababu ya kukataliwa. Ni mojawapo ya sababu kuu inayo leta vidonda katika nafsi ya wengi.

Baba Mungu alificha uso wake kutoka kwa Yesu akiwa msalabani. Yesu naye akalia

**Mariko 15:34 kinasema**

34Mnamo saa tisa Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, ‘‘Eloi, Eloi lama Sabakthani?’’ Maana yake, “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?”

**Waefeso 1:6 inasema**

6Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpandwa.

### **Waefeso 3:16-20 inasema**

16Namwomba Mungu awaimarishe kwa kuwatia nguvu mioyo yenu kwa njia ya Roho Wake kwa kadri ya utajiri wa utukufu Wake,

17ili kwamba, Kristo apate kukaa miyoni mwenu kwa njia ya imani. Nami ninaomba kwamba ninyi mkiwa wenyewe mizizi tena imara katika upendo, 18mwe na uwezo wa kufahamu pamoja na watakatifu jinsi ulivyo upana na urefu na kimo na kina upendo wa Kristo

19na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wa Mungu.

20Basi kwa Yeye auezaye kutenda mambo ya ajabu yasiyopimika kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya uweza Wake ule utendao kazi ndani yetu,

### **Kukombolewa kutokana na kuteswa, huzuni na majonzi**

Isaya 53 inatuonyesha jinsi Yesu alivyoteswa na kuhuzunika kwa ajili yetu

### **Isaya 35:10 inasema,**

10Lakini yalikuwa ni mapenzi ya BWANA kumchubua na kumsababisha ateseke, ingawa BWANA amefanya maishayake kuwa sadaka ya hatia, ataona uzao wake na kuishi siku nyingi, nayo mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake.

### **Kukombolewa kutokana na vyote vinavyosababishwa na mwili na asili ya kitambo**

#### **Wagalatia 5:19-24 inasema**

19 Basi matendo ya mwili ni dhani ni nayo ni haya: Uasherati, uchafu, ufisadi,

20kuabudu sanamu, uchawi, uadui, ugoimvi, wiwi, basira, fitina, faraka, uzushi,

21husuda, ulevi, ulafi na mambo engine yanayofanana na hayo. Nawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya kabla, kwamba watu watendao mambo kama hayo, hawataurithi Ufalme wa Mungu.

22Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23upole, kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.

24Wote walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na tamaa zake.

**Msalaba ulikuwa kamili (thabiti).** Msalaba ulimshinda Shetani (na kila namna ya ubaya) na kumnyang'anya silaha. Msalaba ulishinda hata mabaya yanayoonekana kwamba yanakuja kwako. Chochote kile kinachokupiga, ni lazima kitageuka kuwa baraka. Katika Wakolosai 2:14-15 tunasoma maneno yafuatayo: "(Yesu) akiisha kuifuta ile hati iliyoadikwa ya

kutushitaki kwa hukumu zake (haki zote alizokuwa nazo Shetani za kututendea uovu), iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea **msalabani**; akiisha kuzivua enzi na mamlaka (pepo na Shetani), na kuzifanya mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.” Soma pia Marko 16:15-19 na pia Warumi 6:9.

**Vitu vyote vimepatanishwa kwa njia ya msalaba.** Siyo tu watu, ni vitu vyote. “na kwa yeze kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeze, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.” (Wakolosai 1:20)

**“Kupatanisha” ni neno zito. Itifaki ya Strong** inalifafanua neno hilo kuwa ni “kurudisha hali ya upatanifu iliyokuwepo mwanzo.” Itifaki hiyo inaendelea kufafanua neno hilo kuwa ni “kukarabati, kurejesha utaratibu unaofanya kazi vizuri, kuleta amani kati ya makundi mawili yanayopingana.”

Nayo **Kamusi ya Biblia ya Vines** inalieleza neno hilo kuwa ni “kubadili hali ya uadui kuwa ya urafiki.” Msalaba wa Yesu Kristo unachukua maadui zetu wote, kama ni watu, pepo, mazingira, magonjwa, umaskini, na kila kitu kibaya na kuvibadilisha kuwa marafiki.

Biblia inasema katika 2 Wakorintho 5:18 kwamba, “vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho.” Hii ni huduma yetu hapa duniani; kuchukua maadui wote wa maisha yetu, kuwazamisha katika damu na msalaba wa Yesu Kristo na kuwageuzea kuwa marafiki. Nakuambia kwa Neno la Mungu na kwa usoefu wangu mwenyewe kwamba hii ni kweli. Inafanya kazi ukisimama imara.

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

**Unawezaje kuzifanya faida za Msalaba kuwa halisi katika maisha yako?**


**Unawezaje kuwa na ushirika wa karibu na Mungu?**



**Ni lazima ubebe msalaba WAKO**

*Reproduction, resell, and distribution prohibited*

**Msalaba wa Yesu Kristo uzakia pale bila nguvu hadi pale tutakapouunganisha na msalaba wetu. Hapo ndipo Agano la Damu linapokuwa halisi kwetu.**



**Watu wanadharau nguvu ya chaguo letu. Ni kitu cha pili chenye nguvu sana katika ulimwengu, baada ya nguvu ya Mungu.**

“Akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha. Kwa kuwa yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza, au kujipoteza mwenyewe?” (Luka 9:23-25).

**Hapa kuna mtihani ili kupima utayari wako wa kubeba msalaba  
WAKO. Weka Ndiyo au Hapana mbele ya kila kifungu.**

Usifanye hivyo kabla ya kufikiri sana na kujitoa. Haya ni masuala mazito ya uzima na mauti. Hivyo usimdanganye Mungu, na wala usijidanganye mwenyewe. Ni bora uache kuweka ndiyo au hapana kama hujamaanisha.

\_\_\_\_\_ **Niko tayari kuwa mkweli kuhusu hali yangu (ya mizigo au dhambi) – niko tayari kuwa mkweli kabisa!**

\_\_\_\_\_ **Nimechoshwa na mizigo na dhambi zangu, nataka kuwa huru**

\_\_\_\_\_ **Nimechoshwa na hali ya kujaribu kuishi maisha mema kwa nguvu zangu mwenyewe. Naligeukia Neno la Mungu ili nizae matunda, sawasawa na mapenzi yake.**

\_\_\_\_\_ **Natubu, (nafuata uelekeo mwingine) na kumuomba Mungu anisaidie.**

\_\_\_\_\_ **Naya~~zacha~~ mambo ya “ulimwengu” huu.**

\_\_\_\_\_ **Naamini yale~~wahiyenewa~~ katika Neno kwamba Yesu amechukua mizigo na dhambi zangu.**

\_\_\_\_\_ **Namfanya Yesu kuwa Bwana na nimeamua kumfuata kwa njia ya Neno lake na Roho wake.**

\_\_\_\_\_ **Nabadili mapenzi yangu na kuweka mapenzi ya Mungu. Nawasamehe wale wanaoniumiza.**

\_\_\_\_\_ **Nabadili nia yangu na kuweka nia ya Mungu.**

\_\_\_\_\_ **Nabadili hisia zangu na kuweka hisia za Mungu.**

\_\_\_\_\_ **Niko tayari kupitia mateso na simuonei aibu Yesu.**

\_\_\_\_\_ **Niko tayari kutengwa na ulimwengu bila kujali watu wanafunikiriaje.**


- \ \_\_\_\_\_ Niko tayari kuwa mwaminifu kwa kile nilicho nacho mkononi mwangu sasa hivi.
- \_\_\_\_\_ Nitaishi kwa Neno lake kila siku na kutumia muda mwingu kulitafakari.
- \_\_\_\_\_ Nitaendelea kuamini kwa kulifuata Neno na kumfanya Yesu kuwa Bwana wangu. Nitatoa nafasi ya kwanza katika kujenga uhusiano na Mungu.
- \_\_\_\_\_ Nitasimama kinyume na uongo wote wa Shetani, hata kama itachukua muda mrefu.
- \_\_\_\_\_ Nitatoka katika makundi ya wasio haki na kukaa na Mungu.
- \_\_\_\_\_ Nitatupilia mbali kiburi changu na kumuomba Mungu anipe yote aliyo nayo.



### Maelekezo

**KAMA** umeweka **NDIYO** mbele ya kila kifungu, unaweza kuendelea. Lakini kama hukujibu **NDIYO**, inabidi umuombe Mungu aubadilishe moyo wako. Anaweza kufanya hivyo.

1. Sasa fungua ule ukurasa wa mabadilishano ambapo mambo 16 ya kubadilishana yameorodheshwa. Chora kiduara kwenye “balbu” zinazohusika.
2. Angalia maandiko na uyakiri kwa kinywa chako.
3. Yaandike kwenye karatasi na uyasome kwa sauti kila siku



**Sasa mshukuru Yesu kwa yale aliyokutendea**

*Reproduction, part of the copyright holder's terms of use*

## **2. Sasa tutazungumzia urafiki wa karibu katika agano la damu.**

Ninaamini kwamba watu wengi hawaelewifizuri urafiki wa karibu. Kila mtu aliyeumbwa na Mungu anahitaji urafiki wa karibu. Sisi sote tunahitaji urafiki wa karibu, lakini hatujui njia sahihi ya kuutafuta na kuuonyesha. Watu wamepotosha urafiki wa karibu kwa njia nyingi.

Watu wengi, wanapofikiria urafiki wa karibu, wanafikiri juu ya kujamiihana. Kujamiihana ni sehemu ndogo sana (na ni matokeo) ya baadhi ya aina za urafiki wa karibu, hata hivyo siyo kipengee muhimu.

**Urafiki wa karibu kwa mtoto.** Madaktari wamegundua kwamba watoto wadogo wasipokuwa na rafiki wa karibu, watakuifa. Sisi pia kama watoto tumeumbwa kuwa na urafiki na wazazi wetu. Ni kitu kinachohitajika. Ndivyo Mungu alivyotuumba. Wazazi wengi sana huwaumiza watoto wao katika maisha yao yote kwa kukosa kuwapa urafiki wa karibu. Huwfundisha kwamba kukumbatia na kulia ni mambo yasiyofaa. Huwaambia wasiseme mahitaji yao, bila kujua kwamba baadaye mahitaji yao yatajitekeza kwa njia potovu.

**Urafiki wa karibu kwa mume na mke.** Mara nyingi huwa tunapata urafiki wa karibu wakati wa uchumba. Lakini baada ya kuoana, wanaume huwatenda vibaya wake zao kama watumwa.

**Urafiki wa karibu na Mungu.** Mungu anataka kuwa na urafiki wa karibu na sisi. Alitupatia ule Wimbo Ulio Bora kama mfano wake kuhusu jambo hili. Fungua kitabu hicho, usome mistari ifuatayo: 2:14, 7:13, 8:6-7. Kitabu cha Luka 10:39 kinazungumzia juu ya Mariamu aliyeketi miguuni pa Yesu, akisikiliza Neno lake. Yesu aliona jambo hilo kuwa ni la thamani sana!

**Urafiki wa karibu hutokana na maneno, kutizamana machoni** na kuwa na muda wa kukaa pamoa.

**Hali ya kuwa wawili peke yenu ni moja kati ya mambo muhimu katika urafiki wa karibu.** Kila mmoja wenu anahitaji kujua kwamba hakuna wengine wanaohusika. Kila mmoja anahitaji kujua kwamba mwenzake amejitoa kwake tu. Baadhi huiita hali hii kuwa ni jicho moja. Uhusiano katika ndoa hufananishwa na urafiki wetu wa karibu na Bwana.

**Urafiki wa karibu unahitaji kutoka nje ya kundi.** Unahitaji kujitao kikamilifu kwa mwenzako. Yule Kijana Tajiri katika Mathayo 19 hakutaka hasa kuwa na urafiki wa karibu na Mungu, kilichomvutia zaidi ni dini tu. Alitaka zaidi kuwa na mali kuliko uhusiano na Mungu. Angalia tofauti iliyopo kati ya tajiri huyo na Bartimayo katika Marko 10:46. Bartimayo alikuwa na kitu kingine pia cha kutumaini. Hata hivyo alitupa vazi lake alilolitumaini, akaruka na kumfuata Yesu kikamilifu.

**Musa alitaka urafiki wa karibu na Mungu.** Pale kwenye kile kijiti kilichowaka moto, Musa alionja uwepo wa Mungu. Baadaye katika Kutoka 33 alimsihi Mungu amruhusu aone utukufu wake tena. Musa alitaka kuuona utukufu wa Mungu kwa gharama yoyote. Tunahitaji kukaa moja kwa moja ndani ya Yesu Kristo na kuchacha kujangalia wenywewe au kufikiria mambo yanayosemwa na watu wengine.

**Zaburi ya 91 inaelezea Mahali pa Siri pake Aliye juu.** Wimbo Ulio Bora 2:14 unazungumzia kuhusu mahali hapo hapo pa siri kwamba ni mahali pa kuwa na urafiki wa karibu; mahali ambapo watu wawili hutazamana uso kwa uso na kila mmoja husikia sauti ya mwenzake.

Wale watu 120 katika Matendo ya Mitume sura ya 2 walitenga muda wao na kujitao kwa ajili ya uwepo wa Mungu.

**"Yada" ni neno zito zaidi linaloweza kutumika badala ya urafiki wa karibu.** Katika Mwanzo 4:1 tunasoma kwamba Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba. Neno hilo akamjua ni yada, neno la Kiebrania linalomaanisha kujua kwa kiwango cha urafiki wa karibu. Limetumiwa tena katika Mithali 3:5-6 ambapo tunaambiwa tumkiri BWANA katika njia zetu zote naye atayanyosha mapito yetu. Neno kukiria linatokana na neno yada. Yesu alisema katika Yohana 17:3 kwamba uzima wa milele ni kumjua (yada) Mungu na Yesu Kristo.

**Urafiki wa karibu na Mungu** na mwenzi wako wa ndoa hufanya wawili kubadilika na kuwa mmoja. Yesu alibadilika akafanyika dhambi kwa ajili yetu, sisi nasi tunaweza kubadilika na kuwa mmoja na Yesu.

**Tunahitaji kutoka nje ya kundi.** Beba msalaba wako kwa ajili ya madhehebu, marafiki, familia, mila na kiburi. Mwabudu Mungu kwa unyenyekevu na kwa uchaji, huku ukiinama mbele zake.

**Katika somo la Mto Utiririkao,** tulibeba msalaba wetu kwa ajili ya dhambi, kwa ajili ya utashi wetu na akili zetu. Jambo hili bado linaendelea kwa undani zaidi katika maeneo yote hayo matatu. Ni kubebea aibu ya msalaba, na kukaa ndani ya Mungu.

**Wakati urafiki wa karibu unapoanzishwa na Mungu,** itikio letu ni kumwabudu tu Mungu. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu (Ufunuo wa Yohana 4:8-11).

**Katika 1 Samweli 1-2 Hana aliaibishwa na kufedheheshwa** kweli kweli kwa sababu alikuwa na njaa kwa ajili ya kuwa na ukaribu na Mungu. Alikata tamaa. Yule mama aliyeugusa upindo wa vazi la Yesu, ye ye pia alifedheheka na kukata tamaa (Mathayo 9:20).

### **Urafiki wa karibu ni mpango wa Mungu wa kutoa agano la damu.**

**Urafiki wa karibu ni ubadilishanaji wa maneno** baina ya watu wawili. Kila mmoja anakuwa na nafasi ya kumsikiliza mwenzake. Kumbuka maneno ambayo Yesu alishaambia watu katika Yohana 6:63. "Roho ndiyo ifiayo uzima, mwili haufai kitu; **maneno** hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima." (Yohana 6:63).

**Tunahitaji urafiki wa karibu na Mungu kwa kumwambia maneno yetu** na pia kwa kusikiliza Neno lake. Hali hii hulifanya agano la damu lije kwetu.

**Hatupaswi kuwa kama wanyama na kuzatana yifundo vyetu ili kuwa na agano la damu na Mungu!**



**Maneno ni daraja la mawasiliano kati ya ulimwengu huu na ulimwengu wa roho.**

**Maneno yana "damu ya kiroho."** Njia ya pekee ya kufanya agano la damu kati ya wawili, mmoja akiwa katika ulimwengu wa roho na mwingine akiwa katika ulimwengu huu, ni kwa kutumia maneno.

Katika Mathayo 4:4 tunasoma maneno yafuatayo, "Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila **Neno** litokalo katika kinywa cha Mungu."

Katika Waebrania 4:12 tunasoma pia maneno yafuatayo: "Maana **Neno** la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

**Yesu ni Neno.** Alikuwa daraja na hata sasa ni daraja. Katika Yohana 1:1-3 tunasoma kwamba, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo ye ye hakufanyika cho chote kilichofanyika."

Katika Yohana 15.7 tunasoma, "Ninyi mkikaa ndani yangu na **maneno** yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

Katika Yohana 8:51 Yesu anasema, "Amin, amin, nawaambia, Mtu akilishika **Neno** langu, hataona mauti milele."


### **Nguvu ya Mungu ipo karibu nasi!**

Katika Warumi 10:8-11 tunaambiwa hivi, "Lakini yanenaje? Lile **Neno** li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile **Neno** la imani tulihubirilo. Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika."

"Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa." (Mathayo 12:37).

**Uwe na muda na Mungu na ulipatie kipaumbele Neno lake. Litakupa urafiki wa karibu na mabadilishano!**

**Tunataka mambo yatendeke haraka**



**Mungu anasema tunapaswa kuwa wavumilivu.**

**Yesu alishinda uovu wote pale msalabani, lakini uongo una nguvu.  
Shetani atafanya kila analoweza ili kukuibia kile ulicho nacho.  
Uashinda ukivumilia na kusimama imara!**

**Inahitaji kupiga vya Na hii siyo rahisi!**

We mtu,  
mafundisho hayo  
hayatekelezeki



**Inachukua muda na pia inahitaji uaminifu**

Mara nyingi, kabla ya kupokea faida za msalaba mtu anaweza kujaribiwa kwa muda fulani na hivyo anahitaji uvumilivu. Vile vile mtu anaweza kupata mateso na hata kujisikia kana kwamba hatapata ushindi kutoka kwa Mungu.

Neno la Mungu katika Yakobo 1:2-4 linasema, " Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majoribu mbalimbali, mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpare kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno."

Katika Luka 8:8, 15 tunapata pia maneno yafuatayo, "Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri; zikamea, zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, Mwenye masikio ya kusikilia, na asikie. (mstari wa 15) Na zile penye udongo mzuri ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika, kisha huzaa matunda kwa kuvumilia."

Katika Ufunuo 12:11 tunaambiwa, "Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa."

### **Kumngoea Bwana hututakasa**

Biblia inasema katika 1 Petro 1:6-7 kwamba, "Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majoribu ya namna mbalimbali, ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo."

**Msalaba ni kitu halisi, lakini uongo una nguvu**

*Reproduction  
permitted  
by copyright  
holder*  
**Tunahitaji hekima.**

**Hekima ni kujua na kuanzini ukweli huu kwamba msalaba wa Yesu ulifyonza kila namna ya mabaya na kila hali lazima itabadijika kuwa baraka.** Sheria ya mvutano inasema kwamba kila kinachopaa juu LAZIMA kishuke chini. Sheria ya mabadilishano na sheria ya Roho wa Uzima ule ulio katika Kristo Yesu (Warumi 8:1) inasema kwamba uovu wote umevunjwa nguvu na sasa lazima baraka ziwepo. KAMA unaamini.

**Hekima ni kujua kwamba Shetani amekwisha shindwa kwa damu ya Yesu.** "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, ye ye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu ye ye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa." (Waembrania 2:14,15).

**Tunapaswa kubadili matatizo yetu kuwa faida.** Tunapaswa kuchukua mali ghafi za matatizo na kuzifanya biashara kwa kuzaa baraka. Neno jingine ni **kupatanisha**. Neno hili linamaanisha kugeuza adui kuwa rafiki (kupatanisha).

**Kumnganje Mungu ni andiko lenye uzima.** Tunahitaji kutambua tuko wapi katika andiko. Tukijua hivyo tutaweza kuchukuana na hali ya mateso. Ndiyo, siku moja Yesu atarudi tena duniani, lakini atarudi tena kwako sasa kubadilisha matatizo yako kuwa baraka.

(Tafadhali rejea ile sehemu inayozungumzia, Wajibu wetu ni nini katika kipindi cha kungojea?

### Tunao uthibitisho gani kwamba mambo haya ni kweli?

**Ufufuo ni uthibitisho wetu.** Kama Yesu asingefufuka, tusingekuwa na matumaini. Ukweli kwamba alifufuka ni ushahidi wa kutosha kwamba matatizo yako hayawezi kukuumiza kama uko radhi kuwa wakala wa mabadiliko kwa ajili ya Mungu.



*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

**Yesu ni uthibitisho wetu.** Tuna uhakika gani wa kusini ahadi zinazoonekana kana kwamba haziwezi kutimizwa? Mwenyewe aliapa! Neno la Mungu katika Waembrania 6:15-20 linaonyesha kwamba Mungu alitia kiapo kwamba hawezu kusema uongo. Licha ya kutupatia ahadi, alitia kiapo. Kiapo hiki ni sawa na kusema, "Naapa juu ya maisha yangu mwenyewe na kwa maisha yangu mwenyewe kwamba nitatenda ahadi hii. Unaweza kuitegemea kwa kuwa umelikimbilia Neno langu ili upate matumaini. Matumaini haya ni nanga yako ya kushikilia, na nanga hiyo imesimama katika uwepo wangu hasa."

Haya ndiyo matumaini yetu. Na hivi ndivyo tujuavyo kwamba ahadi za Mungu zitatimia. Aliapa mwenyewe; hakuapa kwa mtu mwagine aliye mkuu. Akasema kwamba kama ahadi haitatimia atakuifa.

Alikufa, kwa njia ya Yesu Kristo pale msalabani. Yesu alichukua laana yetu ili sisi tuweze kurithi hali yake na yote aliyo nayo. Namtia moyo kila msomaji ajifunze kitabu cha Waembrania sura ya 6 ili kulielewa vizuri suala hili.

## **Hii hapa ni njia rahisi ya kukumbuka jambo hilo bila usumbu mwingi**

Katika kitabu cha Kutoka sura ya 4, tunaona kwamba Musa alikuwa hana uhakika kuhusu kazi ambayo Mungu alikuwa amempa. Mungu akamwambia aitupe chini fimbo iliyokuwa mkononi mwake. Alipofanya hivyo, ikawa nyoka. Kisha Mungu akamwambia amshike mkia, alipomshika akageuka kuwa fimbo. Huu ndio ujumbe wote kwa muhtasari

Fimbo ni Neno. Neno ni Yesu aliyefanyika dhambi kwa ajili yetu pale msalabani (nyoka). Musa alipomshika yule nyoka muovu, aligeuka kuwa Neno au baraka. Yesu alifyonza uovu wote uliokuwa ndani ya nyoka na kuufanya baraka.

Kwa sababu ya msalaba wa Yesu tunawenza kuwa na uhakika kwamba uovu wowote tutakaougusa utageuka kuwa baraka. Soma Marko 16:18 na kuendelea. Nawe utashika nyoka wala haitakudhuru, badala yake itakufanya uwe mponyaji.



Fimbo-Neno-Yesu-



Akswa dhambi-nyoka



Tunaposhika uovu, hugeuka kuwa Neno, baraka.

## **Sura ya 10 - Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ukombozi**

**Roho Mtakatifu ni nguvu ya Mungu ya ukombozi katika maisha yetu.** “Alipokuwa katika kumwendea, pepo akambwaga chini, akamtia kifafa. Yesu akamkemea pepo mchafu, akamponya mtoto, akamrudishia babaye. Wote wakashangaa, wakiuona ukuu (**nguvu**)wa Mungu.” (Luka 9:42,43a).

**Katika Agano Jipy, Roho Mtakatifu** anatajwa mara nyingi kuwa ni Kidole cha Mungu. “Lakini, ikiwa mimi natoa pepo kwa kidole cha Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia” (Luka 11:20). Yesu alisema wazi kwamba alitoa pepo kwa Roho Mtakatifu.

**Maadui zetu wa kiroho mara nyingi huwazuia waamini** wasipige mbio vizuri na Mungu, kwa kueneza uongo kwamba hawawaathiri Wakristo. Mara nyingi waamini huzongwa na dhambi na mizigo wanayowekewa na pepo. Tunakubali kwamba watu wanaomwamini Yesu hawawezi “kupagawa” na pepo, lakini najua kwamba wanaweza kuonewa na kuathiriwa na pepo. Haina maana kujua pepo anakaa wapi katika maisha ya mwamini. Suala muhimu ni kwamba tunahitaji kuwafahamu pepo hao ili tuweze kuwatoa nje ya maisha yetu, popote pale walipo.

### **1. Pepo ni nini na Shetani ni nani?**

a. **Shetani alikuwa malaika mkuu, Nyota ya alfajiri.** Alikuwa kiongozi wakati wa kumwabudu Mungu. Kulingana na Ezekiel sura ya 28 na maandiko mengine, alikuwa amepakwa mafuta, huenda alikuwa na vyombo vya muziki ndani ya mwili wake. Alikuwa katika bustani ya Edeni pamoja na Adamu na Hawa. Alikuwa na sura nzuri. Anà kipaji kikubwa cha kufanya kazi na biashara. Huenda ndiye aliyeanzisha wazo la kupata utajiri kwa kumiliki watumwa. Ni mwenye majivuno sana, na anatambua uzuri wake mwenyewe. Ana akili sana na pia ni mlaghai. Anafanya mambo kwa mipango.

b. **Nyota ya alfajiri alimwasi Mungu** na kuchukua theluthi moja ya malaika. Akawapanga katika ngazi za kijeshi na kuiga Ufalme wa Mungu (Waefeso 6).

c. **Shetani sasa ni mkuu wa ulimwengu huu** (Yohana 12:31).

d. **Baadhi husema kwamba pepo ni malaika walioanguka,** na wengine husema ni majini labda kutoka katika jamii iliyokuwepo kabla ya Adamu, au labda kutoka kwa mababu zetu. Maandiko hayaelezi hivyo. Lakini, malaika hawakuumbwa ili wakae ndani ya miili ya wanadamu. Inawezekana kwamba pepo ni wale wale waliokuwa malaika na ambao sasa wanatawala na Shetani au pia ni majini yanayoishi ndani ya wanadamu. Sina uhakika juu ya hayo, ninakisia tu. **Hata hivyo, ufanuzi huo siyo muhimu.** Neno au jina

jingine linalotumika badala ya pepo ni "daimon." Neno hili lina maana ya "kuuja," au "ajuaye."

e. **Tabia zao ni chafu kabisa.** Kamusi ya Vines inasema, "pepo ni mawakala wa kiroho wanaojihusisha na kuabudu sanamu. Sanamu yenyewe si kitu, lakini kila sanamu ina pepo anayejihusisha nayo. Pepo huyo ndiye anayewashawishi watu kuiabudu sanamu hiyo na kutoa kafara, 1 Wakorintho 10:20-21; Ufunuo wa Yohana 9:20; Isaya 13:21. Pepo hueneza uongo na kutafuta kuwapotoa watu wanaomwamini Yesu, 1Tomotheo 4:1. Kama roho zidanganyazo huwadanganya watu waamini kwamba kuitia kwa mtu anayewasiliana na mizimu wanaweza kuongea na watu waliofariki. Pepo hutenda kazi chini ya Shetani na wameruhusiwa kutesa kwa magonjwa ya kimwili, Luka 13:16. Kwa kuwa pepo ni wachafu, huwajaribu wanadamu kwa mawazo machafu, Mathayo 10:1. Hutofautiana katika viwango vya uovu, Mathayo 12:45. Watawaendea wafalme wa ulimwengu wote na kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi, Ufunuo wa Yohana 16:14."

## 2. Wanafanya nini?

- a. Kulingana na Yohana 10:10 huiba na kuchinja (kuua) na kuharibu. Kila kitu wanachokifanya kipo ndani ya mambo hayo matatu.
- b. **Kuua.** Mauaji yao yanahusiana na laana ya milele na pia kifo katika maisha haya.
- c. **Kuiba.** Ni wezi. Huiba mapenzi ya Mungu kwako. Huiba Neno la Mungu katika moyo wako. Huiba ubikira, afya, amani, na mali.
- d. **Kuharibu.** Wanaharibu maisha. Wanaharibu kwa madawa ya kulevyaa na magonjwa. Wanaharibu familia. Wanaharibu kwa kutumia nguvu, udhalilishaji wa kijinsia na mepigo kama vile UKIMWI.

## 3. Wanatimizaje malengo yao?

- a. **Kwa kukujaribu** (Mathayo 4:1). Teago lao ni kukutenganisha na Mungu, uishi bila kumtegemea Mungu.
- b. **Husema na mawazo au fikira zako** (2 Wakorintho 10:5)
- c. **Hutoa ishara na maajabu ya uongo.** (2Wathesalonike 2:9).
- d. **Huiba Neno** ili kuwfanya Wakristo wawe vuguvugu wasizae matunda (Marko 4).
- e. **Huwadanganya watu kwamba mashetani na pepo hawapo.** Mara nyingi huwatumiwa watu wanaoonekana kuwa hawana hatia, wazuri, na wakati mwingine hata Wakristo. Nimekutana na watu katika makanisa wanaoonekana kwa wazi kabisa kwamba wana pepo. Watu hao wakaniambia kwamba hakuna pepo wala ulimwengu wa roho. Wanadai kwamba pepo wabaya ni matendo tu yanayofanywa na wanadamu.
- f. **Hujaribu kukufanya utende dhambi** ili waweze kukutawala na Yesu asipate nafasi. Mshahara wa dhambi ni mauti. (Warumi 6:23).

g. **Husema uongo na kuwashutumu watu wasio na hatia** (Yohana 8:44 na 2 Wathesalonike 2:9-10). Walimshutumu pia Yesu kwamba ana pepo. "Maana Yohana alikuja, hali wala hanywi, wakasema, Yuna pepo." (Mathayo 11:18). "Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalem wakasema, ana Beelzebuli, na, kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo."(Marko 3:22).

h. **Huchukua mamlaka ya mwathiriwa** na kumpa mkosaji.

i. **Huwawezesha watu kutumia uwezo au nguvu zao** (pepo). Muziki wa roki, ufalaki, kupiga ramli, na kadhalika.

j. **Huwatesa watu** kimwili, kihisia na kiakili

k. **Hutawala na kuendesha** ridhaa ya mtu. Wanadhibiti utashi, mawazo na mhemuko wa mtu, na kutenda kazi zao kwa njia ya mtu huyo. Husababisha mtu huyo aseme uongo na kuamini uongo wao.

l. **Huchukua mamlaka yasiyo na mpaka**, na kukiuka mamlaka ya kweli.

m. **Shetani huigiza kazi nyangi** za Mungu. Yeye sio mbunifu, haumbi kitu chochote, ananakili tu na kupotosha yale anayoyafanya Mungu.

**Baadhi ya mambo ya kuigiza anayoyatumia Shetani:**

**Shetani ana uwezo wa kusababisha miujiza kutokea.**

Amesababisha baadhi ya Wakristo kuvutiwa na miujiza hiyo. Amewafanya wengine kuogopa sana miujiza hiyo kiasi kwamba wanakosa kazi timilifu ya Roho Mtakatifu.

**Kuna maandiko kadhaa yanayoweza kutusaidia kutofautisha** kazi za Roho Mtakatifu na kazi za mashetani na pepo. Maneno ya Mungu katika 1 Wakorintho 14:33 yanazungumzia juu ya roho ya machafuko. Roho Mtakatifu hacnezi sarakasi. Yupo ili kumfanya Yesu aonekane wazi katika maisha yetu. Kazi za Roho Mtakatifu kila wakati hupatana na Neno la Mungu. Roho Mtakatifu humwihaa Yesu kila wakati na siyo "Yesu mwingine" (2 Wakorintho 11:4). Dini za kishetani haziwezi kukubali kwamba Yesu alizaliwa na bikira, kwamba ni Mungu, kwamba ni Mwana pekee wa Mungu, na kwamba alifufuka katika wafu. Neno la Mungu katika 1 Yohana 4:2-3 linadhihirisha wazi tofauti hiyo.

#### 4. Baadhi ya mifano ya ukombozi na jinsi pepo wanavyotenda kazi.

a. Yesu alimtoa pepo kwa imani ya mwanamke (Marko 7:29).

b.Yule mtu aliyejikuwa na pepo mchafu katika nchi ya Wagerasi alikombolewa, na pepo wakaingia katika nguruwe (Marko 5:1-20).

c.Katika Mathayo 9:32-33 mtu bubu alianza kuongea baada ya pepo kutolewa.

d.Katika Mathayo 10:1-8 Yesu aliwapa wanafunzi wake amri ya kutoa pepo

e.Katika Marko 9:17-29 pepo bubu alikuwa ndani ya mvulana tangu utoto wake.

f. Agano la kale linaonyesha pia kwa kivuli jinsi pepo wanavyotenda kazi. Soma Zaburi 10, 56, 59, 64 na nyingine nyingi. Mifano mingine mizuri ni vita wakati wa Agano la Kale, makabila na watu kama Yezebeli na Balaamu. Soma habari hizo huku ukijua kwamba yale yaliyofanywa na maadui wa wana wa Israeli yalifanywa na pepo.

## 5. Jinsi wanavyopata nafasi katika maisha yako.

a. **Dhambi zako.** Dhambi zote huwapa nafasi pepo, lakini mojawapo ya dhambi zilizo mbaya ni zinaa. Zinaa huwaunganisha pamoja watu wawili kiroho kwa njia ya kipekee.

b. **Dhambi za vizazi.** Pepo huzifuata familia kutoka kizazi hadi kizazi, na wana haki ya kuweka ugonjwa ule ule na laana juu ya familia hizo (sheria ya kurithi). Dini za mashetani zimejengwa juu ya kuabudu mizimu ili kuendeleza laana na kutawala familia. Hujaribu kuwashawishi watu, na hata Wakristo, kwamba ni lazima watoe pesa kwa mganga wa kienyeji ili walindwe. Na baadhi hutoa vitu na mifugo kwa waganga hao wa jadi kwa kusudi la kupata ulinzi na baraka. Watu hawa huamini kwamba kwa kuwasiliana na roho za mababu zao watabarikiwa na kulindwa wasipatwe na mabaya. Lakini ukweli ni kwamba yanayotokea yanakuwa kinyume na matarajio yao. Watu hawa hugeuka kuwa wafungwa wa adui yao, Shetani!

Sikukuu nyingi kama ile siku ya mwisho kabla ya kuanza Kwaresma (Mardi Gras) huko Marekani zimepangwa kuendeleza laana juu ya maeneo kadhaa. Na wakati mwingine hata kukutana kwa familia yote (katika siku maalum) huweza kutumiwa na pepo kuendeleza laana za kifamilia. Ulozi au vuudu (voodoo) na ushirikina yote hayo yana sikukuu zake. Pepo hupata nafasi zaidi katika laana za vizazi na mara nyingi hujaribu kuwateka vijana katika familia. Ndiyo sababu ukosirini na uasi huonekana kwa wazi zaidi watoto wanapofikia umri wa ujana. Wasipatukiwa kuwateka, hujaribu tena baadaye.

c. **Dhambi katika ulimwengu.** Ulimwengu huu umejaa dhambi na hii huchochea kazi za pepo.

d. **Mizigo, au ukandamizaji** unaoweza kuupata kutoka kwa mtu mwingine. Mbini ya mara kwa mara wanayoitumia pepo ni kumnyanyasa kijana kijinsia na hivyo kupata nafasi ya kuingia ndani yake maisha yake yote. Mizigo sio dhambi uliyotenda ila ni ukandamizwaji unaofanyiwa kwa dhambi ya mtu mwingine.

e. **Kwa njia ya sanamu katika maisha yako.** Sanamu inaweza kuwa kitu chochote unachokipa umuhimu kuliko Mungu. Inaweza kuwa mtu, tabia, desturi, au hata dhehebu.

f. **Kuasi mamlaka.** Kama mtu hataki kumpokea Yesu kuwa Bwana wake, mtu huyo, atakuwa chini ya utawala wa kiumbe kingine. Hawa alidanganywa na Shetani, na ye ye akamdanganya Adamu. Adamu angeweza kutumia mamlaka yake dhidi ya Shetani lakini hakufanya hivyo. Kwa kweli, Hawa alipokea mamlaka yasiyokuwa ya kawaida na Adamu naye hakutumia mamlaka aliyopewa. Dhambi ya asili inaonyesha jinsi dhambi na mamlaka

yalivyoungana pamoja. Ni wazi, kwamba wote wawili wangepaswa kutii mamlaka ya Neno la Mungu (Mti wa Uzima).

g. **Wakristo wanaweza kudhurika** (baadhi ya watu wanapinga jambo hili). Kama mtu ana pepo kabla ya kumpokea Yesu, muda unaweza kupita kabla ya kupokea ukombozi. Baadhi ya watu hawapokei ukombozi kwa sababu hawataki kujiachia kikamilifu mikononi mwa Yesu. Ni kweli kwamba Mkristo hawezi kupagawa na pepo, lakini anaweza kabisa kuathiriwa. Jambo muhimu siyo istilahi gani tutumie: kupagawa, kuathiriwa, au kuonewa? Kitu muhimu ni kujua jinsi ya kushinda kazi za pepo katika maisha yetu.

**Maandiko yafuatayo yanaonyesha kwamba bado tunaweza kudhurika** hata baada ya kuamini. "Basi Roho ananena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitetenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani" (1 Tomotheo 4:1). "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshtaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze" (1 Petro 5:8). "Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asiye akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo. Maana yechelele, maana yeye ajaye akihubiri Yesu mwininge ambaye sisi hatukumhubiri, au mkipokea roho nydingine msiyoipokea, au injili nydingine msiyoikubali, mnatenda vema kuvumiliana naye!" (2 Wakorintho 11:3-4).

**Baadhi ya watu husema kwamba damu ya Yesu huwalinda Wakristo.** Ndiyo na hapana. Damu ya Yesu hutulinda tunapokuwa tu Wakristo watifi. "Kama vile Mungu Baba aliviyotangulia kuwajua katika kutakaswa na roho, hata mkapata kutii na kunyuniziwa damu ya Yesu. Neema na amani na ziongezwe kwetu" (1 Petro 1:2). Wakristo wanahitaji ukombozi.

## 6. Jambo unaloweza kufanya

Shetani alipowashawishi Adamu na Hawa wafanye dhambi, alipata nafasi ya kuwatawala, na kuwatawala wanadamu wote. Ana nguvu kuliko binadamu wa kawaida. Dhambi isiposhughulikwa. Shetani anakuwa mtawala. Yesu alichukua dhambi zetu pale msalabani akalipa adhabu ya mwisho. Tukiujua ukweli huo na kuwa watii, tutakuwa huru mbali na Shetani na pepo.

Ukombozi haumaanishi kila wakati kukemea kwa nguvu na kuwekewa mikono kichwani, ingawa hilo linawezekana na linatokea mara nydingi. Zipo njia nydingine ambazo kwazo sisi tunaweza kukombolewa.

a. **Uwe mwaminifu.** Ungama dhambi zako. Enenda katika uaminifu na ukweli kwa gharama yoyote. Unaposema uongo unamfanya Shetani awe baba yako.

b. **Kataa** kuwa na uhusiano au mawasiliano yoyote ya kipepo uliyokuwa nayo kama vile: muziki, picha au maandishi yenye kutia ashiki (ponografia), televisheni, cinema, madawa ya kulevyaa, ushirikina, uaguzi, kupiga ramli, ubashiri, michezo ya kadi (karata) na kadhalika.

c. **Kataa** uhusiano wowote wa kiukoo unaoweza kutumiwa kueneza laana. Tunaweza kuwa na heshima kwa ndugu zetu katika ukoo bila kupokeea laana zao.

d. **Kaa karibu na Yesu** kwa njia ya maombi, Neno lake, marafiki wazuri na washirika wa kanisa. Hakikisha moyo wako umejaa mambo ya kiroho. Moyo wako ni uwanja wa mapambano.

e. **Uwe tayari kukombolewa kwa njia yoyote ile anayotaka Mungu.** Uwe na haja ya kuwa huru. Usimuwekee mipaka Mungu. Anazo njia nyingi za kukuweka huru. Kazi yake ni kukuweka huru (Luka 4).

f. **Mara nyininge watu huwekwa huru mbali na pepo** lakini hawajishibishi kwa Neno la Mungu na pia hawaishi maisha matakatifu. Kwa njia hiyo pepo huwarudia tena watu hao na hali zao huwa mbaya sana. Ni vizuri kupata ushauri wa kiroho baada ya kukombolewa. “Pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika; asipoona, husema, nitairudia nyumba yangu niliyotoka. Hata afikapo, akaona imefagiwa na kupambwa, ndipo huenda akachukua pepo wengine saba, walio waovu kuliko yeye mwenyewe, wakaingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza” (Luka 11:24-26).

**Hata hivyo, kuna njia ya salama na ya kiutendaji ya kuwekwa huru.** Neno la Yesu liliwatoa pepo katika Mathayo 8:16. Linaweza kufanya vivyo hivyo kwa ajili yako leo. Mimi binafsi nimeshuhudia njia hiyo ikifanya kazi. Kama ukijaza maji kwenye ndoo kabla ya kuyamwaga maji yaliyokuwemo, hakuna hatari ya kuwa na nafasi tupu itakayokaliwa na kitu kingine. Kwa sababu hiyo kama Neno la Mungu likijaa ndani yako, siyo tu kwamba pepo ~~watatoka~~, bali pia hakutakuwa na nafasi iliyoachwa wazi ya wao kurudi.

“Hata kulipokuwa ~~jioni~~ wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote ~~waliokuwa~~ hawawezi” (Mathayo 8:16). Kujaza Neno ndani yako kutawatoa pepo katika maisha yako.

**Ningependa kumualika kila msomaji** ~~akubaki~~ sasa kutumia njia hii. Hata kama huamini kwamba una tatizo lolote, huwezi kujua kwa uhakika.

**Fanya hivi.** Dhamiria moyoni mwako kwamba Neno la Mungu lijae kwa wingi ndani yako na kufurika. Na hapo sasa unaweza kulimimina Neno kwa njia yoyote unayopenda. Soma Biblia, sikiliza kanda za Neno la Mungu, kariri Maandiko, yaweke mdomoni mwako, yatafakari mchana na usiku. Littii Neno. Tenda yale ambayo limesema. Neno litatoo nje kila roho katika maisha yako isiyo takatifu.

g. **Ujazwe Roho Mtakatifu** ili uwe na nguvu ya kushinda (Matendo ya Mitume 1:8).

h. **Yesu alitupatia nguvu na mamlaka ya kutoa pepo** (Marko 16:17).

i. **Tunaweza kuwagundua pepo katika maisha yetu tukikaa karibu na Yesu.** Hata hivyo sio kwamba mabaya yote na magonjwa yote yanatokana na pepo, la hasha. Ugonjwa unaweza kusababishwa na matatizo ya kimaumbile

au masuala ya kimaisha. Mwenendo mbaya unaweza kuwa “mwili” wetu. Hata hivyo kama matatizo haya yasipotatuliwa yanaweza kuwa mlango wa kuingilia pepo. Tunapaswa kujihadhari na mwenendo mbaya, tabia tusizoweza kuzishinda, tamaa mbaya, hofu na hisia za kukandamizwa. Usiruhusu hali ya huzuni au mfadhaiko iendelee bila kupata msaada. Usikubali kutawaliwa na hisia za kuijua, uharibifu au mauaji. Wala usifice hisia za ubasha na zinaa. Tafuta msaada!

## 7. Mungu alimharibu Ibilisi

**Inamaanisha nini tunaposema Mungu alimharibu Ibilisi? Ni kwa vipi damu ya Yesu inatupatia nguvu?**

“Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, ye ye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu ye ye aliye kuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa” (Waebraania 2:14,15).

“Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, **wala mauti haimtawali tena.** Maana kwa kule kufa kwake, alifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu. Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu” (Warumi 6:8-11).

Mistari hiyo inasema kwamba Shetani “aliharibiwa.” Hiyo inamaanisha nini hasa? Inaonekana anazunguka zunguka akifanya kazi ya kuwaharibu wengine.

**Kuharibu maana yake ni kufanya nguvu za Shetani ziwe dhaifu - zisifanye kazi.** Yesu alitanyaue hivyo? Ibilisi bado anazunguka zunguka akiwaharibu wengine. Yesu alipofufuka alikuwa mzaliwa wa kwanza wa jamii mpya kabisa. Yesu aliweka utu mpya ndani yako siku ulipozaliwa mara ya pili. Utu huu mpya uko juu kabisa kuliko pepo na msahetani. Walikwisha ua jamii ya kwanza ya Adamu, katika Yesu pale msalabani. Shetani na pepo hawana kabisa mamlaka juu ya jamii hii mpya, wanachowezza kufanya tu ni kutuambia uongo. Yesu alipofufuka, pepo hawakuwa na nguvu tena juu yake. Aliweka maisha hayo ndani yako.

**Neno kuharibu limeelezwa katika Itifaki ya Strong kama ifuatavyo:**

- 1) kugeuza kitu kisifanye kazi, kikose kazi, kilegee, kisitumike.
- 1a) kumfanya mtu au kitu kisiwe na ufanisi tena.
- 1b) kunyang’anya nguvu, uwezo wa kuathiri na mamlaka

**Ufuataao ni mfano wa kuchekesha lakini unaweza kutusaidia  
kukumbuka na kupata picha inayoelezea maana ya neno “kuharibu”**

Hebu jifanye kuwa paka. Sasa mbwa mkubwa anayemuwakilisha Shetani anakunyanyasa, na kukufanya ukimbi kimbie tu na kujificha. Anaiba chakula chako na hata kuharibu mahali ulipojificha. Hatimaye mbwa huyu anakuua.

Kisha kwa ghafla, kwa njia ya muujiza, wewe, paka, unafuliwa kutoka kwa wafu. Safari hii wewe sio paka tena. Umegeuka kuwa simba! Sasa mbwa yule yule anakuja kwako, anakuangalia halafu anakimbia kwa sababu anajua unaweza kumuua! Mbwa ameharibiwa (amegeuzwa asifanye kazi, amekosa kazi, amelegea, hatumiki, hana ufanisi, amenyang'anywa nguvu, uwezo wa kuathiri na mamlaka)!

**Hebu jaribu kuwaza sasa kwamba mbwa yule amepanga mpango fulani.** Anakuja kwako na kukushawishi uamini kwamba wewe bado ni paka hujawa simba kweli kweli. Itakuwaje sasa mbwa huyo akifaalu kukufanya uishi na kutenda mambo kama paka? Hivyo ndivyo mbwa Shetani anavyofanya kwa Wakristo wengi.

**Jaribu kuwaza tena** kwamba Yesu alikuwa “paka” yule aliyekufa. Lakini muda mfupi kabla ya kufa kwake alipata “ujauzito” pamoja na wewe na mimi katika Bustani ya Gethsemane. Alipokufa na kufufuka, akawa mzaliwa wa kwanza katika wafu. Tunapozaliwa mara ya pili, tunakuwa pia simba.

“Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote” (Wakolosai 1:18).

**Tunahitaji kila wakati kusoma Neno na kumtazama Yesu** ili tuweze kuitunza kweli hiyo katika mioyo yetu. Tukiacha kufanya hivyo, tutachukuliwa upesi sana na uehonge wa dunia hii na kisha tunaweza kudhurika.

## 8. Kumjua Yesu ndipo jambo muhimu

“Si kila mtu aniambiaye, Bwana Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, na kufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!” (Mathayo 7:21-23)

**Maombi : Yaseme maneno haya kwa sauti kila wakati;**

Yesu nakukiri kuwa bwana na mwokozi wangu. Naamini ulikuja duniani kama Mungu katika mwili, na kwamba ulikufa mmsalabani na kuchukua nafasi ya maisha yangu ya dhambi. Asante kwa kunipa uzima wa milele .

Nakushukuru kwa ajili ya neema na rehema. Nimetambua kwamba sikuwa na chochote kizuri ndani yangu sio hata imani niliyokuwa nayo katika dini.

Sasa ninakiri dhambi zangu zote ambazo ninatambua, (Yataje kwa sauti). Asantre kwa kuondoa dhambi hizo, ninapozikiri na kutubu, na akugeuka kutoka katika njia zangu za kale.

Ninawasamehea wote ambao wamenikataa, walionitumia vibaya, walionitendea maovu na kunikosea kwa njia yoyote kubwa au ndogo. Kwa sasa ninavunja uhusiano wote na kushikamana kwa nafsi ambao namekuwa naoo na watu wasiomcha Mungu pamoja na dini za uongo na ushirikina. Kwa sasa ninazungumzia nguvu zote za kiroho amazo zime kita mizizi katika maisha yangu kupitia uhusiano ambazo sio za kiungu zinawache katika jina la Yesu.

Nashukuru kwa kuchukua laana zangu zote ambazo niliziridhi pamoja na zile za kujilettea. Asante kwa kujitolea kwa njia hii ya ajabu kw ajili yangu. Ninaikubali na kuiamini ijapokuwa sita weza kuoona na kuihisi kwa sasa., Ninaamini neno lako kama kweli, na kweli hiyo ninaiamini na kukutegemea wewe.

Nijaze sasa na roho wako mtakatifu ili maisha yangu iweze kuwa maisha ya mazungumzo ya ndani ya kweli na wewe. Nakukabidhi maisha yangu, mwili wangu, nafsi yangu na roho yangu. Kila siku nitatoa maisha yangu kama dhabiu iliyo hai, kulingana na Warumi 12.

Bwana ninajua kwamba kudumu inamaanisha kuishi na kutulia ndani. Ninajua neno lako litafanya upya ~~nia~~ yangu kila siku na hiyo ndiyo nahitaji.

Ninakushukuru bwana wangu mpendwa

Amina

### **Sura ya 11 - Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ubatizo katika Roho Mtakatifu**

Katika Luka 3:16 Yohana Mbatizaji alisema, "...mimi nawabatiza kwa maji, lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; ye ye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto."

**Waamini wengi hawatambui baadhi ya mambo muhimu** ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika Yohana sura ya 14, 15 na 16.

Alifahamu kwamba atauawa na kwamba atafufuka. Alijua pia kwamba atarudi tena kwa Baba lakini atamtuma Roho Mtakatifu kuchukua nafasi yake.

**Aliyasema haya yafuatayo akijua jinsi watakavyojisikia hawana baba** wasipouona uwepo wake. “Sitawaacha ninyi yatima [bila baba]; naja kwenu” (Yohana 14:18).

**Aliwaambia kabla hajapaa mbinguni** kwamba watajazwa Roho Mtakatifu. “Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache (Matendo ya Mitume 1:5). “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo ya Mitume 1:8).

**Aliwaambia wasiogope ye ye atakapoondoka.** Aliwaeleza kwamba Roho Mtakatifu atachukua nafasi yake na kumfanya ye ye (Yesu, Mungu adhihirike katikati yao. Soma maneno ambayo Yesu aliwaambia katika Yohana 14:16-26).

**Yesu aliwaambia kwamba Roho Mtakatifu atamdhahirisha  
Yesu katikati yao.**

**Naamini hili ndilo lengo kuu la Ubatizo katika Roho  
Mtakatifu**

“Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, ye ye atanishuhudia” (Yohana 15:26).

“Lakini mimi nawaambia ilioo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi misipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu” (Yohana 16:7).

**Yesu aliwaambia watu wake kwamba atakuja upesi.** Na kweli alikuja! Alikuja kwa njia ya Roho Mtakatifu Roho Mtakatifu na Yesu siyo watu tofauti, ni wamoja ila tu katika sura tofauti. Roho Mtakatifu huweza kuishi ndani ya wanadamu, wakati ambapo Yesu alikuwa katika mwili mmoja tu.

**Wanafunzi wa Yesu walipata uzoefu wa mambo mawili kuhusu Roho Mtakatifu.** Wanafunzi wale wa kwanza walimpokea Roho Mtakatifu wa Yesu aliyefufuka katika Yohana 20:22. Hata hivyo wanafunzi hao hao hawakuweza kuona badiliko lolote la tabia hadi walipompokea Roho Mtakatifu wa Kristo aliyepaa mbinguni, siku ya Pentekoste katika Matendo ya Mitume sura ya 2.

**A. Jumapili ya Ufufuo, Yohana 20:22.**

**Kristo aliyefufuka.**

**Katika Roho ya uvuvio.**

**Matokeo yalikuwa uzima.**

**B. Jumapili ya Pentekoste, Matendo ya Mitume 2:4.**

**Kristo aliyepaa mbinguni na kutukuzwa.  
Roho aliyemiminwa.  
Matokeo yalikuwa nguvu.**

**Lile kundi la watu 120 katika Matendo ya Mitume sura ya 2** liliachia na kuzama katika uwepo wa Mungu. Walitumia muda na kuongea maneno ya urafiki wa karibu. Walipokea nguvu iliyobadilisha maisha yao, nguvu ya kushuhudia, nguvu ya kupokea mahitaji yao yote, nguvu ya kueneza ufalme wa Mungu katika maeneo mengine na nguvu ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu na ushirika na Kristo aliyetukuzwa, kila siku.

**Yesu sio tena mtu anayetembea juu ya Bahari ya Galilaya**, wala sio mtu anayeteseka msalabani, na wala sio mtu aliyefufuka tu. Sasa yuko tofauti! **Hakuna mwanadamu aliyemuona Yesu katika hali hii**, isipokuwa Yohana katika kisiwa cha Patmo kama ilivoandikwa katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana. Soma Ufunuo wa Yohana sura ya 1.

**Wanafunzi wa Yesu walipata uzoefu wa kitu fulani** siku ile ya Pentekoste, kitu ambacho sisi sote tunahitaji kukipata. Yesu aliporudi mbinguni katika Matendo ya Mitume sura ya 1, alichukua nafasi mpya kuwa Kristo aliyepaa, na sio tu Kristo aliyefufuka. Yesu aliondoka duniani katika umbo la aliyefufuka, lakini alirudi tena katika Roho Mtakatifu akiwa mwenye nguvu zaidi, aliyepaa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu na aliyetukuzwa.

**Angalia, wanafunzi wake hawakuhuzunika** katika Matendo ya Mitume sura ya 1-3 kama walivyofanya katika kitabu cha Yohana aliposulabiwa. Wakati huu, alipoondoka, waliliamini neno alilowaahidi kwamba atarudi ipesi katika nafsi nytingine. Na hazikupita siku nyngi baada ya yeye kuondoka, alirudi tena kama Roho Mtakatifu, na walijazwa. Kisha waliendelea kuishi maisha yao wakiwa na ushirika na Yesu kana kwamba alikuwapo pamoja nao (Alikuwa panoja nao).

**Kubatizwa maana yake kuzamishwa.** Kwanza tulibatizwa kwa maji na sasa kwa moto. Moto ni uwepo wake. Tunapobatizwa katika maji tunakuwa tumekufa, tumeabishwa, lakini maji hayaingii ndani yetu na kutuua kabisa. Ni kwa nje tu. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni moto wa Mungu unaingia ndani yetu. Ni chaguo letu. Tunaweza kuchagua kiburi chetu kitawale badala ya kuwa na uwepo wake au badala ya yeye kututawala. Lakini yeye anataka kuteketeza utu wetu wa kale kwa moto. Mungu alimuahidi Nuhu kwamba maji hayatakuwapo tena, bali moto tu. Pepo huharibiwa na moto siyo maji.


**Je, tunahitaji kujazwa zaidi ya mara moja?** Baadhi ya madhehebu wanapinga jambo hili na kukosa ukweli. Sisi sio kama bilauri inayojazwa maji kwa kutumia gudulia au lagi. Kama hii ingekuwa kweli labda tungehitaji kujazwa tena na tena kwa sababu kuna uwezekano wa kuvuja.

**Neno la Mungu katika Yohana 15 linasema kwamba tumeungana na Yesu** kama tawi la mzabibu. Suala muhimu siyo kujazwa mara kwa mara, bali ni kukaa ndani yake wakati wote. Utomvu ndani ya mzabibu unawakilisha Roho Mtakatifu. Yesu ni mzabibu na sisi ni matawi. Tunahitaji kukaa ndani ya

mzabibu. Yesu anasema kwamba kutii Neno lake ndilo jambo linalotuwezesha kukaa ndani yake wakati wote. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni kufurikwa na uwepo wa Mungu tunapokuwa tumeunganishwa na Yeye kama mzabibu na tawi. Utomvu wake hutiririka ndani yetu, na hivyo tunaendelea kuungana na Yeye tukikaa ndani yake.

Tunakuwa tumeunganishwa  
Tunapompokea Roho Mtakatifu  
Na kumfanya Yesu kuwa Bwana

Tunapoja zwa Roho Mtakatifu,  
kizuizi kinaondolewa na maisha  
kamili ya Yesu hutiririka ndani  
yetu



Mzabibu ni Yesu

*Kiasi ganjua ujazo kinatosha?* Neno la Mungu katika Luka 6:45b linasema hivi: "Kwa kuwemtuu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake." Mimi binafsi napenda waze hili kwamba Roho Mtakatifu anatiririka kutoka katika kinywa changu akiniambla kwamba nimejazwa!

**Kumekuwa na utatanishi na matibazo mengi** kuhusu Ubatizo katika Roho Mtakatifu. Baadhi ya watu husema kuwa karama za Roho ndilo jambo muhimu na wengine husema kwamba jambo muhimu ni kunena kwa lugha. Na wengine nao wanasema kwamba ubatizo ni kwa ajili ya huduma, na kwamba kama kweli tunahitaji kumtumikia Yesu na kushuhudia kwa nguvu za Mungu, tunahitaji kujazwa Roho Mtakatifu. Hawajakosea, wote wana sababu nzuri, lakini siamini kwamba wamegusa kusudi la msingi la ujazo wa Roho Mtakatifu.

#### Vipi kuhusu karama za Roho?

Ninaona kwamba ni vizuri tuliache suala la utoaji wa karama kwa mtoaji mwenyewe. Mimi binafsi nimekuwa na karama nyingi zikitenda kazi katika maisha yangu mara kwa mara, lakini siyo zote.

**Ninaamini kunena kwa lugha** kwamba ni karama muhimu na ya thamani. Mungu huitumia sio tu katika huduma inayofanyika katika kundi la watu, bali pia hutawala miyo yetu kwa faida yake. Yakobo alisema kwamba ulimi ni kama usukani

mdogo sana unaoongoza merikebu yote. Kama unataka kumpa Yesu usukani wa maisha yako, mpe ulimi wako. Kuna mafundisho kamili juu ya jambo hili katika mtaala wa ISOB unaoitwa “Roho Mtakatifu na ulimi.”

**Sio vizuri watu** waliopokea karama kuwafanya wale ambao hawajapokea wajisikie kana kwamba wamefanya kosa fulani. Na pia sio vizuri kwa watu ambao hawajapokea karama kuwahukumu walio nazo. Yesu, katika Mathayo 12:31, anaonyesha wazi kwamba kukufuru kazi anazofifanya Roho Mtakatifu ni njia ya uhakika ya kukosa kupokea baraka hizo katika maisha yako mwenyewe. Kumkufuru Roho Mtakatifu ni kusema kwamba jambo fulani halitokani au halijafanywa na Roho Mtakatifu wakati ni kweli jambo hilo limefanywa na Roho Mtakatifu. Kama hunu uhakika, sawa, lakini uwe mwangalifu usiseme kinyume na jambo hilo isipokuwa tu kama una uhakika kabisa na unao uthibitisho kwamba jambo fulani ni la kishetani. Ni vizuri ujihadhari vinginevyo utakuja kuilaumu!

**Yesu anawezaje kutimiza yote aliyotuahidi asipodhahirika kwetu? Roho Mtakatifu humdahirisha Yesu kwetu ili aweze kufanya yale yaliyoahidiwa katika Isaya 61.**

**Mungu anataka kutuweka huru mbali na utumwa wa aina mbalimbali.** Hata hivyo, uhuru sio lengo kuu. Lengo kuu ni kutupatia uhuru ili tuweze kuingia katika uwepo wake na kuwa na ushirika naye, jambo ambalo litatufanya tuzae matunda kwa ajili ya maisha yetu na kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

1. Uhuru kutoka  
katika utumwa



2. Kufurahia Uwepo wake na  
kuzaa matunda

Katika kijapu cha Kutoka, Mungu alimtumia Musa kuwatoa watu wake Israeli katika utumwa wa Misri na Farao. “Wape watu wangu ruhusa waende, ili kunifanyia sikukuu jangwani” (Kutoka 5:1b). Uhuru kutoka Misri halikuwa suala kubwa kito muhimu kwa Mungu ni “sikukuu jangwani.” Au kwa maneno mengine, ushirika pamoja naye katika uwepo wake.

1. Uhuru kutoka  
katika utumwa

**Yesu alidondo Isaya 61 katika Luka 4:18** wakati alipotangaza kusudi la huduma yake. Isaya 61 inaanza na maneno anayosema Yesu kwamba Roho ya Bwana MUNGU amemtia mafuta awahubiri wanyenyekevu habari njema; amemtuma awagange waliovunjika moyo. Yesu anatangaza uhuru kwa mateka, anafungua magereza kwa wale waliofungwa, na kutangaza “Mwaka wa Bwana uliokubaliwa” au “Mwaka wa jubili” (wakati ambapo watumwa huwekwa huru). Anaendelea kuorodhesha mambo mengine mengi yatakayofanywa na huduma yake.

**Anasema kwamba wafungwa hawa na wanyenyekevu watabadilishwa** na kuwa miti ya haki, watakuwa na nguvu na pia watampendeza Mungu. Anasema

kwamba hawatakuwa tena na roho nzito kwa sababu ya maombolezo bali watajazwa furaha.

**Kisha anasema kwamba watajenga upya mahali palipoharibiwa.** Kwa maneno mengine maisha yao yaliyoharibiwa yatajengwa upya, kama Nehemia (ambaye jina lake linamaanisha mfariji au Roho Mtakatifu) aliyejenga upya kuta za Yerusalemu zilizokuwa zimebomoka. Vile vile, alisema kwamba mahitaji yao yote yatasughulikiwa na kwamba watakuwa makuhani wa Mungu, au wawakilishi wake binafsi. Kisha na wao watawakomboa wengine na kuwaweka huru.

**Kwa muhtasari Isaya 61** inaeleza kwamba Yesu atawabadilisha watu kutoka katika hali ya kuwa wafungwa hadi kuwa makuhani kwa njia ya Roho Mtakatifu. Hivi ndivyo tulivyosema katika Sura ya 1 ya kitabu hiki, kwamba tutaza matunda katika maeneo yote matatu ya maisha yetu; tabia zetu, mahitaji yetu na huduma zetu kwa wengine. Kutoka hali ya kuwa wafungwa hadi kuwa makuhani.

**“Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu;** kwa sababu BWANA amenitia mafuta:

1. niwahubiri wanyenyekevu habari njema,
2. amenitura ili kuwaganga waliovunjika moyo,
3. kuwatangazia mateka uhuru wao,
4. na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao” (Isaya 61:1).
5. “kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa na
6. siku ya kisasi cha Mungu wetu;
7. kuwafariji wote waliao;” (Isaya 61:2).
8. “kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu,
9. mafuta ya furaha badala ya maombolezo,
10. vazi la sifa badala ya roho nzito;
11. wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA , ili atukuzwe”(Isaya 61:3).  
*(Handwritten note: "Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa na siku ya kisasi cha Mungu wetu; mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA , ili atukuzwe")*
12. “Na watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipoikuwa ukiwa zamani, watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi” (Isaya 61:4).
13. “Na wageni watasimama na kujisifi mukundi yenu, na watu wa kabile nyingine watakuwa wakulima wenu, na watunzaji wa mizizi yu yenu” (Isaya 61:5).
14. “Bali ninyi mtaitwa makuhani wa BWANA, watu watwai teni wahudumu wa Mungu wetu; mtakula utajiri wa mataifa, na kujisifia utukufu ‘wao” (Isaya 61:6).
15. “Badala ya aibu yenu mtapata maradufu, na badala ya fedheha watafurahia sehemu yao; basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele” (Isaya 61:7).

Alimtuma mfariji mwengine, Roho Mtakatifu, achukue nafasi yake. Roho Mtakatifu ndiye sasa anayesimamia na kutoa ahadi hizi kwetu. Hatuwezi kupata baraka zote hizo tusipokuwa na ushirika na Yesu kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**Tunahitaji Yesu adhihirike kwetu.** Tunahitaji kuungana naye ili tupate yote aliyoyaahidi katika Isaya 61. Mambo yanapokwenda kombo katika maisha yetu, tukimsikia Yesu anasema nasi, kila kitu kitakuwa sawasawa!

**Kama tu wafungwa, na kama tu wanyenyekevu,** waliovunjika moyo na kupigwa, hatuhitaji kungojea twende mbinguni ili tupate msaada; tunahitaji msaada huo SASA! Tunaweza kuupata sasa katika maisha haya, lakini lazima tuwe na ushirika na Mungu. Anahitaji kujidahirisha kwetu. Anahitaji kuwa zaidi ya dini, zaidi ya mafundisho ya dhehebu letu, zaidi ya

maneno ya Maandiko Matakati (kama jinsi yalivyo muhimu). Tunahitaji kuwa na ushirika na Yesu aliye hai kama jinsi wanafunzi wake walivyo kuwa wakati Yesu alipokuwa duniani, na kama jinsi walivyo endelea kuwa na ushirika naye hata baada ya yeze kupaa mbinguni, kama tunavyoona katika Matendo ya Mitume.

**Neno la Mungu katika Waefeso 3:18-19 linasema, “ili mpate kufahamu** pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwangi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.”

**Mungu alidhahirika kwa Yakobo katika Mwanzo sura ya 28.** Yakobo alionja uwepo wa Mungu na hakupenda kuuachia! Maneno ya Mungu katika Mwanzo sura ya 28 mstari wa 10-17 yanalezea jinsi Yakobo alivyo sika uwepo wa Mungu wakati alipoota ndoto kuhusu ngazi inayounganisha mbingu na nchi. Asubuhi iliyofuata, Yakobo aliamka na kujenga madhabahu pale na kuита Betheli, yaani nyumba ya Mungu. Alikuwa amekamatwa kikamilifu na hali nzuri ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu. Mungu alidhahirika kwake. Yakobo alikuwa kama wewe na mimi. Alihitaji mabadiliko makubwa. Utu wake wa asili ulikuwa umeharibika. Ili kumbadilisha Yakobo, Mungu alimvuta awe na urafiki wa karibu pamoja naye. Mungu akajidhahirisha kwa Yakobo. Yakobo akampenda sana Mungu, na kumfuata maisha yake yote. Baadaye, walipokuwa wakitembea pamoja, Yakobo alibadilishwa kutoka Yakobo na kuwa Israeli.

**Kabla Yesu hajaingia katika maisha yangu, nilikuwa kweli mfungwa wa kiroho.** Kulikuwa na pepo waliokuwa wakitawala maisha yangu. Nilipomuona Yesu katika kitabu cha Ufuno wa Yohana kama Kristo aliyepaa mbinguni, mshindi na mkombozi, nikapatu kuwa mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Hii ilitokea tarehe 26 mwesi Agosti, mwaka 1979. Yesu alidhahirika wazi kwango kama ninavyo muona jirani yangu. Alisema na mimi na kunisikiliza. Alikuwa pamoja nami katika maumivu na shida zangu. Watu waliponidhifikasi, alinifariji. Watu walipojaribu kunifanya mateka, alinifundisha kweli iliyoniweka huru. Baada ya muda mfupi, kama Isaya anavyosema katika sura 10:27, nira yangu (ya kukandamizwa na kuteseka) shingoni mwangu iliharibwa, kwa sababu ya kutiwa mafuta.

**Kidogo kidogo,** Yesu aliniweka huru mbali na pepo waliokuwa wakinathiri na kunishika na pia wala walijokuwa wamefanya mwili wangu kuwa “nyumba” yao. Nilipofanya ushirika na Yesu ~~katika Neno na kwa njia ya maombi, niliweza kulia bila kujizuia, machozi na makamasi yalinitoka sana~~ ~~Tuna~~ katika Luka 11:24 kwamba pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji (mahaali palipo) akitafuta mahali pa kupumzika; asipoona hutafuta kurudi tena mahali palipo na “maji”. Mahali palipo na maji, nyumba yao ya kwanza, ni mtu. Na sehemu kubwa ya mwili wa mtu ni maji. Ukombozi ~~ni~~ mliendelea kila wiki kwa kipindi cha miezi kadhaa, au hata miaka - siwezi kukumbuka.

**Siku zilivyoendelea,** niliwekwa huru mbali na pepo ~~walio~~ nifanya mateka. Tabia yangu ikaanza kufanana na tabia ya Yesu. Nikaanza kupata mahitaji yangu. Mungu akanipa chaguo lake la mke na familia.

**Baada ya miaka mingi ya nidhamu,** amenifanya kuwa mhudumu wa Mungu, kama alivyoahidi katika Isaya 61. Mungu alimtumia Roho Mtakatifu kuleta mabadiliko haya katika maisha yangu. Naye Roho Mtakatifu akamdhahirisha Yesu kwango. Yesu hakufanya hivyo, bali Roho Mtakatifu ndani yangu alieyondoa kila kitu kisicho cha Mungu.

2. Kufurahia uwepo  
wake na kuzaa  
matunda.

**Baada ya uhuru kutoka katika utumwa, Mungu anataka tupate  
uzoefu wa uwepo wake na Ufalme wake**

**Roho Mtakatifu hufanya Ufalme wa Mungu udhahirike kwetu katika  
maisha haya. Waschranje 12**

Maandiko ya wazo kuu au dhamira ya Sehemu hii ya Pili yanatoka katika Waebrania 12. Sura hii inazungumzia kupiga mbio, lakini pia inazungumzia kuweka kando kila mzigo na dhambi. “Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile itizingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu” (Waebrania 12:1).

**Sura hii inaendelea kuzungumzia juu ya ukweli wa mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni**, uitwao pia mlima Sayuni. Inavyoonekana, kuweka kando dhambi na kila mzigo, na kufuata mengine yote yaliyoelezwa katika waebrania 12 ni kuufanya ufalme wa Mungu udhihirike katika maisha yetu.

**Hebu tuchunguze yale aliyozasema mwandishi wa kitabu hicho cha Waebrania** kwa watu wale kuhusu kupiga mbio, kuweka kando kila mzigo mzito na dhambi na ufalme wa Mungu kudhihirika kwetu.

1. Katika Waebrania 12:2-4 tunaambiya kwamba tunapaswa **kusimama kwa uvumilivu**, bila kuchoka. Tunapaswa kuvumilia mapingamizi, kutokuelewka na mateso. Kusimama kwa uvumilivu pamoja na Yesu ni kuotesha mbegu miyoni mwetu kwa ajili ya kuzaa matunda.

2. Katika Waebrania 12:5-11 tunaambiya kwamba Mungu **ataturudi**, sio kutupiga, bali kutusahihihsa kama wana kwa upendo na kwa faida yetu wenywewe. Ni kweli tunahitaji kurudiwa na Mungu. Kuna mambo mengine tusiyoyaona.

Yakobo alikowea na ubinaksi tena mkaidi. Mungu alimrudi kwa njia ya mazingira hadi jina lake lilipobadilishwe kutoka Yakobo na kuwa Israeli, na kutoka mlaghai kuwa mtu anayeshindana na Mungu.

Tunahitaji kuyaona mazingira yetu kuwa amepangwa na Mungu ili kwamba tunapopita katika mazingira hayo, mwenendo weusi orodhishive ufanane na wake. Hii haina maana kwamba Mungu huleta mazingira au mambo mabaya katika marsha yetu. La hasha; Shetani ndiye anayefanya hivyo. Lakini, unaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu anayatumia mazingira hayo kutufanya tufanane naye. Mungu hutumia Neno lake kulturudi, lakini kuna maeneo ya utu wetu wa kale yanayohitaji kwanza kupitia katika majaribu ili yasafishwe.

3. Katika Waebrania 12:12 na 13 tunatiwa moyo tusonge mbele wakati hali sio nzuri.

4. Katika Waebrania 12:14 tunaambiya tutafute kwa bidii amani na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.

5. Tunaambiya katika Waebrania 12:15-16 tusiipungukie neema ya Mungu na pia tuijepushe na uchungu. Tunaambiya pia tuisive kama Esau aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza na hakuweza tena kutubu.

6. **Sasa, hii hapa ni thawabu.** Soma Waebrania 12:18-29. Mmeufikilia mlima Sayuni, ufalme wa kiroho, Ufalme wa Mungu. Ni sasa, sio tu wakati ujao. Mungu anataka tuishi katika ufalme wa mbinguni, sasa hivi wakati bado tupo duniani. Tunaweza kuishi katika “zamani zijazo,” (Waebrania 6:5), lakini tunahitaji kwanza kujazwa Roho Mtakatifu. Anataja kwamba mlima Sayuni, au ufalme wa Mungu, una sifa kadhaa.

- a. **Kwanza, ni Mungu aliye hai.** Roho Mtakatifu anatuwezesha kuwa na ushirika na Mungu aliye hai sasa kwa sababu yupo hapa pamoja nasi.
- b. **Pili, ni Yerusalem wa mbinguni.** Roho Mtakatifu anatuwezesha kuishi katika ufalme wa Mungu, sasa.
- c. **Kisha, malaika wanatajwa.** Hatuhitaji sana kulenga macho yetu kwa malaika, lakini tunahitaji kujua kwamba wapo hapa ili kupigana vita kwa ajili yetu na wanafanya hivyo kwa Neno la Mungu.
- d. **Tumelifikia kanisa** la Mzaliwa wa kwanza, Yesu, wale walio raia wa mbinguni. Hii inatuonyesha kwamba tunapaswa kukaa katika kanisa zuri linaloamini Biblia na ambalo limejazwa Roho.
- e. **Mungu, Mwamuzi** anatajwa katika mstari wa 23. Ninafurahi kwamba Mungu ni mwamuzi wangu; hiyo inamfanya Mwokozi wangu awe pia mwamuzi wangu. Yeye anatufanya tuone makosa yetu ili tutubu na kushinda. Vile vile, Mungu ni hakimu wa adui yetu, Shetani. Amekwisha mhukumu Shetani. Mungu atakuhukumu wewe mwenye haki na kumhukumu pia Shetani katika kila eneo la maisha.
- f. Waebraania 12:23 inataja roho za watu wenye haki waliokwenda mbinguni. Siamini kwamba ninaweza kuwasiliana na roho za watakatifu waliotutangulia, lakini ninaamini kwamba wanatuona. Tunaonwa na kushangiliwa na wingu kubwa la mashahidi. Ushuhuda wa imani yao ndio tunaouona.
- g. Katika Waebraania 12:24 tunaambiwa kwamba tunaye **Yesu mijumbe** wa Agano la damu. Tunamshukuru Mungu kwa hili. Yesu sio tu kwamba anafanya agano la damu pamoja nasi, lakini pia alifufuliwa kutoka katika wafu ili awe mptanishi na mdhamini wa agano. Tunapofanya makosa, Yesu hutuwezesha kuungama na kutubu dhambi zetu na kisha hutupatanisha na Mungu. Ni mptanishi na wakili wetu. Anahakikisha kwamba tunashinda.
- h. Katika Waebraania 12:25 tunaonywa tusimkatae ye ye anenaye, vinginevyo hatutaokoka tukijiepusha na ye ye atuonyaye.
- i. Katika Waebraania 12:26-28 tunaambiwa kwamba **Mungu atatemeshwa** kila kitu mbinguni na duniani, in kwamba vile vitu vinavyotakiwa kuondolewa, viondolewe na vile ambavyo vimesimama imara, katika ufalme wa Mungu, vitashinda jaribu hilo na kuendelea kusimama imara.
- j. Mwisho, katika Waebraania 12:29 tunamjiwa kwamba **Mungu ni moto ulao.** Moto ulao ni Roho Mtakatifu. Amekuja kutukomboa kutoka katika yale yote yanayoweza kutetemeshwa, na pia kutoka katika masazo ya utu wa kale, mwili na hali ya dhambi.

### Tufanyeje ili tushirikiane na Mungu?

1. **Tunahitaji kuwa na njaa ya kuona Mungu akijidhihirisha kwetu.** Wale watu 120 orofani walikuwa baadhi tu ya watu ambao Yesu alikuwa amejidhihirisha kwao baada ya kufufuka. Kulikuwa na watu wapatao 500. Kitu gani kilitokea kwa hao wengine? Labda hawakuwa na njaa ya kutosha. Au labda walijivuna sana au huenda walikuwa wamefungwa na shughuli zao au na familia zao. Inawezekana pia walikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi watu wengine watakavyowafikiria. Kumbuka wale 120 walishutumiwa na kuchekwa.
2. **Tunahitaji kuwa na mizizi** katika Neno ili tuwe washindi. Agano la damu huondolewa kwa maneno na siyo damu. Neno likijaa kwa wingi ndani yako, utakuwa na damu nyingi pia, na pia maisha yako yatajaa tabia ya Kristo. Kwa jinsi hiyo dhambi zako zitaondolewa kwa wingi. Pepo hawatakuwa na athari kwako. Utajazwa Roho Mtakatifu. "Kwa kuwa ye

aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo” (Yohana 3:34).

**3. Tunahitaji kujiandaanukataliwa na ukoo wetu au dhehebu letu.** Katika Luka 12:49-52 imeandikwa hivi: “Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi? Lakini nina ubatizo unipasao kubatizwa, nami nina dhiki kama nini hata utimizwe! Je! Mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, La, sivyo, bali mafarakano. Kwa kuwa tokea sasa katika nyumba watakuwamo watu watano wamefarakana, watatu kwa wawili, wawili kwa watatu.”

**4. Tunahitaji kuwa wazi** kwa Yesu na kumwamini. Katika Luka 11:11-13 tunaambwa hivi: “Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawewe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?”

**5. Roho Mtakatifu kila wakati anahestimu toba.** Huonekana tunapotubu dhambi na kuyaacha mambo ya ulimwengu, kiburi na uvivu wetu. Katika Matendo ya Mitume 26:18 imeandikwa hivi, “uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekeaa nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekeaa Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi mionganii mwao waliotakaswa kwa imani ilio kwangu mimi.”

**6. Tunampokea Roho Mtakatifu kwa imani.** Imani katika nini? Yesu alizungumzia ujazo wa Roho Mtakatifu katika Yohana 7:38-39, “Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa **hajatukuzwa**.”

Kwa hiyo Yesu alihitaji **kutukuzwa** kwanza kabla hatujawa na imani ya kumpokea Roho Mtakatifu kama mafuriko ya mto ulio hai. Kutukuzwa maana yake nini? Kutukuzwa ni neno linalomaanisha kufunua au kuweka wazi kitu cha kweli. Ni kama mtu anayeondoa kitambaa kilichofunika sura ya kitu fulani na kuionyesha wazi sura hiyo kwa mara ya kwanza.

Katika Yohana 17:4-5 Yesu alimwomba Baba, akisema, “Mimi **nimekutukuzwa** duniani, hali nimeimaliza kazi ile ~~liloyonipa~~ niifanye. Na sasa, Baba, **unitukuze** mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa na pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako.” Yesu alimfunua Baba kwa watu aliotutana nao. Sasa ilikuwa zerau ya Baba kuionyesha Yesu alikuwa nani hasa.

**Yesu alitukuzwaje?** Kumbuka, kutukuzwa maana yake ni kuionyesha sura ya kweli au sura halisi ya mtu au kitu. Katika Luka 24:13-27 alikuwa akizungumzia na watu wawili katika njia ya kwenda Emau. Akasema, “Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika **utukufu** wake? Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe” (Luka 24:26,27). Kisha wale watu wawili walisisimka sana na walipowaona mitume 11 walianza kuwaambia yale ambayo Yesu ameyafunua. Ghafla Yesu aliyefufuka alitokeza katika mkutano huo akaanza kunena nao. “Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote nilyoandikiwa katika torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu” (Luka 24:44-46).

Aliwapa ufunuo au alijitukuzwa mwenyewe katika vitabu vya Musa, Zaburi na Manabii. Alikuwa akizungumzia vitabu vitano vya Musa, vitabu vya Manabii na Zaburi.

Hatimaye baada ya hayo, siku ya Pentekoste iliwadiwa wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu na moto!

**Alijitukuzwa mwenyewe katika vitabu vya Musa:**

**Katika Mwanzo** alijitukuza kama muumbaji. Alijionyesha mwenyewe kuwa muenezaji wa jamii mpya kwa njia ya agano la damu ili kuchukua nafasi ya jamii ya Adamu iliyoanguka dhambini.

**Katika Kutoka**, alijionyesha kama mtoa sheria na kama Kondoo wa Pasaka kwa ajili ya sheria zilizovunjwa. Yeye ndiye aigawanyaye bahari ya shamu ya maisha yetu na kutuo katika vifungo vya ulimwengu.

**Katika Mambo ya Walawi**, yeye ndiye aliyefanya agano la damu, na ndiye anayetuomba kwamba tuchukue msalaba wetu na kuishi katika utakatifu.

**Katika Hesabu**, yeye ndiye atupaye mahitaji yetu katika jangwa la maisha yetu; yeye ndiye mana yetu kutoka mbinguni na maji kutoka mwambani.

**Katika Kumbukumbu la Torati**, ni yeye anayetukomboa kutoka katika laana ya sheria.

### **Alijitukuza mwenyewe katika Zaburi:**

**Katika Zaburi**, ni mchungaji wetu tunayeweza kumtwika masumbufu yote ya mioyo yetu kwa unyofu bila kukemewa, kama Daudi alivyofanya.

### **Alijitukuza mwenyewe katika Manabii:**

**Katika Isaya** ni Mwokozi anayeteseka anayechukua dhambi na magonjwa yetu.

**Katika Yochi**, anaonyesha ahadi ya ubatizo katika Roho Mtakatifu. Hata hivyo kabla ya ahadi katika Yochi sura ya 2, alionyesha hali inayotakiwa ya kujiweka wakfu kabla ya kupokea ahadi hiyo.

**Aliwaonyesha pia** yale nifiyoyona nilipookoka na kujazwa Roho Mtakatifu wakati huo huo, katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana kama kili yoelezeza kabla katika kitabu cha Ezekiel na Danieli.

**Katika Ezekiel 37**, ni yeye anayeipa uhai mifupa yetu mikavu, kwa Roho Mtakatifu. Katika sura ya 38-39, anawashinda adui zetu. Katika sura ya 40-42 anatuonyesha hekalu la Mungu ili tujue kwamba tumekaribishwa kuwa na uhusiano wa karibu pamoja naye.

**Katika Ezekiel 43**, aliwaonyesha utukufu wa kiti chake cha enzi na maskani ambapo Mungu anakutana na mwanadamu kama katika Ufunuo wa Yohana 21. Katika sura ya 44-46 anatuomba tujiweke wakfu ili tuweze kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

**Katika Ezekiel 47**, kama katika Ufunuo wa Yohana 22, yeye ndiye anayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kusababisha mto utiririke kutoka ndani yetu hadi katika bahari ya chumvi ya wanadamu ili watu waweze kufanywa hai na Mungu.

**Katika Ezekiel 48:35** jina lake ni “BWANA yupo hapa,” katika Yerusalemu wa mbinguni akiishi na watu wake.

**Katika Danieli** sura ya 1-6 anajifunua mwenyewe kama anayetuomba tuwe ulimwenguni lakini tusiwe wa ulimwengu. Yupo pamoja nasi katika tanuru la moto na katika matundu ya simba ya maisha yetu.

**Katika Danieli** sura ya 7, anajionyesha mwenyewe kama mzee wa siku aliywapa watakatifu ushindi. Katika sura ya 8-9 vita vinafananishwa na vita katika Ufunuo wa Yohana.

**Katika Danieli 10:5**, Anaonyesha Kristo mshindi aliyepaa mbinguni kama katika Ufunuo wa Yohana sura 10 na 11 zinavyoonyesha vita zaidi.

**Danieli 12** inaelezea umuhimu wa kusimama, maana baadhi watachakazwa na adui. Sasa angalia Danieli 12:12. Watakaosimama imara hadi mwisho, watapata ushindi. Hivi ndivyo nilivoona nilipookoka na kujazwa Roho Mtakatifu wakati huo huo mwaka 1979!

**Katika Agano Jipyä**, Yesu alijifunua kama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Anaelezea ule utata katika Agano la Kale usemao kwamba Mungu ni mwenye rehema, husamehe dhambi lakini mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao na wana wa wana wao pia hata kizazi cha tatu na cha nne (Kutoka 34:6-7).

**Alijidhihirisha mwenyewe** kama Mwana wa Mungu, kama Neno la Mungu, kama Njia, Kweli na Uzima!

**Alijidhihirisha mwenyewe** kama Masihi atakayekuja mara ya pili kama **Mfalme mkuu katika kitu cha enzi**.

**Katika Yohana 14-16**, alijidhihirisha kama Roho Mtakatifu atakayekaa ndani ya wanafunzi wake.

**Katika Luka 24 na Matendo ya Mitume 1** Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuyaweka wakfu maisha yao na kungojea ahadi itimie. Hii ndiyo sehemu yetu: utii, kujiweka wakfu na kujachia.

**Maombi**. Bwana Yesu, Neno la Mungu linasema kwamba unahitaji kunijaza kwa Roho wako ili kwamba wewe na mimi tuzidi kuwa marafiki. Nina njaa ya kuwa na wewe na kuwa katika uwepo wako katika maisha yangu. Yesu, ninaliamini Neno lako. Ninakiri mbele zako kwamba ninahitaji kila ulicho nacho kwa ajili yangu. Njoo, Yesu, unibatize katika Roho Mtakatifu na moto. Niko wazi na niko tayari kupata moto katika maisha yangu. Nakataa na kutubu dhambi zote katika maisha yangu. Namsamehe kila mitu aliyenikosea. Najitoa kwako kuwa dhabihu ilioyai. Wewe ni mtawala wa maisha yangu. Navitoa kwako viungo vyangu vyote, kinywa changu, ulimi wangu, mikono yangu, migule masikio na macho.

Vichukue vyote!

## Kiambatisho A – Orodha ya Masomo ya ISOB

Orodha ya masomo ya ISOB yanayopatikana kwenye “CD ROM” kwa ajili ya Kompyuta za “Windows” au “Macintosh”

**Masomo 7 ya kwanza yameambatana na sauti.**

- **Kitabu cha Kukua au Kufa Sehemu ya 1**
    - 01. Kukua au Kufa Kuzaa Matunda
    - 02. Wafungwa katika Nchi ya Ahadi
    - 03. Mto Utiririkao – (liendelezwe kila siku)
    - 04. Mungu ni Nani
    - 05. Kuketi
    - 06. Kuenenda
    - 07. Kupinga
  - **Kitabu cha Kukua au Kufa Sehemu ya 2  
(Damu na Moto)**
    - 08. Nguvu ya Kupiga Mbio
    - 09. Msalaba
    - 10. Ukombozi – Pepo
    - 11. Ubatizo katika Roho Mtakatifu
- .....

#### **4 Mungu Ni Nani (somo moja moja)**

- 01. Kumjua Mungu wetu wa ajabu
  - 02. Utatu
  - 03. Mungu Baba
  - 04. Mungu Baba – 2
  - 05. Mungu ni wa agano
  - 06. Uzao Mtakatifu
  - 07. Uzao Mtakatifu – 2
  - 08. Yesu ni nani sasa?
  - 09. Sura ya Mungu
  - 10. Mungu Neno
  - 11. Mamlaka ya Neno la Mungu
  - 12. Ukamilifu wa Neno
  - 13. Utakaso Unaofanywa na Neno
  - 14. Kristo Mwamba
  - 15. Unabii wa Biblia –  
Jina la Yesu katika Agano la Kale
  - 16. Mungu Roho Mtakatifu
  - 17. Roho Mtakatifu na Lughaa
  - 18. Ubatizo katika Roho Mtakatifu
- 

#### **5 Kuketi Somo moja moja:**

- 01. Muhtasari wa Kuketi – Kuketi na Kristo
- 02. Neema
- 03. Utambulisho
- 04. Upendo Mkuu
- 05. Nilinunuliwa toka utumwani

- 06. Ukombozi**
  - 07. Nani alikuambia**
  - 08. Uponyaji wa Miili yetu**
  - 09. Mizizi**
  - 10. Ushindi juu ya Dhambi**
  - 11. Hofu**
  - 12. Hatia**
  - 13. Nguvu ya kumaliza mshindano – Msalaba**
- .....

## **6 Kuenenda**

- 01. Muhtasari wa kuenenda**
- 02. Kurudi nyuma**
- 03. Kijana Tajiri – Kuweka wakfu**
- 04. Kuwa na shughuli nyingi kwa ajili ya Mungu**
- 05. Imani**
- 06. Samehe**
- 07. Ulimwengu**
- 08. Ukweli/Zaka**
- 09. Ukweli wa Adhabu ya Kifo**
- 10. Ukweli**
- 11. Mamlaka**
- 12. Tubu**
- 13. Usomaji wa Biblia**
- 14. Mwenendo kwa Mtu aendaye Mbinguni**
- 15. Angalia Yasiyoonekana**
- 16. Utumishi**
- 17. Kuwatanguliza wengine**
- 18. Mheshimu kwa mwili/wako**
- 19. Mwitikie Mungu**
- 20. Linda moyo wako**
- 21. Zaka – Uchumi**
- 22. Maombi**
- 23. Utumie Urithi wako**
- 24. Enenda kwa Roho**
- 25. Kukubaliana**
- 26. Maneno Yako**
- 27. Ombo - Imani**
- 28. Kurudi Nyuma**
- 29. Rehema**
- 30. Uwe Mkweli**
- 31. Lawama**
- 32. Upendo**
- 33. bada**
- 34. Urafiki**
- 35. Sifa – Wimbo mpya**
- 36. Marafiki zako**
- 37. Ushirika na waaminio**

- 38. Ubatizo**
  - 39. Hukumu**
  - 40. Kuchezea Neema**
  - 41. Kufunga**
- 

## **7 Kupinga**

- 01. Muhtasari wa Kupinga – Kuzipinga hila za Shetani**
- 02. Damu ya Vita**
- 03. Chumba cha Mahakama**
- 04. Amani Iwepo**
- 05. Ufunuo**
- 06. Gombo**
- 07. Matatizo**
- 08. Imetiwa Mhuri**
- 09. Aketipo Shetani**
- 10. Siyo mapenzi yangu**
- 11. Shetani, pepo, mashetani, ukombozi**

**Mtaala wa ISOB na kazi za darasani**

**Uanafunzi wa Yesu/Uongozi III**

## **Kuwa Huru**

- 01 Kuwa Huru**
- 02 Majitu/Yanaizunguka Ahadi yako?**
- 02 Ukweli Mwingine**
- 04 Huzuni**
- 05 Uchawi**
- 06 Ushirika wa Wasioona Aibu**
- 07 Kuusisimua Mwili**
- 08 Upatanisho wa Mabaya I**
- 09 Upatanisho wa Mabaya II**
- 10 Upatanisho wa Mabaya III**
- 11 Mamlaka - Jumba Kubwa la Mfalme**
- 12 Makusudi ya Kujaribiwa**
- 13 Maono - Ndoto**
- 14 Huduma**
- 15 Mateso**
- 16 Mithali**
- 17 Kitabu cha Yohana**

**Mafundisho mengine ya ISOB**

**Mafundisho ya Biblia**

**Wokovu**

**Uumbaji - 1**

**Roho, Nafsi, Mwili**

**Unajuaje kwamba Biblia ni ya Kweli?  
Uumbaji - 2  
Roho Mtakatifu wa Milele**

**Timu Yenye Nguvu kwa watoto**

**Masomo 13 kutoka katika Kitabu cha Yohana kwa watoto  
(pamoja na katuni) (Kanda zinatolewa)**

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

**Kiambatisho B –Jinsi ya kuendelea katika ISOB  
(Masomo yote ya ISOB yanapatikana katika CD ROM)**

**1. Mahitaji ni yapi?**

Tunahitaji Neno na Roho Mtakatifu amdhihirishe Yesu kwetu . Tunahitaji uwepo wa Mungu, siyo tu kanisani, bali pia katika maisha yetu ya kila siku.

Tunamhitaji Mungu na Neno lake litusafishe na kutufanya wanafunzi wa Yesu. Tunahitaji njia ya kivitendo ya kubeba msalaba wetu kila siku na kumfuata Yeye.

Tunahitaji elimu ya Neno ili tushinde mambo magumu tutakayokutana nayo maishani.

Tunahitaji kuwa na uhusiano na wengine katika mwili wa Kristo, kama washauri na wanafunzi.

Tunahitaji kuufikia ulimwengu unaoangamia, na kuuruhusu uwepo wa Mungu utiririke kutoka kwetu hadi kwa watu wengine.

**Tunahitaji kuwapa mamilioni ya watu wanaokolewa kila siku pote ulimwenguni, mafundisho yaliyo wazi, rahisi kueleweka. Wanahitaji kujuua ukweli ili waweze kukua wasishindwe.**

## **2. ISOB**

Ni njia ya kuwfundisha wanafunzi wa Yesu na wahudumu kwa ajili ya Agizo Kuu.

Ni njia ya kuja katika uwepo wa Mungu kwa ajili yako mwenyewe.

Ni njia ya Mungu ya kufanya Neno na Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu wako.

Ni njia ya kujifunza jinsi ya kujilisha mwenyewe Neno la Mungu.

**Kulipata kwa wingi Neno la Mungu siyo tu suala la kuwa na nidhamu** katika kuisoma zaidi Biblia. ISOB itakupatia utaratibu mzuri wa kulifanya Neno la Mungu lihusike kabisa na wewe na pia liwe la kuvutia.

**3. ISOB siyo Shule hasa ya Biblia.** Inaweza kutumika kama mfumo wa kushauri, watu wanapojifunza pamoja au mtu anapojifunza mwenyewe. Dhana kamili ni kuwawezesha watu wasioweza kwenda Shule ya Biblia kuwa wanafunzi wa Yesu na viongozi. Ni njia rahisi ya kukua katika Bwana. Inaweza kufanyika nyumbani, kanisani, au sehemu yoyote nyingine Bwana atakayotoa. Maelezo haya yatafanua kwa undami jinsi mfumo huu unavyofanya kazi na hatua unazopaswa kuchukua ili kuanza. Maandiko ambayo kwayo Bwana ameianzisha kazi hii ni haya:

Bwana yanainoa neno lake; **Wana wake watangazao habari ni jeshi kubwa** (Zaburi 68:11)

Waefeso 4:11-16 "Naye alioa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; **kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya nadima itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;** hata na sisi sote tutakapoufikia umoja we imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeche katika yote, yeche aliye kichwa, Kristo. Katika yeche mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo."

Maandiko hayo yananiambia kwamba tunapaswa kuwajenga watakatifu (washauri na wanafunzi) ili waweze kuingia katika huduma.

## **4. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi kwa mwanafunzi mmoja mmoja:**

Kama wewe ni mwanafunzi binafsi, unaweza kutumia masomo haya kama upendavyo. Tunashauri utumie muhtasari wa mtaala.

## **5. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi mahali ambapo watu wanajifunza kwa pamoja:**

Baadhi ya viongozi wa ISOB hupendelea kuwa na vipindi vyta kujifunza Biblia katika kikundi tofauti na kuandikisha washauri. Kiongozi anachofanya tu ni kuwa na mahali pa

kukutania kila wiki na kisha hufundisha kila somo la ISOB kwa kufuata mpangilio. Nafasi ya kuuliza maswali au kujadiliana inaweza kuwepo. Kiongozi anaweza kuwapa wanafunzi fomu ya maoni waijaze au la.

#### **6. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi mahali panapotumika kutolea ushauri:**

Tunaona kwamba mfumo wa kushauri siyo tu kwamba unaokoa fedha na muda, lakini unajenga **mahuasiano** ya ajabu kati ya mshauri na mtu mzima. Tunao mpango hapa katika kanisa letu la nyumbani unaoitwa "Light Force" ulio sehemu ya ISOB. Katika mpango huo kuna wastani wa wanafunzi 60 (wenye umri wa miaka 12-14) na washauri (watu wazima) 20. Tuko katika mwaka wa nne na ni baraka kweli.

- a. Nia ni kuweza kutoa nakala za kila somo kwa kila mwanafunzi ili kwamba waweweze kwenda nazo nyumbani, wazisome huko huko nyumbani na kuleta ripoti wakati kikundi kinapokutana. Kwa kuwa masomo ya ISOB hutolewa kwa gharama naafuu au hata bure, kila mahali ambapo kuna ISOB, wanahimizwa kumruhusu kila mwanafunzi awe na masomo yake mwenyewe. Mwanafunzi anaposoma sura moja, hujaza Fomu ya Maoni ya Mwanafunzi na kumpa mshauri wake. Mshauri siyo lazima awepo wakati mwanafunzi anaposoma sura yake na kujaza fomu yake.

Ni vizuri kubadili badili masomo katika Sehemu ya "Mungu ni nani," "Kuketi," "Kuenenda," na "Kupinga." Usifanye masomo yote ya "Mungu ni nani" kabla ya kuanza somo la "Kuketi." Yachanganye.

b. (Ni lazima pawepo na mshauri mmoja kwa kila wanafunzi 3 au 5 - wanafunzi wanawenza kuwa zaidi iwo mshauri anao muda). Mshauri siyo lazima awe mwalimu au mtu aliyehitimu mafunzo katika Chuo cha Biblia. Mshauri anapaswa tu kuwa mwanafunzi wa Yesu na aliyeazimia hasa kuingia katika huduma ili kuwafikia wengine. Jambo la kukumbuka hapa ni kwamba Roho Mtakatifu na Neno katika kitabu ndio wanaofundisha, mshauri anachofanya tu ni kutia moyo na kutegemeza. Akiweza kujibu maswali, yema. Asipoweza, usiwe na wasi wasi kuhusu hilo. Tafadhalii soma masomo yaliyoambainishwa kuhusu uongozi na kushauri.

c. Kisha mshauri humjibju mwanafunzi kwa kujaza fomu ya Maoni ya Mshauri. Majibu yake yanawenza na kuwepo kwenye fomu ya Maoni ya Mwanafunzi au kwa njia ya maneno machache; au anaveza kuandika maoni yake kwenye karatasi ya kawaida. Ni vizuri mwanafunzi akitunza ripoti yake na maoni ya mshauri mahali pa salama ambapo anaweza kuiangalia wakati ujao.

d. Labda utapenda kuwa na mikutano kila wiki au nusu mwezi pamoja na washauri na wanafunzi katika eneo moja kwa ajili ya ushirika na kujifunza. Tunakutana na kikundi cha "Light Force" kila Jumapili ya kwanza na ya tatufioni.

e. Wakati mwingine ushauri unaweza kutolewa kwa njia ya barua pepe(e-mail) au kwa njia ya Posta kwa watu walio katika nchi tofauti.

f. Tunapendekeza kwamba orodha ya kupimia ya kila nusu mwezi au kila mwezi itumwe katika ofisi ya nyumbani ili tuweze kuona kazi inavyokwenda na kuiombea huduma na wanafunzi wako.

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*


## ISOB

International School of the Bible  
(Shule ya Kimataifa ya Biblia)

Inafundisha Watu Wazae Matunda kwa ajili ya Ufalme wa  
Mungu

1.a Mwanafunzi  
anasoma sura moja  
katika kitabu  
/kanda au somo la  
ISOB

2. Mwanafunzi anajaza fomu  
ya maoni na kuirudisha kwa  
mshauri wake



### Fomu ya Maoni ya Mwanafunzi

Jina \_\_\_\_\_ Tarehe: \_\_\_\_\_  
 Kitabu \_\_\_\_\_ Sura ya: \_\_\_\_\_

1. Andika hapa mambo yaliyokuvutia zaidi katika sura hii

2. Andika hapa jambo, kama lipo, unalosikia kwamba Mungu anataka ulifanye au ilitii katika sura hii. Kwa maneno mengine, Unajisikia kwamba unataka kufanya nini sasa baada ya kusoma sura hii.
3. Ni jambo gani katika sura hii unalopenda kulifahamu zaidi. Je, una maswali yoyote unayoona kwamba yanahitaji kujibowi? Andika maswali yako hapa.
4. Andika hapa maombi unayopenda tuombe pamoja nawe kwa mapatano.

*Reproduction, resale or internet posting prohibited*

# Kukua au Kufa

## Mfululizo wa Semina

Ni jambo gani lililo muhimu kuhusu agano la damu?



Kitabu cha Kukua au Kufa kitakupeleka katika agano la damu hadi  
katika uwepo wa Mungu!

### Mahitaji yetu yapo katika uwepo wake –

Katika Wafilipi 4:19 tunaambiwa kwamba “Na Mungu wangu atawajzeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.”

Mahitaji yetu na kusudi la Yesu la kuufikia ulimwengu huu yanaletwa na utaratibu wa kuzaa matunda unoaoanzia katika uwepo wake.

Kukua au Kufa ni kitabu kinachohusu jinsi ya kwenda katika uwepo wa Mungu na kuenenda katika utaratibu wa kuzaa matunda, kufuatana na mpango wa Mungu.